ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg Yahya Khamis Hamad	**Kny: Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Pili – Tarehe 19 Januari, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaanza shughuli yetu naomba nikupeni taarifa muhimu sana juu ya jambo ambalo mwenzetu Mhe. Ismail Jussa Ladhu jana aliarifu Baraza ili tuone umuhimu wa kiasi gani juu ya suala zima la eneo la Bahari Kuu ambalo kumekuwa na taarifa ya kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepeleka maombi Umoja wa Mataifa kuongeza upeo wa eneo hilo.

Tuliona uzito wake jambo hilo na umuhimu wake na kwa pamoja tukaielekeza serikali walifanyie kazi ili watupe taarifa rasmi juu ya jambo hilo kwa sababu ni suala linalohusu masuala yetu ya Muungano wetu, mnasaba na mambo ambayo tulikwishaamua kitu huko nyuma kuhusiana na masuala ya mambo ya mafuta.

Nimearifiwa hivi punde asubuhi kwamba serikali imelifanyia kazi jambo hilo na taarifa rasmi ilikuwa itolewe hapa Barazani leo hii asubuhi, lakini waziri ambaye alitegemewa atoe taarifa hiyo amepoata msiba wa kufiliwa na ndugu yake. Kwa hivyo, aliniletea taarifa mapema asubihi kwa kumtuma mjumbe kwamba amepata msiba wa kufiliwa na ndugu yake Mheshimiwa mwenzetu Waziri wa Ardhi, Maji, Ujenzi na Nishati. Kwa hivyo, tukasema kwa sababu jambo hili linaweza likawa lina maswali baadae tukubaliane kwamba jambo hilo tunaweza tukatoa taarifa pengine kesho atapokuwa yupo mwenyewe, lakini kimsingi serikali walikwisha kulifanyia kazi.

Nimeona nitoe taarifa hiyo kwa sababu hili suala lina umuhimu na uzito wake mkubwa, lakini waziri amepatwa na jambo ambalo haliwezi kuepukika. Najua serikali ipo, lakini ili pale ambapo tutakuwa na maswali ya kuweza kuuliza basi tuweze kuliweka vizuri jambo hilo na waziri aweze kujibu maswali yanayohusika na jambo hilo. Niwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe tustahamili nafikiri mpaka kesho na litaingia rasmi katika *order paper* hii ili kutoa taarifa katika vikao vyetu hivi. Nawashukuru.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 53

Upatikanaji wa Fomu ya PF3 Vituo vya Polisi

Mhe. Hija Hassan Hija (Kny.) Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza:-

Utaratibu uliopo sasa wa kuwashughulikia wagonjwa wa ajali unaambatana na kupatikana kwa Fomu ya Polisi maarufu kama PF3 form. Kuna wakati utaratibu huu hausaidii na unasababisha madhara kwa majeruhi walio katika hali mbaya.

(a) Kwa nini usiwekwe utaratibu wa kuweka Kitengo cha Polisi cha kutoa fomu hiyo katika maeneo ya hospitali badala ya kuwasimamisha majeruhi kwenye vituo vya polisi wakati inaposubiriwa fomu hiyo ili kunusuru maisha ya wale walio katika hali mbaya.

(b) Ni lini serikali kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi itaanzisha utaratibu huo wa kuharakisha taratibu za kiusalama bila ya kucheleweshwa wagonjwa kutibiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza kwa ruhusa yako naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo hii kutimiza miaka 52. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Ussi Jecha Simai swali lake Nam. 53 lenye kifungu a na b naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Spika, PF3 ni fomu ya polisi nambari 3 ambayo hupewa mtu anayehitaji kufanyiwa uchunguzi wa kidaktari, ama majeruhi baada ya kujaziwa taarifa zake muhimu pamoja na kufunguliwa taarifa za awali katika kitabu cha taarifa zinazoripotiwa kituo cha polisi ambacho hujulikana kama *report book*.

Kwa mujibu wa utaratibu uliopo Jeshi la Polisi halikatazi majeruhi kupatiwa matibabu bila ya kuwa na PF3, bali utaratibu huu unamtaka Askari Polisi mara baada ya kupokea taarifa ya ajali kufika katika eneo la ajali hiyo na kama wapo majeruhi waliopelekwa hospitali kwa matibabu askari huyo anatakiwa kufika katika hospitali husika ili kuwajazia fomu za PF3 wahusika hapo walipo. Aidha, kama majeruhi aliwahi kutibiwa kabla ya kujaziwa PF3 na bila ya polisi kuwa na taarifa atalazimika kufika kituo cha polisi na kujaziwa fomu hiyo ambayo hutumika kama ni kielelezo kwa ushahidi Mahkamani baada ya

kujaziwa na daktari husika juu ya taarifa za aina ya majeraha na kiwango cha maumivu aliyoyapata majeruhi huyo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake Nam. 53 lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kutokana na utaratibu uliopo sasa wa PF3 Jeshi la Polisi halikatazi majeruhi kupatiwa matibabu bila ya kuwa na PF3, hivyo kinachotakiwa sio kubadili mfumo bali ni kutoa elimu kwa madaktari wa jamii kuelewa utaratibu huu unavyotumika ili usiwe kikwazo kwa kutoa matibabu ya haraka kwa majeruhi.

(b) Mhe. Spika, changamoto iliyo mbele yetu ni serikali kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kutoa elimu kwa madaktari na jamii hasa kupitia mpango wake wa polisi jamii ili isionekane kuwa PF3 ni kikwazo cha kuwapatia matibabu majeruhi hao.

Mhe. Spika, kupitia Baraza lako tukufu napenda kutoa wito kwa Jeshi la Polisi kuanzia sasa mara moja kutoa elimu hiyo kwa madaktari na jamii ili kunusuru maisha ya watu wetu.

Nam. 83

Uingizwaji wa Mifuko ya Plastic Zanzibar

Mhe. Wanu Hafidh Ameir – Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kuwa Zanzibar ni nchi ya pili Afrika Mashariki katika kudhibiti utumiaji wa mifuko ya plastiki ikitanguliwa na Rwanda. Hata hivyo, juhudi zaidi bado zinahitajika ili kutokomeza kabisa utumiaji wa mifuko ya plastiki hapa Zanzibar kama ilivyo kwa wenzetu wa Rwanda.

Je, serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ina mpango gain wa kupiga marufuku uingizwaji wa mifuko mmoja mmoja kupitia wasafiri wanaoingia Zanzibar kwa njia ya Bandari na Viwanja vya Ndege vya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 83 sina budi kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupokea pongezi zilizotolewa na Mhe. Mwakilishi kwa kuziona na kuzithamini jitihada za

serikali yetu katika kuzuia suala zima la uingizwaji wa matumizi ya mifuko ya plastiki hapa nchini kwetu.

Mhe. Spika, baada ya kupokea pongezi hizo sasa napenda kumjibu Mhe. Wanu Hafidh Ameir swali lake kama ifuatavyo:-

Marufuku iliowekwa na serikali ya kuzuia uingizaji wa mifuko ya plastiki nchini haijabagua makundi ya watu, kwa maana hiyo hata wasafiri wanaoingia Zanzibar pia wana wajibu wa kutekeleza marufuku hiyo. Hivi sasa serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaendelea na mpango wake wa kuhakikisha marufuku hiyo inatekelezwa ipasavyo. Miongoni mwa mipango hiyo ni kuweka mabango ya matangazo juu ya marufuku hiyo katika maeneo mbali mbali yakiwemo ya bandarini na viwanja vya ndege ili kuwafahamisha wasafiri na wananchi kwa ujumla kuwepo kwa marufuku hiyo.

Sambamba na mabango hayo, serikali inaendelea na utoaji wa elimu kwa wananchi na wasafiri kuhusu marufuku ya plastiki. Hata hivyo, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais itaweka mkazo maalum kukutana na wasimamizi wa maeneo ya viwanja vya ndege na bandari na pia wamiliki wa vyombo vya usafiri ili kushirikiana nao katika utekelezaji wa marufuku hii.

Mhe. Spika, changamoto iliyopo hivi sasa juu ya utekelezaji wa marufuku hiyo ni kwamba kanuni ya mwaka 2008 iliyoweka marufuku ya mifuko ya plastiki ilikuwa na kasoro za kimsingi za kisheria ambazo zilikwamisha kupatikana kwa ufanisi wa utekelezaji wake. Hata hivyo, baada ya mashauriano na ofisi za Mkurugenzi wa Mashtaka, Jeshi la Polisi na Mahkama kasoro hizo zimefanyiwa marekebisho na tayari marekebisho hayo yameshachapishwa na mpiga chapa wa serikali na kufuatia uchapishaji huo wa kanuni mpya ya kusimamia mifuko ya plastiki. Serikali imeshaweka mikakati ya kuhakikisha kuwa kanuni hiyo inatekelezwa ipasavyo.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na:

1. Kuunda kikosi kazi maalum cha kufanya operesheni kinachosimamiwa na Jeshi la Polisi chini ya Mkuu wa Operesheni wa jeshi hilo. Kikosi kazi hicho kinategemewa kuanza rasmi operesheni zake hivi karibuni baada ya kukamilika upatikanaji wa mahitaji yake.
2. Kutayarisha Mahkama za Manispaa ili ziweze kutumika wakati wa operesheni zitakazofanyika mara mara baada ya operesheni hizo kuanza rasmi na

3. Kuendelea kuelimisha wananchi juu ya madhara ya mifuko hiyo na kanuni mpya ya usimamizi wa mifuko hii ya plastiki.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu washirikiane na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ili kufanikisha azma ya serikali ya kupiga marufuku mifuko ya plastiki nchini. Aidha, nawaomba waendelee kujikataza wao wenyewe kutumia mifuko hiyo pamoja na kuwaelimisha wananchi kwenye majimbo yao kwani kanuni mpya inamtia hatiani mtu yeyote yule atakayekamatwa hata kama atakamatwa na mfuko mmoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, tangu serikali kupiga marufuku mifuko hii wafanyabiashara wetu wamekuwa wakitumia mifuko ya karatasi na magazeti na kutokuwa madhubuti mifuko hiyo na magazeti bidhaa zao hadi kumwagika, hivi sasa kuna teknolojia mpya ya kutengeneza mifuko ya kuyeyuka. Je, serikali itakuwa tayari kuja mwekezaji huyo kuwekeza mifuko hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna matumizi ya mifuko mbadala ya magazeti na mifuko ya karatasi ambayo inatumiwa na wafanyabiashara wetu na inalalamikiwa na wateja wetu wengi.

Mhe. Spika, ofisi yangu imekutana na wadau wakubwa ambao ndio watakaosaidia katika kutayarisha mifuko madhubuti mbadala ambao ni wafanyabiashara kwa ajili ya kulizungumzia suala zima la wao kufanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba kunapatikana mifuko mbadala ambayo ni madhubuti. Tayari ipo kwenye soko lakini iliyopo kwenye soko nayo inalalamikiwa kwa bei zake. Kwa hivyo, bado jitihada zinaendelea na ofisi yangu haina dhamana ya moja kwa moja isipokuwa inashirikiana na wadau husika ambao ndio wafanyabiashara tuliowakabidhi shughuli hii ili kuona kwamba kunapatikana mifuko mbadala ambayo ni mizuri.

Hata hivyo, bado ndani ya jamii yetu upo mbadala kabla ya hiyo mifuko mingine kuja, watu wengi wanalalamikia matumizi ya mifuko ya karatasi kwa kutia vitu vya maji kama vitoweo vya samaki, nyama na mambo kama hayo.

Kipindi cha nyuma mwaka 2008 Mhe. Spika, marufuku hii ilipoanza wananchi wengi walijikita katika kutumia visadolin (vijidoo vya plastiki) ambavyo hivyo havijapigwa marufuku katika shughuli hiyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba mifuko hii mbadala wanaachiwa wafanyabiashara kutengeneza jambo ambalo litawaathiri sana Wazanzibari kwa upande wa bei, kwa nini Mhe. Waziri hashirikiani na Waziri wa Kazi kuandaa mpango maalum wa kutayarisha mikoba asilia ya Zanzibar ili badala ya kuwaachia wafanyabiashara tutengeneze mikoba yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kwamba nilikuwa sijataja tu mifuko mbadala yote ambayo ipo. Hivi sasa ndani ya jamii yetu mifuko hiyo anayoizungumzia ya asili ipo kwa wingi na kama alikuwa Zanzibar wakati wa ufunguzi wa *Sunday market* mifuko hiyo ilikuwepo kwa wingi sana na ipo katika maeneo yote na masokoni.

Kwa hivyo, jitihada kubwa tufanye kuwaelimisha wananchi wetu kurudi katika matumizi ya mifuko hiyo ambapo ukinunua mmoja unaweza ukautumia kwa mwaka mzima.

Nam. 39

Udhibiti wa Magendo ya Karafuu

Mhe. Hamza Hassan Juma – Aliuliza:-

Kwanza tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuongeza bei ya Karafuu na kwa kujitahidi kuweka doria ili kuzuia magendo ya karafuu.

(a) Kwa kuwa magendo ya karafuu hupitishwa baharini, serikali imechukua hatua gani kuimarisha kikosi cha KMKM katika kuhakikisha kunafanya vyema kazi zake.

(b) Je, boti ngapi zimenunuliwa kufanikisha kazi hiyo.

(c) Je, ni wavushaji magendo wangapi hadi sasa wamekamatwa tangu kuanza mwaka 2011, Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Jimbo la Kwamtipura swali lake Nam. 39 lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa kutoa pongezi hizi kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuongeza bei za karafuu. Ni imani yetu kwamba kichocheo hiki ndio kimesaidia sana kufanikisha uchumaji mzuri wa zao la karafuu na kusaidia kudhibiti au kuwafanya watu wasipeleke nje karafuu kwa magendo.

Lakini pia naomba Mhe. Spika, nitoe shukurani maalum kwa wananchi wote wa Unguja na Pemba pamoja na vikosi vyetu vya SMZ kwa kutoa ushirikiano wao mkubwa katika kukabili magendo ya zao la karafuu. Sasa baada ya utangulizi huo naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali imekiimarisha Kikosi ya KMKM kwa kukipatia nyezo muhimu ambazo huzitumia kwa ulinzi wa nchi kavu na ulinzi wa bahari kuu. Nyenzo hizo zimesaidia sana ulinzi wa kupambana na magendo ya karafuu katika kipindi chote cha msimu wa uvunaji wa zao hilo ambao unaonekana kuimarika sana.

(b) Jumla ya boti tano za ziada zimenunuliwa na serikali ambazo zinatumika kuimarisha ulinzi wa doria katika pwani ya visiwa vya Unguja na Pemba.

(c) Jumla ya matukio mawili yaliripotiwa na kuthibitishwa tangu kuanza kwa mwaka 2011 yanayohusiana na magendo ya karafuu ambapo jumla ya magunia 151 ya karafuu yenye ujazo wa kilo 6693 zenye thamani ya shilingi 37,039,500 yamekamatwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza namshukutu Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pamoja na hayo naomba kumuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kwamba katika kukiimarisha kikosi cha KMKM katika udhibiti wa suala la magendo wameweza kununua boti tano na kimsingi boti hizo sio kama zimenunuliwa kwa kudhibiti magendo tu, lakini tunajua kwa mujibu wa majukumu ya kikosi hicho kina kazi ya kuweka ulinzi katila maeneo ya baharini.

Swali, Mhe. Spika, pamoja na hizo boti tano zilizonunuliwa lakini bado serikali haioni kama kuna haja ya kikosi hiki cha KMKM sasa hivi kupatiwa helkopta ambayo itaweza kusaidia kufanya kazi kubwa zaidi ukiacha ya kudhibiti magendo, lakini vile vile hata yanapotokea majanga kuweza kugundua.

Pili, Mhe. Spika, tunawashukuru sana wananchi kwa katika kipindi hiki baada ya serikali kuongeza bei ya zao la karafuu magendo kidogo yamepungua, lakini bado pamoja na hayo kuna dalili sasa ya magendo kutaka kurudi tena hasa baada ya kuona kwamba wananchi karafuu zao baada ya kwenda kuuza sasa hivi wanakuwa wanakopwa.

Je, serikali ina mpango gani sasa hivi ili kuona baada ya wananchi kuuza karafuu zao wanalipwa kwa haraka ili wasivutiwe na wale wafanyabiashara wa magendo kwa sababu wao wanalipa *cash* kwa *cash*.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kabisa kwa wazo zuri alilotushauri la kutafuta helkopta kusaidia ulinzi wa doria katika pwani zetu. Nafikiri hilo ni suala zuri lakini kwa sasa hali yetu ya uchumi bado hatujawanayo. Nafikiri lazima tukubali gharama ya ndege ya helkopta ni kiasi gani, lakini Tanzania nzima au Afrika Mashariki nzima…*(Makofi)*

Mhe. Spika: Nasema tuweke utaratibu, waziri akisema mkipiga makofi maana yake majibu yale yatakuwa hayasikiki itakuwa sio utaratibu mzuri na ile haja ya suala la nyongeza la Mheshimiwa litakuwa limeelea tu. Kwa hivyo, nadhani makofi tupige kwa utaratibu na jambo hili tunaambizana kwa muda mrefu kidogo. Mheshimiwa endelea.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Nakushukuru kwa muongozo wako Mhe. Spika. Nilikuwa naomba kusisitiza tu kwamba gharama za helkopta ni kubwa sana na mfano mzuri kuongesha kuwa gharama zake ni kubwa na umiliki wake si rahisi tuhesabu kwa Tanzania nzima au Afrika Mashariki nzima kuna helkopta ngapi. Mimi ninavyoziona machoni tu nashukuru *Alhamdulillah,* viwanja vya ndege vingi vya Afrika Mashariki nimesharanda sifikiri kama zinatimia kumi, pale Dar es Salaam naiona moja tu ya polisi ndio inayofanya kazi.

Kwa hivyo, hii inaonesha kwamba hili suala sio rahisi ni gumu sana. Lakini tunashukuru sana kama nilivyozungumza wako watu au kampuni binafsi wanazo helkopta na pia kuna ulinzi shirikishi kwa kutumia chombo chetu cha *SADC* wanayo helkopta moja ambayo inatusaidia ulinzi katika bahari kuu.

Nafikiri helkopta hiyo itazidi kutusaidia kuweza ku-*monitor* suala la ulinzi katika nchi yetu. Lakini kwa ujumla kama nilivyosema helkopta ni ghali na kwa hivi sasa serikali haina mipango hiyo kwa ughali wake.

Kuhusu kukopwa wananchi kwa kweli sijapata taarifa ya kwamba kuna wananchi wanakopwa kwa kuuza karafuu zao. Serikali inajitahidi kununua karafuu zote na hata kama wamepungukiwa *ZSTC* basi ina mipango ya kupata fedha zaidi imeshafanywa na kwa kweli hatujasikia, kama imetokezea labda pengine kutwa moja lakini jioni wanapata, kwamba zitoke huku pesa ziende huko, lakini kama imetokezea kukopwa kwa kweli hatujalipata. Nazidi kuthibitisha kwamba kwa hili serikali imejidhatiti, tumesema hata kama karafuu itapunguka bei katika soko la ulimwengu sisi huku hatutopunguza bei, tutanunua kwa bei ambayo tumeiweka kwa wananchi wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kidogo niongezee katika lile swali lililoulizwa na Mhe. Hamza Hassan.

Mhe. Spika, serikali imeandaa utaratibu mzuri wa kuweza kupata pesa kwa ajili ya kununua karafuu za wananchi Unguja na Pemba. Hivi sasa tayari serikali imeshatumia shilingi 60 milioni kwa ajili ya kununua karafuu na kwa taafira tu Mhe. Spika, tumeandaa mipango kutoka *ZSSF* pamoja na Benki yetu ya Watu wa Zanzibar ili kuipatia fedha *ZSTC* pale itakapoishiwa na kwa habari ambazo zimezipata jana tayari *ZSTC* kwa jana na juzi na juzi wameshauza tani 150 ns pesa wanazp za kutosha ili waweze kununua karafuu za wananchi.

Mhe. Salum Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la mwisho kabisa la nyongeza kwa suala hili. Mhe. Waziri katika kutoa majibu ya kifungu (c) alisema kuna matokeo mawili ya magendo yaliyokamatwa na katika matokeo hayo jumla ya gunia 1151 zilikamatwa na thamani yake ni shilingi 37.395 milioni.

Swali la kwanza, kwa sababu karafuu zimeongezwa bei maradufu kabisa na serikali ilifanya makusudi ili kuzuia watu wasisafirishe karafuu kwa magendo. Kwa bei hii kubwa serikali iliyoweka kwa makusudi tumefanya utafiti gani mpaka ikawa watu bado wananunua karafuu kwa magendo na mtu hawezi kununua karafuu kwa magendo kama kule anakouza hapati bei zaidi.

Mhe. Spika, swali la pili ni nani na nani waliokamatwa katika matukio haya mawili na adhabu gani wamepewa.

Mhe. Spika, la mwisho kama Mhe. Waziri alivyosema kuwa hana habari ya kuwa serikali inakopa watu katika karafuu zao wanazonunua. Kukopa maana yake ni mtu kuleta mali yake ukamwambia pesa njoo uchukue kesho au kesho kutwa, hakuna *definition* nyengine.

Kwa hivyo, inaweza ikatokea labda wanapeleka pesa kidogo kituoni kuliko karafuu tunazoleta. Tunaomba basi serikali ipeleke pesa za kutosha ili iondoke balaa hii ya kukopwa pesa zao kwa kuuza karafuu zao na hata makonyo limeshatokea suala hili.

Mhe. Spika: Maswali yamekuwa marefu sana ingawa nilipendekeza yawe mafupi. Mhe. Waziri majibu lakini kwa ufupi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza umefanywa utafiti gani kuhusu magendo. Kwa kweli tumefanya utafiti huko nyuma na tulichogundua kwamba kubwa sana kwa wakati ule ilikuwa bei wanayolipwa wakulima ilikuwa ndogo. Sasa baada ya kuimarika bei katika soko la dunia na sisi tukaona tupandishe bei na ndio maana magendo yakapungua.

Mhe. Naibu Spika, mbali ya hivyo kuna watu wana utashi tu hawana *analysis* ya bei na uchumi, anaona atakwenda Kenya atapata bei zaidi, lakini hata hapati bei zaidi pengine anapata hasara hasa ukiangalia hizo gharama zake. Wao wenyewe sasa wamegundua kwamba wakipeleka Kenya kwanza hizo *risk* za kusafirisha na kule bei watakayoipata haihalisi na ndio maana wameacha.

Mhe. Naibu Spika, hili la nani na nani waliokamata, wapo waliokamatwa na wameshafikishwa katika vyombo vya sheria, taarifa sasa hivi hapa sina tu lakini baadae naweza kuzitafuta.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa pesa kidogo kupelekwa vituoni. Namshukuru Mhe. Mwakilishi kwa ushauri wake na hili kama nilivyosema na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kazidi kusisitiza pesa za kutosha zipo, tutajitahidi sasa vituo vyote vipate pesa za kutosha karafuu zote za wananchi zinunuliwe.

Nam. 56

Shughuli za Shirika la Bima la Zanzibar Nje ya Zanzibar

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:

Nalipongeza sana Shirika la Bima la Zanzibar kutoa huduma zake hapa Zanzibar hadi huko Tanzania Bara: Arusha, Mwanza, Mbeya n Dodoma.

(a) Je, Mhe. Waziri Shirika linamiliki majengo yake huko Tanzania Bara.

(b) Kama hawana majengo Shirika limejipanga vipi kumiliki rasilimali hiyo.

(c) Kwa kuwa mwelekeo wa sasa ni kwenda ki-Afrika Mashariki Shirika linajipanga vipi katika ushindani wa soko la Afrika Mashariki.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 56 lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, Shirika la Bima la Zanzibar hawana jengo wanalomiliki huko Tanzania Bara.

(b) Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Bima ya mwaka 2009, mashirika ya Bima hayatakiwi kumiliki majengo mengi. Hata hivyo, Shirika la Bima la Zanzibar linatafuta kiwanja huko Dar es Salaam kwa ajili ya kutekeleza mpango wake wa kuwa na jengo la ofisi.

(c) Mhe. Spika, ni kweli soko la Afrika Mashariki litakuwa na ushindani mkubwa katika shughuli mbali mbali zikiwemo za Bima. Kutokana na hali hiyo, Shirika la Bima la Zanzibar linaendelea na utafiti utakaosaidia kutoa matokeo ya jinsi ya kuingia katika soko la Afrika Mashariki. Shirika pia limepanga kuajiri wataalam wa fani ya Bima wenye uzoefu wa kimataifa pamoja na kutoa huduma kwa kutumia mawasiliano ya kisasa. Kukamilika kwa mpango huo kutasaidia sana katika kukabiliana na ushindani ndani ya soko la Afrika Mashariki.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri katika jibu lake mama amekiri kwamba Shirika la Bima halijamiliki majengo Tanzania Bara. Je, Mhe. Waziri ni kiasi gani cha fedha kinachotumika katika kukodi majengo haya.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, Shirika la Bima la Zanzibar limekodi jengo Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma na Mbeya. Kwa sababu majengo haya yana kodi tofauti naomba nimpatie baadae ili aweze kuona kodi tunazotoza katika majengo hayo yanayotumiwa na Shirika la Bima.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba hivi sasa hiyo sheria iliyokuwepo imepitwa na wakati. Je, kama ni hivyo Mhe. Waziri, huoni kuwa tuilete sheria hapa kurekebisha na kuweza kuokoa fedha za wavuja jasho.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nikubaliane nae kimsingi kwamba sheria yoyote inayopitwa na wakati inapaswa kufanyiwa marekebisho. Lakini kwa Sheria ya Bima haijapitwa na wakati kwa sababu zifuatazo.

Bima ni fedha za wananchi na fedh zile kwa kiwango kikubwa hazitakiwi kuwekezwa zinatakiwa ziwepo wananchi wanapopata matatizo ili waweze kufidiwa kwa wale ambao wameweka bima. Kwa sheria hii bado haijapitwa na wakati vyenginevyo ukiwaruhusu mashirika ya Bima kujenga majengo. Sote ni mashahidi Shirika la Bima la Taifa lilipata matatizo ilibidi *asset* zake waanze kuziuza ili kulipa bima za watu walioweka bima zao.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika kuingia katika ushindani wa Afrika Mashariki mashirika ya Bima sasa hivi yamejikita katika huduma ya bima ya afya. Je, kwa upande wa Zanzibar shirika letu liko wapi kwa agenda hii. Lakini swali (b) yapo mashirika hivi sasa ambayo hutembea na fedha katika mikoba yao ili kuondosha urasimu wa huduma ya bima. Naomba kujua kwa shirika letu hali ikoje.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza shirika letu sasa hivi liko katika utafiti mzito kuweza kujua ni kwa kiwango gani linaweza likashiriki katika bima ya afya.

Kwa sababu Mhe. Spika, bima ni fedha za watu, unaweza ukaanza kufungua ikawa wewe unakula hasara. Sasa wamo katika utafiti kuangalia bima za afya, kuangalia mahospitali gani ambao watapeleka wagonjwa wao. Baada ya utafiti huo na wao watatupa maelezo serikalini kwamba tunaweza tukaingia katika bima ya afya au hatuwezi. Lakini la pili hali ya mfuko wa Shirika letu la Bima nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba mfuko wetu ni mzuri na Shirika la Bima la Zanzibar linafanya kazi vizuri.

Nam. 15

Punguzo la Ushuru kwa Vyombo vya Usafiri wa Anga na Baharini

Mhe. Salma Mussa Bilal – Aliuliza:

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza ushuru wa vyombo vinavyosafirisha abiria wanaotumia vyombo hivyo ili kuvutia wawekezaji kuwekeza katika sekta hiyo na kupunguza tatizo la usafiri katika maeneo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 15 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, vyombo vya kusafirishia abiria viko aina nyingi mfano gari, meli, ndege, reli na kadhalika kwa mujibu wa Sheria Nam. 11 ya 2004 ya *ZIPA* imetoa fursa ya kusamehe kodi kwa mwekezaji anayetaka kuwekeza hapa Zanzibar katika maeneo mbali mbali yakiwemo ya usafiri na usafirishaji. Mwekezaji awe mgeni au mwenyeji kama atasajiliwa chini ya Sheria ya *ZIPA* atapata fursa za misamaha ya kodi. Vitu ambavyo vimepewa msamaha wa kodi ni pamoja na mashine, malighafi na vyombo vya kusafiria abiria vinapoingizwa nchini kwa mara ya kwanza. Vile vile mwekezaji anaweza kufaidika kutolipa kodi ya mapato ya makampuni *corporate tax* kwa kipindi cha miaka kumi ya awali kama atawekeza chini ya utaratibu wa maeneo huru.

Mhe. Spika, kwa utaratibu huo serikali tayari imeshatoa unafuu wa kodi mbali mbali kwa vyombo vinavyosafirishia abiria kama vyombo hivyo vinanufaisha umma badala ya mtu mmoja mmoja. Kwa vyombo vya mtu mmoja mmoja vinapaswa kulipiwa kodi kama ni sehemu ya mchango wao katika maendeleo ya nchi.

Nam. 50

Marekebisho ya Mshahara katika Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Mhe. Hamza Hassan Juma - Aliuliza**:**

Hivi karibuni Serikali imeongeza kiwango cha mishahara kwa kuzingatia vigezo mbali mbali ikiwemo elimu, lakini inaonesha viwango hivyo havikuzingatiwa kwa askari wenye viwango vya Diploma na Post Graduate Diploma.

(a) Je, suala hilo ni kweli.

(b) Kama ni kweli ni sababu gani zilizopelekea askari wetu wenye elimu kukosa haki yao ya kulipwa kwa mujibu wa elimu yao.

(c) Ni hatua gani zitachukuliwa kurekebisha suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 50 (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli kuanzia mwezi wa Oktoba, 2011 Serikali imeongeza viwango vya mishahara kwa kuzingatia vigezo mbali mbali ikiwemo elimu.

Ingawa kabla ya marekebisho haya askari kwa upande wao walikuwa na utaratibu wa kulipana mishahara kwa mujibu wa vyeo walivyonavyo badala ya elimu na walipenda utaratibu huo uendelee. Hata hivyo, baada ya mashauriano ya vikosi vyenyewe kuhusu umuhimu wa kuzingatia elimu, mtazamo huo ulibadilika na kukubaliana kama ifuatavyo:

(a) Kwamba sasa utaratibu maalum umeandaliwa ambapo askari wenye sifa za kielimu wanalipwa sawa na wenzao wenye sifa kama zao walioko katika mawizara na taasisi mbali mbali za serikali.

(b) Katika hali hiyo hivi sasa askari wetu nao wanalipwa kwa mujibu wa elimu yao.

(c) Hakuna hatua za kuchukuliwa kwa vile suala hili limekwisha shughulikiwa.

Nam. 1

Fursa ya Watu wenye Ulemavu kutoa Maoni

Mhe. Raya Suleiman Hamad - Alijibu**:**

(a) Mhe. Waziri kuna utaratibu gani ulioandaliwa ambao utawawezesha watu wenye ulemavu kuweza kutoa mapendekezo yao kwenye marekebisho ya Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Je, Mhe. Waziri, huoni kwamba wakati umefika sasa wa kuingizwa Haki na Fursa ya watu wenye ulemavu kwenye Katiba.

(c) Tarehe 12 Oktoba, 2006 Baraza la Wawakilishi lilipitisha Sheria Nam. 9 ya 2006 ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa). Sheria hiyo haiwezi kufanya kazi pasipokuwa na Kanuni. Je, Wizara yako imefanya jitihada gani kuandaa Kanuni hizo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 1 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

1(a) Kwa mujibu wa kifungu cha 12(1) cha Katiba ya Zanzibar sambamba na ibara ya 13(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinaelezea bayana kuwa "watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupatiwa haki sawa mbele ya sheria". Vile vile kifungu cha 10(e) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinasisiza kwa kusema kwamba:

"kila raia atakuwa na haki sawa, majukumu na fursa sawa kwa mujibu wa sheria, utu wa mtu utaheshimiwa na heshima ya mtu itaenziwa na kuendelezwa."

Kwa mantiki hiyo basi, muda huo utakapofika wa wananchi kutoa mapendekezo yao, kila mmoja wetu atapata fursa sawa na kushiriki na kutoa mapendekezo yake kwa utaratibu utakaopangwa ambao utamuwezesha kila mmoja kuweza kuitumia haki na fursa hiyo kikamilifu. Serikali itahakikisha inaweka utaratibu bora wa kuwawezesha watu wenye ulemavu wote kushiriki kikamilifu na kutoa mapendekezo yao kwenye Tume ya kupokea maoni ya kurekebisha Katiba. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa utaratibu mzuri utafanywa kwa kumpa fursa hat mlemavu ambaye hawezi kusema, au hasikii au aliyekuwa haoni ili nae aweze kuchangia katika suala hili muhimu. Kwa sababu kazi ya kukusanya maoni ni ya Tume itakayoundwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kushauriana na kukubaliana na Mhe. Rais wa Zanzibar. Napena nilihakikishie Baraza lako Tukufu kuwa maoni haya mazuri tutayafikisha katika Tume hiyo kwa kuzingatiwa.

1(b) Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inatambua kabisa kuwepo kwa haki na fursa za watu wenye ulemavu. Haki na fursa zinatolewa kwa

wananchi wote bila ya upendeleo wowote. Kama nilivyosema kifungu cha 12(1) kinathibitisha hilo.

Pia kifungu 12(5) kinafafanua zaidi kwa kueleza bayana maeneo ambayo yametajwa kuwa ubaguzi huo usifanywe kwa kisingizio cha ukabila, jinsia, ulemavu, rangi au dini." Kifungu cha 10 (g) cha Katiba ya Zanzibar vile vile kimetoa upendeleo kwa watu wasiojiweza, wazee, wagonjwa na walemavu, naomba ninukuu.
"Kwa mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi ana fursa ya kufanya kazi na kwamba msaada utatolewa kwa wale wasiojiweza, wazee, wagonjwa, watoto na walemavu."

Hivyo ni dhahiri kwamba haki na fursa kwa watu wenye ulemavu zinatambulika na kulindwa na Katiba yetu ya Zanzibar na hata ile ya Jamhuri ya Muungano. Kwa maana hiyo, hakuna haja tena ya kuingiza haki hizo na fursa kwa watu wenye ulemavu katika Katiba kwa sababu Katiba zetu zote mbili zinakidhi haja hiyo.

1(c) Kifungu cha 47 cha Sheria Nam. 9/2006 ya Watu wenye Ulemavu (Haki na Fursa) kinampa uwezo Waziri mwenye dhamana juu ya mambo ya walemavu chini ya kifungu 47 cha sheria hii kutengeneza kanuni ambazo zitaweka utaratibu bora wa matumizi ya masharti ya sheria hiyo. Waziri mwenye dhamana na mambo ya watu wenye ulemavu kwa hivi sasa ni Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Kwa maana hiyo, mamlaka hayo ya kufanya kanuni hayapo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Hata hivyo, kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe, naomba muelewe kwamba sheria hii inafanyiwa mapitio ili iweze kukidhi mahitajio zaidi ya watu wenye ulemavu, na kwamba Wizara husika yaani Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais hivi sasa inaandaa sera ya watu wenye ulemavu ili iweze kujadiliwa na kukubaliwa. Pia ni vyema tukaelewa kwamba sheria inaweza kutekelezwa bila ya kuwepo kwa kanuni, kwani sheria huwa inaelezea mambo yote ila pale inapohitajia ufafanuzi zaidi ndio Kanuni hutungwa kama kisaidizi.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri lakini haoni kucheleweshe kanuni hii kwa watu wenye ulemavu ni kuwanyima haki na fursa ya kufanya kazi zao kwa upana kabisa na ufanisi. Kwa sababu watu wenye ulemavu wana matatizo kama tunavyojua kudhalilishwa, kutelekezwa na mambo mengine. Sasa tunamuomba Mhe. Waziri atusaidie.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo hivi sasa sheria ipo na utaratibu huo unatekelezwa na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Lakini Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais iliona kwamba ipo haja ya kurekebisha au kupitia tena sera hiyo ya walemavu na ndio maana hivi sasa inafanya jukumu hilo ili kuziweka vizuri zaidi fursa hizi na kanuni hizi. Kwa maana hiyo, mpaka hapo ambapo utaratibu huu utakamilika bado naomba tutumie sheria ile ile pamoja na kanuni zile zile na tukishirikiana na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais tutahakikisha kwamba matatizo ya walemavu yanashughulikiwa kwa mujibu wa utaratibu ulivyo hivi sasa.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa walemavu na wao wana haki sawa katika taifa lao. Je, Mhe. Waziri atatwambia ni lini sheria hiyo. Kwa kuwa toka tuko jengo la zamani la Kikwajuni tulikuwa tunaulizia matatizo ya walemavu yatatatuliwa lini kwa sababu na wao wana haki sawa na binaadamu katika haki yao.

Je, watatuhakikishia ni lini sheria hiyo au sera hizo zitapitiwa lini na kuleta sheria ili kuhakikisha kwamba na wao wanapata haki zao.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza napenda aelewe kama nilivyosema mwanzo suala la walemavu haliko katika Wizara ya Katiba na Sheria, suala la walemavu liko katika Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

La pili nilisema kwamba kwa mujibu wa katiba pamoja na sheria zilizopo hivi sasa walemavu wanashughulikiwa kwa utaratibu huo. Pia nilisema kwamba kweli serikali imeona kwamba kuna haja ya kuimarisha zaidi uhuru wa walemavu na ndio maana nikasema sera ya walemavu inajadiliwa upya na baada ya kujadiliwa sera bila shaka kama kutahitajika marekebisho ya sheria iliyopo basi itafanywa hivyo.

Kwa maana hiyo, napenda nisisitize kwamba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inashughulikia hiyo na pale ambapo watakuwa tayari basi bila shaka sera hiyo itatolewa na kama kuna uhitaji wa kurekebishwa sheria basi sheria nayo pia itarekebishwa kwa faida ya ndugu zetu walemavu.

Nam. 9

Ukusanyaji wa Taarifa za Vyama vya Ushirika

Mhe. Salma Mussa Bilal - Aliuliza**:**

Idara ya Ushirika imekabiliwa na zoezi gumu la ukusanyaji wa taarifa za vyama vya ushirika vya Unguja na Pemba *(Data Base).* Watendaji wa zoezi hilo wanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo upungufu wa wafanyakazi na wataalam, uhaba wa vitendea kazi na kadhalika.

Je, Wizara ina mpango gani wa kusaidia na kutia nguvu kufanikisha zoezi hilo.
Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli Wizara yangu kupitia Idara ya Ushirika imepanga kuvihakiki vyama vyote vya ushirika vilivyopo, ili kujua hali ya mitaji, uwezo wao na changamoto zinazovikabili vyama hivyo.

Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba zoezi la ukusanyaji taarifa za vyama vya Ushirika lililokwisha anza ni gumu na limekabiliwa na changamoto nyingi baadhi yake ni kama alizozitaja. Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika imechukua hatua kadhaa zikiwemo, kuchukua watendaji kutoka Idara mbali mbali ndani ya Wizara, ili kuongezea nguvu zoezi hilo. Aidha, shughuli hii imeingizwa katika mpango wa Wizara kwa mwaka 2011/12 na imetengewa bajeti yake.

Mhe. Spika, zoezi hili tayari limeshakamilika kwa Wilaya nne za Zanzibar ambazo ni Wilaya ya Mjini na Magharibi kwa Unguja na Wilaya ya Micheweni na Mkoani kwa upande wa Pemba.

Taarifa zilizokusanywa zinaonesha kuwepo idadi ndogo ya vyama vya Ushirika kuliko inavyosomeka kwenye madaftari ya usajili, ambapo kati ya vyama 2,021 vilivyotarajiwa kuhakikiwa ni vyama 576 tu ndivyo vilivyoonekana na kuhakikiwa. Idadi hii ni sawa na asilimia 28.5 kwa Wilaya nne. Hivi ndivyo vyama ambavyo viko hai na vinaendelea kufanya kazi katika Wilaya hizi nne.

Mhe. Spika, ili kulipa nguvu zoezi hili, tumeshirikiana vyema na Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* ambao wametusaidia kutupatia mtaalam wa kusaidia uendeshaji wa zoezi hilo pamoja na *computer* zitakazotumika katika uwekaji wa mfumo wa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya vyama vya ushirika. Naomba kutoa shukurani za dhati kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Shirika la *ILO* kwa msaada walioutoa, lakini pia kwa wadau wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine kulifanikisha zoezi hili hadi hapa tulipofikia.

Tunategemea kukamilisha zoezi hili kwa nchi nzima ifikapo mwezi Februari, 2012.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika utekelezaji wa mpango wa serikali wa kupunguza umaskini moja wapo ni kuanzisha vyama vya Ushirika vilivyo imara na madhubuti. Lakini katika hali isiyo ya kawaida katika majibu yake Mhe. Waziri ameeleza kwamba kati ya vyama 2,021 ni vyama 576 sawa na asilimia 28.5 ndio vilivyo hai.

Je, Mhe. Waziri atatueleza ni tatizo gani ambalo linasababisha hali hali na wizara yake ina mpango gani ili kuweza kunusuru hali hii ya kufa hivi vyama vya Ushirika ili vyama viweze kurudi katika hali yake ya kawaida na viweze kuwasaidia wananchi na lengo la serikali liweze kutimia.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, tumekuwa tukilieleza hili katika maswali ambayo yameulizwa huko nyuma mara nyingi kwamba vyama vya Ushirika hivi vilivyoanzishwa vilianzishwa tu kwa sababu watu walitaka kuanzisha vyama hivyo kwa sababu mbali mbali. Pengine walianzisha kwa matakwa yao, kwa hisia zao tu wawe na vyama vile, lakini hata utaratibu wao wa kuanzisha vyama kama hivyo hata hivi sasa vinaendelea.

Sisi viongozi tumo humu ndani huko vijijini na kwenye mitaa yetu wananchi wanakuja wanavita vikundi vya ushirika. Lakini huwezi kuanzisha vikundi tu mpaka uhakikiwe, tuje tuangalie taaluma zilizokuwepo na uongozi uliokuwepo, kwa hivyo huko nyuma tatizo hilo halikuangaliwa vizuri. Kwa hivyo, tunachojitahidi sasa hivi ni kuhakikisha kila chama ambacho kinaanzishwa cha ushirika au vyama vya ushirika watendaji wake na viongozi wake tunawapatia mafunzo ya kutosha ili waweze kuvisimamia vyama hivyo.

Mhe. Spika, katika uhakiki tuliofanya ilikuwa tuhakiki vyama 2,021 kama nilivyosema, lakini tumevikuta vyama vya ushirika vimekufa, viko ambavyo viko ICU vinangojea matibabu hali ni mbaya sana. Sasa kuvitia roho vile sio kazi ndogo na kuvipatia matibabu hivi vyengine pia sio kazi ndogo. Lakini tumejipanga katika bajeti yetu hii ya mwaka 2011/2012 *Inshaallah* basi tutaviimarisha vyama hivyo ili vilete tija ile ambayo imekusudiwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru sana. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize swali moja tu la nyongeza Mhe. Waziri. Kwa kuwa uhakiki wa vyama hivi ni kujaribu kupata taarifa na kuzifanyia kazi. Je, ni mpango gani uliopangwa wa kuweza kuviimarisha ili badala ya vile 2,021

vilivyokufa angalau hivi 500 viweze kufufuka au ni taarifa tu zitakaa kwenye kompyuta.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, naomba kumjibu rafiki yangu Mhe. Rashid Seif swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, napenda nimuhakikishie Mhe. Mjumbe pamoja na wajumbe wote wa Baraza hili lako tukufu kwamba haitokuwa kuhakikiwa na baadae kukaa kwenye kompyuta vyama vile ikawa tunaviangalia tu. Lengo ni kuviwezesha, ukishavipatia mafunzo vyama hivi yaani viongozi wake wakishapata mafunzo ili kuweza kujitegemea na kufanyakazi kwa makini zaidi na kusaidia ajira kwa sababu wizara yangu inakusudia kuongeza ajira kwa kupitia vyama vya ushirika, huwezi kuongeza ajira kama vyama hivi hatujaviwezesha.

Mhe. Spika, tunajipanga na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akipenda katika mwezi wa April kuna mfuko maalum utaanzishwa kwa lengo hilo hilo, fedha hizo zitasaidia vyama vya ushirika, kwa wale ambao wanafanya shughuli za kilimo watawezeshwa kwa upande wa kilimo, wanaofanya shughuli za uvuvi watasaidiwa kwa upande wa uvuvi na wanaofanya biashara zao nyengine mbali mbali tu basi tutawasaidia vile vile. Hatutoviwacha kwenye kompyuta namuhakikishia Mhe. Rashid Seif tutaviwezesha na ndio kazi ya wizara hii.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza rafiki yangu swahib yangu Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa ziara zake alizozifanya katika wilaya zetu mbali mbali kwenda kuhamasisha wananchi ili kuanzisha vikundi vya ushirika ili serikali iweze kuwa karibu nao na kuweza kuwasaidia.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Waziri katika usajili wa vyama vya ushirika vimesajiliwa karibu orodha ya vyama 2,028. Lakini bado uhakiki wamegundua kwamba vyama vilivyokuwa hai ni vyama 500 tu na hivyo vyama 500 vyengine vinasua sua, vyengine viko ICU na vyengine kidogo ndivyo ambavyo vinajiendesha.

(a) Mhe. Waziri huoni kwamba iko haja sasa hivi, badala yakupita kuhamasisha wananchi waendelee kujisajili katika kuunda vyama vyengine vya ushirika, lakini huoni kwamba ilikuwa iko haja kwanza ya kuviimarisha na kuvifufua hasa hivi 500 ambavyo tayari vimeonekana viko hai.

(b) Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri swali hilo Mhe. Waziri kwa sababu mimi katika jimbo langu tayari kuna SACCOS ambayo yeye mwenyewe Mhe. Waziri anaijua. SACCOS ya Jimbo la Kwamtipura, ambapo sasa hivi ni mwaka wa tano na unaelekea mwaka wa sita tayari wameshajisajili wamepata mafunzo na bado hawajapata ruzuku yoyote au mkopo wowote kutoka serikalini au taasisi nyengine yoyote.

Mhe. Spika: Swali.

Mhe. Hamza : Je, haoni iko haja kwanza baada ya kuendelea kuwahamasisha wananchi wetu, kila siku kutudai Shs. 100,000/= kwa ajili ya kusajili vyama vyengine, kwanza angala akaanza kusaidia vile mbavyo vimeshasajiliwa na vimepata mafunzo ili na wale wengine waendelee kupata moyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, maswali yote haya mawili nitayajibu kwa pamoja, kwa sababu yote yanahusiana. Kwanza napenda nimuhakikishie kwamba hilo ndio lengo.

Vile vyama ambavyo tayari vimeimarika vinamuelekeo basi hivyo tutaviimarisha na kuvipa nguvu. Napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba hata ushirika wake huo uliokuwepo Kwamtipura ni miongoni mwa SACCOS ambazo tumezipa kipaumbele.

Mhe. Spika, kumetokea tatizo na napenda niliseme hapa ili wajumbe wako walisikie. Mikopo ya AK JK hii, muda mrefu hivi sasa haijatoka na kutokana na urasimu ambao umekuwepo hapo nyuma, tumebadilisha utaratibu sasa hivi kwamba tumepunguza urasimu na wizara yetu itakuwa moja kwa moja inahusika katika utowaji wa mikopo hiyo.

Pia kuna mazungumzo ambayo yanaendelea na yamefikia hatua nzuri kwamba fedha zile sasa lakini kwanza itabidi lazima taratibu za kisheria zifuate kama vile mwanzo tulivyoamua kuwa pesa hizi tukazipeleka Benki ya Watu wa Zanzibar ili zikae kule na wao ndiowenye uwamuzi wa mwisho.

Sasa tuna utaratibu ambao tumekaa tukafikia kwamba sasa fedha zile zisimamiwe na wizara wenyewe moja kwa moja ili kurahisisha utaratibu wa kutoa mikopo hiyo. Kuna mikopo kama 200 hivi sasa iko PBZ imekwama, miongoni mwa walioomba nina uhakika ni wananchi wa Jimbo hilo la Kwamtipura.

Kwa hivyo, tunakamilisha taratibu hizo haraka sana. Sio ule utaratibu ambao jana mheshimiwa mmoja alisema tuko mbioni tunafuatilia tunakaa. Sisi

tukisema tunalifanyia kazi basi tunalifanyia kazi wala hatulikalii kitako kwa sababu ukilikalia kitako halitokuja juu, tutalisimamia ili tuhakikishe kwamba tunalifanyia kazi haraka iwezekanavyo.

Nam. 10

Ushirikiano Baina ya Wizara ya Kilimo Zanzibar na Wizara ya Kilimo na Ushirika Tanzania Bara

Mhe. Salma Mussa Bilal – Aliuliza:-

Miaka ya nyuma Wizara ya Kilimo ilikuwa na ushirikiano na Wizara ya Kilimo na Ushirika ya Tanzania Bara, kwa kupitia ushirikiano huo, wizara iliweza kusomesha maafisa ushirika kadhaa katika Chuo cha Ushirika Moshi kwa ufadhili wa Wizara ya Ushirika ya Tanzania Bara.

Je, wizara yako inaendelea na mpango huo. Kama unaendelea nafasi ngapi zimetengwa kwa mwaka huu wa masomo, kwa ajili ya wanafunzi wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake namba 10 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli hapo nyuma kulikuwa kuna mashirikiano na Wizara ya Kilimo ya Tanzania Bara, kusomesha maafisa wa ushirika kwenye Chuo cha Ushirika Moshi. Mara ya mwisho kufaidika na mpango huo ni mwaka 2009/2010, ambapo afisa wetu mmoja alipatiwa ufadhili wa masomo kwa ngazi ya cheti katika fani ya *Microfinance* huko Chuo cha Ushirika Moshi.

Kwa mwaka huu hatukupatiwa nafasi yoyote na inawezekana ni kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo kwa kutumia bajeti yake wizara itaendelea na juhudi ya kuongeza uwezo kwa wafanyakazi wake, wakiwemo maafisa wa ushirika wawili ambao wanaendelea kupatiwa masomo katika Chuo cha Ushirika Moshi.

Aidha, katika kuimarisha mashirikiano na taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wizara yangu imeshafanya mawasiliano na wizara inayoshughulikia masuala ya ushirika na nyenginezo zinazohusiana na hizo kwa lengo la kuendeleza mashirikiano katika nyenja mbali mbali.

Tumekusudia kuwasilisha hoja ya kufufua na kuendeleza mpango huu wa mashirikiano ya mafunzo kwa wenzetu kwa Wizara ya Kilimo na Ushirika wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kama ni hoja mojawapo katika ajenda za vikao vyetu vya mashirikiano tunavyotegemea kuvianzisha.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Spika, mpango huu wa ushirikiano ni mzuri na ulisaidia sana maafisa wa vyama vya ushirika katika kupata mafunzo huko Tanzania Bara, umetueleza kuwa hizi hatua zinachukuliwa ili kurejesha ushirikiano ule.

Je, hatua hizo zimefikia wapi kwa hivi sasa za mpango huo wa mashirikiano katika hizi taasisi ulizosema na lini utaanza huo mpango ili maafisa wetu waendelee kupata mafunzo kule na watakaporudi waweze kuanzisha vyama vya ushirika vilivyo imara na madhubuti, ambavyo havitatetereka na kufa kama vilivyokufa vile vya nyuma. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu kwamba sasa hivi tuko katika matayarisho ya kufanya mazungumzo ya pamoja kati ya wizara yetu na wizara inayohusika na mambo ya vyama vya ushirika yaani kwa kule upande wa Tanzania Bara ni Wizara ya Kilimo.

Mhe. Spika, pia hivi sasa kuna wanafunzi wetu wawili ambao wanaendelea na mafunzo hayo na tayari kwa kutumia bajeti yetu ya wizara basi tunawasomesha sisi. Napenda nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba katika bajeti inayokuja tutaweka kifungu maalum cha kusomesha maafisa wetu wa vyama vya ushirika, ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nina hakika itakuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

Tunalolifanya sasa hivi ni kuwahamasisha vijana wetu wapende kusoma na kujiendeleza na hilo linatia moyo kuona kwamba vijana wetu wako tayari kufanya hivyo.

Nam. 3

Maktaba ya Chake-Chake na Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Raya Suleiman Hamad – Aliuliza:-

Mhe. Waziri, Maktaba Kuu iliopo Chake Chake ni jingo la ghorofa.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba wanafunzi wenye ulemavu wa viungo (wenye kutumia vigari na magongo) hawafaidiki na maktaba hiyo.

(b) Kama ni hivyo wizara imejiandaa vipi kulikabili tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 3 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba tawi la maktaba kuu huko Pemba liko katika jengo la ghorofa. Jengo hilo kiasili halikuwa maktaba bali imeanzishwa maktaba ndani yake kutokana na kukosekana jingo mahsusi kwa ajili ya maktaba. Pia ni kweli kuwa wanafunzi wenye ulemavu wa viungo wenye kutumia wenye kutumia vigari na magongo hawawezi kupanda juu, hivyo ni vigumu kwa watu hao kuweza kutumia na kufaidia na huduma za maktaba.

(b) Wizara yangu imeona kasoro hiyo na imeanzisha mradi wa ukarabati wa ujenzi wa maktaba hiyo. Kwa mwaka 2011/2012, jumla ya milioni 200 zimetengwa kwa kazi hiyo na milioni 60 zimepatikana kwa kuanzia. Michoro iliyoandaliwa imezingatia mahitaji ya watu wote, wakiwemo watu wenye ulemavu. Ujenzi na ukarabati wa maktaba hiyo umeanza na utakapomalizika utawezesha watu wenye ulemavu kutumia huduma za maktaba katika sehemu ya chini ya jengo hilo. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri huoni majengo haya ya ghorofa kwa watu wenye ulemavu yanawanyima haki zao za fursa zote ikiwemo pamoja na elimu. Jengo hili lina watu ambao wanakwenda kujifunza kutoka sehemu mbali mbali, wengi wao ni walemavu wanakwenda kutafuta haki zao za msingi.

Je, Mhe. Waziri utatuambia ni lini utatufanyia utaratibu wa kuweza kupata nafuu na sisi kuweza kuingia katika jengo lile.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyozungumza kwenye swali mama ni kwamba kasoro hiyo tuliiona kwamba ilikuwa inawanyima watumiaji ambao wana ulemavu kuweza kupata huduma hii. Ndio maana wizara kwa makusudi ikaanzisha huu

mradi ambao tayari uko katika hatua za mwanzo, kuhakikisha kila ambaye ana mahitaji ya kwenda maktaba basi anapata mahitaji hayo.

Vile vile Mhe. Spika, mbali ya hii maktaba ambayo iko Pemba na watu wetu wanatumia, tuna *mobile* maktaba ambazo ziko katika TTC zetu zote Unguja na Pemba. Kwa hivyo, hizi mheshimiwa huwaruhusu mbali ya wanafunzi lakini kwa sababu huduma ya maktaba wanatumia watu wote basi kuweza kutumia huduma hizo, nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Je, ule mpango wa kutaka kujenga maktaba mpya pale Chake Chake bado upo vile vile.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, mpango wa kujenga maktaba mpya Pemba tunao. Tatizo ambalo limejitokeza mpaka hivi sasa ni sehemu nzuri ya kiwanja ambacho bado hatujakipata, kwa sababu tulitaka tujenge *center* na *center* ya Pemba ni Chake-Chake, lakini mpaka hivi sasa bado hatujapata kiwanja ambacho tunahisi kinafaa, huu ukarabati ambao tunazungumza ni sawa sawa na ujenzi mpya. Kwa sababu nyuma ya maktaba yetu kuna kiwanja na hiki kiwanja ndicho ambacho tutakitumia kujenga maktaba mpya, nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Nakushukuru Mhe. Spika. Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba tatizo la ujenzi wa maktaba hii ni kiwanja na ametuambia kwamba nyuma ya jengo hilo kuna kiwanja kinasafishwa. Ninavyojua mimi mchoro ambao wanao unagharimu zaidi ya bilioni 1, ambapo bajeti ya serikali ni milioni 70. Hadi sasa maktaba ya Pemba wamepewa milioni 40. Kwa hivyo, atuambie tatizo ni kiwanja au fedha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nilizungumza katika swali mama kwamba katika bajeti ya mwaka huu 2011/2012, tumetenga milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa maktaba. Kwa hivyo, niseme kwamba tatizo sio fedha kwa sababu hizi fedha tayari tumetenga na milioni 60 tayari tumeingiziwa, hivyo tatizo ni kiwanja cha kuweza kujenga hiyo maktaba mpya.

Nam. 23

Wananchi Waliokatiwa Miti Yao Kutolipwa Fidia

Mhe. Mohammed Haji Khalid – Aliuliza:-

Katika utengenezaji wa barabara ya Mtambile Kangani na Mtambile Mwambe Wizara ilikata na kufyeka miti ikiwemo mikarafuu mingi hata katika sehemu ambazo barabara haikufika, mikarafuu ambayo ni sehemu kubwa ya uchumi wa Zanzibar. Pamoja na ukatwaji huo bado wizara haijalipa fidia kwa wale ambao mali zao zimeharibiwa.

(a) Kigezo gani kinachotumika kukata miti hasa sehemu ambazo barabara haikufika.
(b) Je, ni lini wizara italipa fidia kwa wale walioharibiwa mali zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 23, lenvye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, katika utaratibu wa kawaida wa shughuli za ujenzi wa barabara ni lazima eneo tosha la ujenzi liandaliwe, hivyo utaratibu huo ndio uliopelekea kukatwa kwa miti mingi ikiwemo hata mikarafuu, ili kupata eneo la kufanikisha mradi mzima wa ujenzi wa barabara husika. Miti hiyo yote iliyokatwa ilikuwemo katika maeneo ambayo yangestahiki kuwa ni maeneo ya akiba ya barabara na ndio kigezo kilichotumika kuona kwamba barabara zetu hizi ni vyema tukazipatia maeneo tosha yakiwa kama akiba kwa matumizi ya siku za baadae.

(b) Mhe. Spika, napenda tena kurejea kauli ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ya kwamba tutaendelea na utaratibu wetu wa kulipa fidia kwa kuanzia na nyumba na mwishowe vipando na miti. Napenda ifahamike kwamba katika barabara hizi hakuna nyumba zilizovunjwa, isipokuwa kuna nyumba zilizoathirika na ujenzi wa barabara hizi. Napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano italipa fidia ya miti na nyumba hizo kwa muda wowote hali ya fedha itakaporuhusu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekubali kwamba miongoni mwa miti iliyokatwa na mikarafuu ilikuwemo na ni kweli. Karafuu hivi sasa thamani yake ni kubwa licha ya mkarafuu wenyewe. Je, Wizara itafidia kiasi gani kwa kila mkarafuu tukitilia maanani kuwa karafuu ina bei kubwa hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, utaratibu wa kulipa fidia kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, wizara husika inapofanya utafiti wa mazao na miti ni wizara ya kilimo. Wizara yetu sisi tunalipa fidia hiyo baada ya kupata taarifa ya tathmini ambayo imefanywa na wizara husika ya kilimo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kumekuwa na kilimo kirefu cha wananchi wa Pemba katika upanuzi wa uwanja wa ndege kwa mazao yao kulipwa fidia kwa wananchi wa Furaha na Mfikiwa.

Je, kuna mpango gani wa kulipwa fidia hizo wananchi hao.

Mhe. Spika: Ni suala zuri sana, lakini haliendani na suala liliopo hapa. Nikuombe basi kwa heshima zote mheshimiwa uulize kwenye swali la msingi.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Kwa kuwa serikali huwa na mipango yake inapotaka kuleta maendeleo katika sehemu yoyote ile. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba wamewanyima fursa ya kuwalipa wananchi hawa fedha zao kwa wakati na kuwanyima haki zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tumeeleza katika majibu mama ya kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina dhamira ya kumcheleweshea mtu kumlipa malipo au fidia yake. Tatizo tulilonalo ni upungufu wa fedha. Napenda nimuhakikishie Mhe. Asha Bakar kwamba nia ya serikali ipo pale pale na madhumuni ya serikali yapo pale pale, hivyo hali ya fedha itakaporuhusu tutafanikisha azma hiyo kwa kuwalipa,kwani tunatambua hii ni sehemu ya wananchi wetu na sisi kama serikali tunalazimika kuitumikia na kuwatumikia wananchi wetu.

Nam. 30

Uhaba wa Wafamasia

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Aliuliza:-

Katika kudhibiti biashara ya madawa, wizara yako iliweka utaratibu wa wafamasia kudhamini maduka ya madawa badala ya madaktari. Kanuni hizo zilikwenda mbali zaidikwa kutaka mfamasia mmoja adhamini duka moja tu.

(a) Kwa nini serikali isipunguze ukali wa kanuni hizo na kuruhusu mfamasia mmoja kudhamini angalau maduka mawili ili kuondoa tatizo la uhaba wa maduka ya madawa.

(b) Je, kuna tatizo gani kwa daktari ambae yeye ndiye dhamana kwa magonjwa asipewe kibali cha kudhamini duka la dawa ili kukabiliana na uhaba wa wafamasia jambo ambalo serikali inalitambua.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 30 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza ningependa kutoa maelezo mafupi baadae ndio nijibu swali lake.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria za udhibiti wa madawa maduka makubwa ya dawa, yanasimamiwa na wataalamu wa dawa yaani wafamasia na sio madaktari. Udaktari na ufamansia ni taaluma tofauti za afya zinazoongozwa na sheria tofauti zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi. Ili daktari aweze kufanya kazi zake hapa Zanzibar ni lazima asajiliwe na Baraza la Madaktari chini ya sheria nambari 12 ya mwaka 1999.

Aidha, akitaka kudhamini hospitali binafsi daktari huyo ni lazima apate kibali kutoka katika bodi ya ushauri wa hospitali binafsi kwa mujibu wa sheria nambari 4 ya mwaka 1994. kwa upande wa famasia ambao ndio wadhamini wa maduka ya madawa ni lazima wasajiliwe na bodi ya chakula dawa na vipodozi kwa mujibu wa sheria nambari 2 ya mwaka 2006. kwa mujibu wa sheria hiyo kanuni za dawa na miongozo ya dawa mfamasia mmoja anaruhusiwa kudhamini duka moja tu.

(a) Sheria hiyo ya chakula na dawa na vipodozi nambari 2 ya mwaka 2006 imewekwa kwa mujibu wa taratibu za kimataifa za udhamini wa maduka ya madawa.

(b) Uhaba wa famasia utatatuliwa tu kwa mikakati ya kuwasomesha wanafunzi wengi katika fani hiyo na sio kwa kubadilisha taratibu zinazodhibiti taaluma husika.

Nam. 97

Matangazo ya Pombe Michezoni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara inayohusika na masuala ya michezo imekuwa ikikataa udhamini wa mashindano mbali mbali kwa Makampuni yanayotengeneza pombe au timuzetu kuvaa jezi zenye matangazo ya pombe na maandishi mengine ambayo hayatowi taswira nzuri kulingana na mila na utamaduni wa Mzanzibari. Hata hivyo hivi karibuni wakati wa sherehe za miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara, Timu ya Mpira wa Baraza la Wawakilishi ilipopambana na Timu ya Mpira ya Wabunge katika Uwanja wa Taifa Dar es Salaam ilivaa jezi zenye matangazo ya pombe.

(a) Je, Mhe. Waziri kitendo hicho cha timu hiyo kuvaa jezi hizo si kwenda kinyume na agizo la wizara yako.

(b) Ni lipo hasa tamko la serikali kuhusiana na jezi zenye matangazo ya aina hiyo au udhamini wa makampuni yanayotengeneza pombe michezoni.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 97 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa sera ya michezo ya Zanzibar ya mwaka 2007 kifungu cha 2(10)(1) ufadhili wa michezo kupitia matangazo ya vileo pombe, hayakubaliki katika visiwa vya Zanzibar. Tamko hili linalindwa ndani ya mipaka ya Zanzibar. Hata hivyo, timu yoyote nje ya Zanzibar inaweza kuwa na maamuzi yake juu ya suala la ufadhili ingawaje sio busara kutumia ufadhili usio halali.

Mhe. Spika, tamko la sera ya michezo ya mwaka 2007 ambalo linasema ufadhili wa michezo kwa kutangaza bidhaa zote halali kwa ajili ya kukuza michezo unakubalika, bango kutangaza aina zote za vileo katika viwanja vya michezo hayatakubaliwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama alivyojibu Mhe. Waziri katika Sera ya Michezo kwenye kifungu ambacho amekitata yeye kinaeleza kwamba Matangazo ya Pombe hayaruhusiwi katika Viwanja vya Michezo. Sisi Zanzibar hivi sasa tumo katika

harakati za kutaka kujiunga na *FIFA* pamoja na vikwazo vidogo vidogo, lakini naamini baada ya kumaliza mchakato wa Katiba mpya, basi Zanzibar itaweza kujiunga na Shirikisho la Soka la Dunia *(FIFA). (Makofi)*

(a) Sasa Shirikisho la Soka la Dunia linaelezea kwamba siruhusa kuingia na vileo katika viwanja vya michezo, lakini sio siruhusu matangazo.

Je, hatuoni kwamba hii Sera ya Michezo ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inakwenda kinyume na ile Sera ya Shirikisho la Soka Duniani (*FIFA*) ambalo sisi tunataka kujiunga?

(b) Kwa mujibu wa takwimu za Kampuni ya Bia *Breweries* Zanzibar imo katika mikoa mitatu bora, ambapo wanatumia pombe aina ya *Serengeti Lager*. Pombe hii inaingia Zanzibar, inalipishwa kodi na serikali na miongoni mwa kadi hiyo ni mishahara yetu ambayo tunayolipwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Wazanzibari wote.

Je, serikali haioni kwamba hivi sasa tunawacheza shere wananchi kwa kuzuia matangazo lakini tunaruhusu uvyaji wa hicho kilevi chenyewe?

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kama nimemsikia vizuri Mhe. Hamza Hassan Juma amesema kwamba Zanzibar ni katika miongoni mwa mikoa mitatu bora. Kwa hivyo, hapa naomba atusahihishie, kwa sababu ninavyojua mimi Zanzibar sio mkoa. Ahsante sana. *(Kicheko)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza niombe radhi sana wananchi wote wa Zanzibar, narejea tena nawaomba radhi wananchi wote wa Zanzibar kwa kusema kwamba miongoni mwa mikoa mitatu katika hiyo mikoa wanayoisafirisha huko Bara, yaani Zanzibar sio Mkoa Zanzibar ni nchi ya Zanzibar, haivuki mkoa mwengine wowote zaidi ya mikoa miwili kule Bara. Kwa hivyo, Zanzibar sio mkoa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kutoa ufafanuzi zaidi kuhusiana na sera hii. Ni kweli kama alivyoeleza Mhe. Naibu wangu pale kwamba Zanzibar ina sera yake kuhusiana na masuala ya michezo na ni kwamba haturuhusu matangazo ya aina yoyote yanayohusiana na pombe kudhamini vilabu vyetu au timu zetu za hapa.

Vile vile nataka nieleze tu kwamba kila nchi inakuwa na sheria zake na kwa sababu hii haikuwa Sheria ya Kimataifa, kwa hivyo tuna haki ya kufanya hivyo. Hii ni sheria inayohusu Zanzibar tu, hata kama Bara kule tumedhaminiwa na kampuni ya pombe ni kweli kwa sababu kule ni nje ya mipaka ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nilistaajabu sana suala hili limetokana na miongoni mwa Waheshimiwa Wajumbe ambao na wao walishiriki katika mashindano haya, japo kuwa hakuvaa ile jezi, lakini alishiriki yale mashindano. Kwa hivyo, ndio itakuwa yale nyama hakula lakini mchuzi amekunywa. *(Makofi)*

Pia niseme kwamba tunatarajia kuwa member wa *FIFA* baadaye *Inshaallah* pamoja na kwamba tutakuwa, lakini tunazo sheria zetu za ndani vile vile. Kwa kweli pamoja na kuwa kuna Sheria ya Kimataifa, lakini nayo huwa inajaribu kuzingatia mila, silka pamoja na sheria za mule ndani.

Kwa hivyo, na sisi tutazitizama kama tunaiona sheria ile haina maslahi, basi tutaambia wenzetu sheria hii wacha iwemo lakini kuwe na masharti (a), (b) na (c). Kwa maana hiyo, tuache Sheria ya *FIFA* ije, lakini na sheria zetu za ndani tutaziangalia.

Mhe. Spika, kama anavyosema Mhe. Mjumbe kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi ambazo zinatumia sana ulevi. Kweli sikatai unajuka sana ulevi, lakini je unakuja kimichezo, kwa sababu mtu mmoja mmoja hajakatazwa, sasa sisi ni michezo, yaani vilabu au michezo yetu kudhaminiwa na kampuni yoyote ya pombe au kuva jezi ambayo ni ya kampuni ya pombe, sasa mtu kunywa ana hiyari yake.

Kwa mfano, hata Makka unakatazwa ulevi na wala si kama watu hawanywi, lakini mtu anakunywa ndani na sio nje au kwenye hadhara ya watu hiyo hauruhusiki. Kwa hivyo, mtu hajakatazwa kunywa, isipokuwa sisi tulichokataza ni kwamba vilabu vyetu visidhaminiwe na kampuni za pombe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nafikiri nimekidhi kwa kiasi fulani. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa kuwa kampuni hizi za bia huwa zinatengeneza vinywaji baridi kama vile *Malta* na vinywaji vyengine baridi ambavyo vinaruhusika kunywewa hapa Zanzibar.

Je, serikali haioni kuwa ipo haja ya kuziruhusu kampuni hizo za bia kudhamini michezo, ikiwa timu zetu za taifa au vilabu hata Ligi yetu ya Zanzibar kupitia vinywaji vyao baridi?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Spika, ni suala zuri kwa kweli. Sasa ikiwa kampuni ile inatengeneza vinywaji baridi basi hatuna mashaka nayo, yaani ni kitu ambacho kinazungumzika, basi tutazungumza na tukiona kama matangazo ni ya vinywaji, kwani ni sawa na soda kama vile *Fanta* au *Coca Cola* na wala hatuna matatizo tutaruhusu sisi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Nam. 17

Viwanja vya Serikali Vilivyogaiwa kwa Waheshimiwa Wawakilishi

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.17 kama hivi ifuatavyo:-

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nasikitika kuwa nimetoa maelekezo labda hukunifahamu, nilizungumza kuwa swali hili nimeliondoa. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana, hii inaonesha kwamba Mawaziri wanakuwa tayari kabisa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Nam. 32

Uwekezaji katika Sekta Mbali Mbali

Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Mhe. Waziri pamoja na serikali kuwa na nia njema kuwapa nafasi watu wenye uwezo kuanzisha viwanda pamoja na kufungua hospitali binafsi na mabo mengine ambayo lengo lake ni kuipunguzia mzigo serikali na kero za wananchi wake. Kwa vile tunalo eneo kubwa la Tunguu, ambalo bado halijaendelezwa.

Je, huoni kama kuna umuhimu wa serikali kuweka mkakati maalum wa kuanzishwa viwanda katika eneo hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusu yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 32 kama ifuatavyo:-

Kwanza Mhe. Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi juu ya nia nzuri kabisa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kutoa fursa kwa watu wenye uwezo kuanzisha viwanda, kufungua hospitali binafsi pamoja na mambo mengine kwa lengo la kuipunguzia mzigo serikali na kero za wananchi wake.

Vile vile nikubaliane naye kuhusu umuhimu wa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za viwanda. Kwa kulifahamu hilo ndipo Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko mnamo tarehe 21/04/2011 iliwasilisha barua yenye kumbukumbu Nam. WBVM/H.20/C.17 kwa wizara inayosimamia masuala ya ardhi kuhusu pendekezo la kutengewa eneo la viwanda katika sehemu muafaka na kulingana na mipango ya matumizi ya ardhi.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa barua yetu hiyo bado haijajibiwa, lakini kufuatia mawasiliano mazuri kabisa tena ya karibu sana baina ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara inayoshughulikia masuala ya ardhi, tumejuilishwa kwamba hivi sasa wizara hiyo imo katika kuandaa Mpango wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi, ambapo maeneo maalum kwa ajili ya viwanda yatatengwa.

Nam. 111

Uvuvi Haramu Pemba

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Baadhi ya Wavuvi kutoka Kenya wamekuwa wakifanya uvuvi haramu katika Ukanda wa Pemba *Channel* kwa kutumia meli za uvuvi na nyavu zenye macho madogo zinazoburuzwa na mabomu.

(a) Je, serikali inaelewa taarifa ya jambo hilo na imechukua hatua gani kuzuia uvuvi haramu?

(b) Je, serikali ipo tayari kuliwasilisha jambo hili kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki?

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Aliuliza:-

Nakushukuru Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 111 lenye vifungu (a) na (b). Lakini kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kumfahamisha kuwa Ukanda wa Pemba *Channel* ni eneo la bahari lenye upana karibu kilomita 40 lilipo baina ya kisiwa cha Pemba na bahari ya Mkoa wa Tanga. Kwa mujibu wa sheria nusu ya ukanda huo, yaani kilomita 20 unasimamiwa na Mamlaka ya Uvuvi ya Tanzania Bara na sehemu iliyobaki kilomita 20 inasimamiwa na Mamlaka ya Uvuvi ya Zanzibar.

Aidha kwa upande wa kaskazini Pemba *Channel* imepakana na Jamhuri ya Watu wa Kenya. Mpaka baina ya maji ya bahari ya ndani katika Pemba Channel unaogawa bahari ya Tanzania Bara kwa upande wa magharibi na bahari ya Kenya kwa upande wa kaskazini ni mkondo wa maji wenye kina cha mita 820.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Uvuvi kwa kutumia meli unahitaji kina kikubwa cha maji, ili meli za wavuvi kutoka Kenya waweze kuvua kwa kutumia nyavu zenye macho madogo, nyavu za kuburuzwa na uvuvi wa kutumia mabomu upande wa Zanzibar.

Kutokana na hali hiyo, itabidi meli hizo zivuke kutoka bahari ya upande wa Tanzania Bara au kutoka mpaka wa Kaskazini wa Bahari ya Kenya wauvuke mkondo wenye kina cha mita 820, eneo ambalo nyavu zenye macho madogo na nyavu za kuburuzwa haziwezi kusimama na pia waingie kwenye maji madogo Magharibi ya Kisiwa cha Pemba, ambako nako meli zinaweza kukwama.

Hata hivyo, Kikosi cha Doria cha Idara ya Uvuvi wala Kikosi cha KMKM havijawahi kugundua wala kupata taarifa ya kuweko meli za uvuvi haramu kutoka Kenya kwenye maji madogo ya Pemba *Channel* upande wa Zanzibar.

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, asubuhi tumepokea wageni, lakini kwa bahati mbaya walichelewa kidogo wakati tumeanza utaratibu wa Maswali na Majibu.

Kwa hivyo, niliona si vyema kuingilia mtiririko ule utaratibu, kwa kweli ni wageni muhimu ambapo mwenzetu Mhe. Mbarouk Wadi Mussa ndiye

aliyewaleta na hawa ni wageni wetu wanaohusu Taasisi ya Utafiti, Upangaji na Utekelezaji na Kutafuta Wafadhili wa Miradi (*Research Planning and Project Writing Association*). Makao Makuu yao ni pale *Diamond Trust Bank* Msimbazi Dar-es-Salaam.

Waheshimiwa Wajumbe, wenzetu hawa kupitia kwa Mhe. Mbarouk Wadi Mussa wamekuja hapa Zanzibar na wapo Kilimani mkabala ya Hospitali ya Al-Rahma. Lengo la ujio wao ni kuweza kuwasaidia Waheshimiwa Wajumbe juu ya masuala hayo ya miradi. Hivyo, leo hii ndio wamefika hapa kwenye Baraza leo na ningependa tuwakaribishe na kuwakaribisha kwake kwa mujibu wa taratibu zetu ni kuwataja.

Wageni hao wanaongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo Patrick Bettelo, naomba asimame. Kwa upande wa *Board Member* yuko Bahadur Dewji, naomba asimame. *(Makofi)*

Vile vile yupo Mfadhili wa Miradi ambaye ni Mchungaji Naaman Shauri, pia yupo Mkurugenzi Mkaazi wa hapa Zanzibar ndugu yetu Ally Omar Albarvan. Waheshimiwa Wajumbe, wengine ni Mkuu wa Utawala ndugu yetu George Mwaimu, pia yuko Mkurugenzi wa Masoko ambaye ni Antony Makoke, yuko Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Kimataifa Joram Mhongo. *(Makofi)*

Wengine ni Mkurugenzi wa Usalama wa Misaada Ahmed Semtunguja, yuko Mkurugenzi wa Afya Dkt. Ayoub K. Jungo, pia yupo Mkurugenzi wa Halmashauri za Wilaya Cliff Sonoko, inaonekana amepata dharura ametoka nje. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hawa ndio wageni wetu naomba kwa niaba yenu Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kuwakaribisha sana na kuomba radhi kwamba wamekaa muda mrefu wakisubiri watambulishwe rasmi kwenu, kwa sababu tulikuwa tuko kwenye Kipindi cha Maswali na Majibu. Hivyo, wageni wetu tunawashukuru na karibuni sana. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Maslahi ya Viongozi wa Kisiasa

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba nichukue nafasi hii kukushukuruni kwa mjadala wa mswada huu ambao unaendelea. Mhe. Naibu Spika, jana aliendelea mjadala na tulifika pahala ikawa sasa Waheshimiwa

Mawaziri wameanza kuchangia. Sasa nilipokuwa nikifuatilia mjadala huu nilimuona Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria anaendelea kusaidia kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo ambayo Waheshimiwa Wajumbe walikwishaanza kuchangia.

Kwa kweli ni utamaduni wetu wa kawaida huwa tunaacha *backbenchers* kwanza kuchangia, ili halafu baada ya hapo twende na utaratibu wa kuwaita Waheshimiwa Mawaziri ambao wamejipanga nao wachangie kwa ajili ya kusaidia kutoa ufafanuzi na hatimaye mwisho kabisa kumwita Mhe. Waziri ambaye aliyetoa hoja.

Waheshimiwa Wajumbe, huu ni utamaduni hasa iliomo ndani ya Kanuni ni kwamba Waziri mtoa hoja ataitwa mwisho ili kutoa majumuisho kwa lengo la kufafanua mambo mbali mbali.

Lakini ni utamaduni wetu ambao tuliouweka kwa muda mrefu kujaribu kuona kwamba, kwa sababu miswada au maswali wakati mwengine yanahusu wizara hii na nyengine. Sasa kwa kuwa serikali inafanyakazi kama timu ya pamoja, basi hatimaye mawaziri husaidia hapa na pale kwa kutoa michango nao sehemu nyengine kuibia, kwani wengine wanayo majibu kutoa mambo ambayo kama vile kutoa tahadhari, ili tuone mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria jana kuanza kutoa ufafanuzi wa hapa na pale, basi palifumka wimbi kubwa la Waheshimiwa Wajumbe ambao wametaka kuchangia. Jambo ambalo kidogo limeondoa ule utamaduni wetu wa kawaida wa mtiririko wa kuanza *backbenchers* na baadaye tukenda kwa mawaziri. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, nimepata majina karibu 17 baada ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kuanza kutoa ufafanuzi, ambao yatakayokuja baadaye sasa inaweza pengine yeye iwe hakupata nafasi ya kuisaidia serikali. Waheshimiwa Wajumbe, nasema kwamba utaratibu wetu mzuri ni hasa ule wa kuzungumza *backbenchers* tukafikia pahala tukaridhika kuwa wamemaliza na halafu ikaanza safu ya mawaziri. *(Makofi)*

Wakati fulani wengine inakuja kwa sababu ya kwamba wakati wa kuchangia hawapo au bado walikuwa hawajaamua na wengine kwa bahati mbaya inakuwa hakuwahi kujipanga na inaleta tabu kidogo katika kupanga muda.

Kwa kweli wakati mwengine unashindwa kumzuia Mhe. Mjumbe kwa sababu unajua huna wajumbe wengine, kwa hiyo unampa kwa mtiririko pengine wa dakika za nyongeza juu. Lakini inapokuja mfumko wa wajumbe wengine

kutaka kuchangia na muda sasa umeshakuwa finyu kidogo inaleta tatizo katika kugawa muda na Waheshimiwa Wajumbe kuwapa haki ya kutoa mawazo yao katika mjadala wa jambo ambalo liko mezani.

Waheshimiwa Wajumbe, ninachoshauri ni kwamba tuendelee na utamaduni kwamba Waheshimiwa Wajumbe hasa *backbenchers* kuleta maombi ya kutaka kuchangia mapema, ili hatimaye tunapoanza mawaziri basi isijetena ikawa kuna Mjumbe mwengine anataka kuchangia.

Kimsingi itaondoa ule mtiririko mzuri na Mjumbe anaweza kuhisi maelezo atakayotoa baadaye hayakupata majibu, kwa sababu mawaziri wengi wameshatoa ufafanuzi wa baadhi ya maelezo na Mhe. Waziri mtoa hoja pengine ule muda aliopangiwa hautatosha kumaliza yote yale ambayo yamekuja baadaye.

Kwa maana hiyo, naelekeza kwamba tuendelee na utaratibu huo na hii timu iliyoingia hivi sasa kwa kuwa bado tuko kwenye muda, nitajaribu lakini sasa itabidi tuwe tunatoa muda mfupi, ili tuelewe kwamba kuna shughuli zetu nyengine tumezipangia baada ya hapa. Kwa kweli jana Mhe. Naibu Spika, alifikiri kwa kuwa hana mjumbe yeyote *backbenchers* ni kwamba *backbenchers* tayari wamemaliza, ndio maana muda ulikuwepo akamwita Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Sasa naendelea kuomba mashirikiano makubwa makubwa ya Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na Mawaziri kusaidia kiti, ili kuendeleza shughuli zetu ziende vizuri zaidi. Tutaendelea baada ya hapo na ilikuwa ni zamu ya Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, lakini ameniomba dharura kwa sababu ametokezewa na jambo na nafasi hiyo sasa ameridhika na pale alipokwisha kuchangia.

Kwa hivyo, nimkaribishe Mhe. Saleh Nassor Juma kwa muda mfupi, yaani tutumie dakika 10, lakini twende kwenye *point* kwa utaratibu mzuri, ili baadaye tumalize timu ya mawaziri na kuhakikisha kuwa tumemaliza shughuli hii kwa kadri hali itakavyokuwa. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa hii kuweza kutoa mawazo yangu hukusu hoja iliopo mbele yetu.

Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutujaalia uwezo wa kutoka majumbani kwetu mpaka kwenye ukumbi huu, kwa ajili ya kuujadili mswada ambao kwa kweli naita kitanzi kwa walipakodi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mswada uliopo mbele yetu ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ulipaji Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam. 4 ya mwaka 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Nam. 6 ya mwaka 1999 na Kutunga Sheria Mpya ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Baada ya Kustaafu pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, viongozi wastaafu waliotajwa hapa ni pamoja na Rais, Makamu wa Rais, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Spika, Mawaziri, Naibu Mawaziri Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Mshauri Maalum wa Rais.

Kwa kweli mimi nataka tatizo kwa mswada huu. Mhe. Spika, mswada huu kama utauangalia unawabagua wananchi, unaleta ubaguzi mkubwa. Kwa sababu umesema Naibu Waziri na Waziri pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Huwezi kuwa Naibu Waziri wala Waziri kama hujawa Mwakilishi. Leo unataka kuleta maslahi unawa – *standardizes*, ungetaja mwakilishi tu angekuwa keshaingia Waziri na Naibu Waziri. Sasa unambagua Naibu Waziri inamaana unajenda makundi. Msada huu nawaombeni Waheshimiwa Wawakilishi msiupitishe kwa sababu unatubagua. Lakini ndani ya Wawakilishi tumebaguliwa katika makundi. Mimi nadhani Mswada huu waurudishe. Kama umetubagua sisi watu ambao tumo ndani ya chombo cha kutunga sheria umetubagua, je, hao waliokuwepo nje watafanywa nini.

Mimi nadhani Mhe. Spika, kuna msemo wa Kiswahili unasema nyimbo ya kufunzwa haikeshi ngoma. Kama tumeangalia uzoefu wa mabunge mengine kwa mfano Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1999 walipitisha Mswaada kama huu. Bunge la Kenya, walipitisha Mswada kama huu. Lakini wao kabla ya kupitisha waliangalia nguvu za uchumi wao. Sisi hatukuangalia tumekurupuka tu, tumefunzwa nyimbo kumbe haitaki kukesha ngoma yetu.

Mhe. Spika, Mswada huu nimesema unawabagua wananchi. Hivi sasa mfanyakazi wa serikali wa hapa Zanzibar analipwa laki moja na elfu ishirini na tano ni sawa sawa kwa siku ni shilingi elfu tano. Leo unataka tuyakusanya mapesa haya tuyapeleke kwenye familia moja. Kama pesa zipo kwa nini ha hawa wafanyakazi wa serikali msiwaongeze pesa ili wakaweza kuishi vizuri. Huu ni ubaguzi, inatia aibu.

Waheshimiwa Wawakilishi hivi sasa mimi nataka nimpatie Mhe. Spika, shilingi elfu kumi atumie nyumba yake kwa siku atatumia vipi. Leo kama pesa zipo hizi tunazichukua tunakwenda kuzipeleka kwa MaRais wastaafu, Makamo wa Rais wastaafu, na hatujui mpaka ukifika mwaka 2040 tunaweza tukawa na

utitiri wa MaRais Wastaafu na Makamo wa Rais Wastaafu. Waheshimiwa ni lazima tuwe makini katika hili.

Hivi sasa mwananchi na mlipa kodi wa nchi hii anaambiwa achangie huduma ya Afya hata afya ya uzazi. Kama pesa zipo kwa nini tuwapelekee Ma-Rais Wastaafu, tusiwapelekee akina mama wakaweza kujifungua vizuri, wakafanya mambo yao vizuri. Hii ni dhulma.
Mhe. Spika, sisi lazima tujue wajibu wetu Wawakilishi. Wajibu wetu sio kupitisha tu bajeti ya serikali ni pamoja na kuangalia matumizi mazuri ya fedha za walipakodi wan chi hii. Kutoa mamilioni ya fedha tukazipeleka kwa maRais wastaafu, makako wa Rais wastaafu sio matumizi mazuri ya walipa kodi wa nchi hii, tunawadhulumu, watatushtaki. Mswada huu ni wa ubaguzi na unajenga matabaka.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba ya kale ni dhahabu. Katika TANU wenzetu walikuwa wakipiga vita "**Kupe, Mabwanyenye, Makabaila**," wenzetu wa TANU na Afroshirazi walikuwa wakifanya kazi hiyo. Sisi tunajenga makabaila, tunakiuka katiba yetu wenyewe. Kwa mujibu katika nchi ya "**Ujamaa na Kujitegemea**" ambayo hii ilikuwa ni sera ya Chama cha Mapinduzi na ndiyo siasa iliyokuwa ikutumiwa na Mwalimu Nyerere nafikiri mpaka sasa ndio hiyo hiyo sera iliyokuwepo, anakwambia kwamba mapato ya wananchi hayapitani sana. Leo unatuita hapa sisi tumlipe Rais Mstaafu posho la asilimia 80 la Rais aliyekuwepo madarakani.

Mheshimiwa nakuhakikishia hili ni tatizo. Na huu Mswada nasema urudi kwa sababu hakuna Mwakilishi yeyote anayejua mashahara wa Rais hapa. Sasa kama tupitishe asilimia 80 ya nini. Kitu gani hichi tukifanyie 80% kilichokuwa hakijulikani. Wawakilishi mimi nadhani mtakapoupitisha Mswada huu nawaomba sana Mhe. Spika, katika kuupitasha Mswada huu utaratibu utumike wa *role call*, kusudi Mwakilishi yeyote atakayeuunga mkono akahukumiwe na wananchi aonekane hasa. Naomba sana Mheshimiwa utumike utaratibu huo, kusudi itakaepitisha dhulma hii, atakaewatia kitanzi wananchi wa Zanzibar basi ajulikane na wananchi wamuhukumu kupitia masanduku ya kura.

Mhe. Spika, kwa kweli Rais wetu tunampenda sana na Katika Rais tunaempenda katika nchi ni Dokta Sheni pamoja na na Makamo wake. Na tunaishukuru GNU kwa kuleta amani na utulivu katika nchi, kuleta mshikamano wa kitaifa. Tunamshukuru sana Dokta Sheni na timu yake kwa kuweza mpaka sasa hivi kwamba tumetulia, tunapendana, tunatembeleana. Hii ni faida kubwa, lakini unapogusa kodi za wananchi hili lazima tuwe na utaratibu mzuri.

Mhe. Spika, nakuomba sana na Waheshimiwa Wajumbe kwamba wananchi wa nchi hii wana matatizo mengi. Sisi tupitishe fedha hizi kuwalipa maRais wastaafu, makamo wa Rais wastaafu wakati Wazanzibari wa nchi hii, chombo cha kusafirisha cha kwenda Pemba cha uhakika hakuna. Kumbe mapesa yapo basi kwa nini watu waendelee kufa na maboti mabovu mabovu. Kumbe mnatudhulumu, sisi tunakufa kwa maboti na mameli mbovu hapa, kumbe pesa mnazo mnataka muwalipe maRais wastaafu. Hili ni tatizo, muko *bias*.

Mhe. Spika: Unazo dakika mbili.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante, naomba nimalizie kwa kusema kwamba sheria hii irudishwe kwa sababu Wenyeviti wa Kamati za Baraza hawakuukubali na *back benchers* sote tukiwa Wawakilishi wa Wananchi hatukuukubali. Mtakapoupitisha Mswada huu ni dhuluma na tunawaonea wananchi wetu.
Vile vile jana Mhe. Abubakary alisema kwamba hii sheria ni kongwe. Hii si sheria kongwe, ni sheria mpya na imefuta sheria mbili. Hii ni mpya bwana. Kwa hivyo kuna haja sasa itakapotungwa sheria hii tumpangie Rais mshahara wake ili tujue ni asilimia ngapi tuweze kukata. Kwa hivyo Mhe. Abubakary asitwambie kwamba hii sheria ni mpya imefuta sheria mbili.

Kwa mfano Mzee Jumbe sasa hivi anataka apumzike, ukimpa lakini tano kwa simu, utambabaisha, saa 24, atakuwa anazungumza na watu, afanye hili, wakati yeye anatakiwa apumzike muda mwingi Rais wetu mstaafu Mzee Jumbe. Hizi laki tano za nini?
Mhe. Spika, tusiwadhulumu wananchi. Nimalizie kwa sababu bado dakika mbili, nasema siiyungi mkono hoja hii na naomba ikiwa mtaipitisha kwa nguvu basi muipitishe kwa *role call*, ili atakayepitisha hoja hii basi ahukumiwe na wananchi kwenye masanduku ya kura huko kwenye majimbo yao.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii fupi ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Ulipaji Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam. 4. Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ulipaji wa Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam. 4 ya Mwaka 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Nam. 6 ya Mwaka 1999 na Kutunga Sheria Mpya ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Baada ya Kustaafu Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia kwanza naanza kwa kutoa shukurani kwa wote waliochangia na nawapongeza, nashukuru michangio mizuri iliyotolewa na wanadhimu pamoja na *back benchers* na mchango mzuri wa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria tumeusikia lakini bado haujafikiwa na wakati wake.

Mhe. Spika, kwanza naomba ufafanuzi kuna jaduweli hili la marekebisho ya Sheria ya Mafao ya Viongozi Wastaafu wa kisiasa nambari (1), (2) na (3). Hili nambari (1) ambalo ni huduma tegemezi imeeleza kuwa naomba kunukuu.

Kifungu cha 16 "Endapo Rais, Makamo wa Rais au Spika wa Baraza la Wawakilishiatafariki wakati akiwa madarakani mtoto au watoto wao watahudumiwa na mamlaka husika hadi watakapotimia umri wa miaka 20 au ikiwa mtoto wa kike pale atakapoolewa."

Lakini kumeongezwa maneno "au lolote litakalotokea mwanzo" hapa kidogo naomba ufafanuzi.

Mhe. Spika, la pili hiki kifungu cha 3 kilichorekebisha Sheria Nam. 20.2 kinasema

> "Rais ataweka asilimia maalum katika kifungu 17 kwa kushauriana na Spika wa Baraza la Wawakilishi na Makamo wa Pili wa Rais"

Mhe. Spika, hapa naomba kupata maelezo kwa sababu moja. Kwa mijibu wa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 84, ukifungua ukurasa wa 28 kifungu cha 39 Nam. 5 na Nam. 7 kinaeleza hivi.
Kifungu Nam. 5 Makamo wa kwanza wa Rais atakuwa ni mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake na atafanya kazi zote atakazopangiwa na Rais. Na kifungu Nam. 7 kimeeleza kuwa Makamo wa Pili wa Rais atakuwa ndiye mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake na pia atakuwa ndiye kiongozi wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi.

Kwa vyovyote iwavyo Mhe. Spika, Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais ni washauri wakuu wa Rais. Lakini kwa nini katika kifungu hichi ikawa Mhe. Rais atashauriana na Mhe. Spika, na Makamo wa Pili wa Rais, huyu Makamo wa Kwanza wa Rais kwa nini ikawa hakuingizwa wakati na yeye ni mshauri mkuu wa Rais. Hapa nataka nipate ufafanuzi.

Mhe. Spika, jengine Mswada huu kila mtu ameusoma ameufahamu na hii ni mara ya pili kuletwa. Wengi waliyotangulia kuchangia kulikuwa kuna marekebisho kadhaa yaliombwa tokea kwenye Semina na hata kwenye Kamati husika lakini yote hayakuingizwa.

Mhe. Spika, tunaijua hali yetu ilivyo hivi sasa ya kiuchumi, ni juzi tu tumepitisha bajeti, kuna Wizara zimepata hadi kufikia asilimia 12 ya makadirio yao, ni hatari. Tumeshuhudia viongozi wetu wakuu akiwemo Mhe. Rais, Mhe.

Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na wengineo wametembea nchi mbali mbali duniani kutafuta misaada kutokana na hali yetu ngumu ya kiuchumi.

Hivi sasa tunaona hali ya elimu ilivyoanguka mpaka primary vitabu hakuna, Sekondari vifaa chungumzima hakuna. Mishahara ya walimu ndio kama ilivyo. Juzi hapa tulizungumza kuhusu elimu ya juu wanafunzi wetu waliojitahidi katika hali ngumu wamefanikiwa, serikali imeshindwa kuwalipa na badala yake wakasema kuwa watawalipa wale wa sayansi tu kwamba. Hii ni kutokana na hali mbaya ya uchumi, vyenginevyo wote wengiliendelea na masomo na hali ingelikuwa nzuri.

Jana tumezungumza na tumeona kuna maskuli chungumzima yamejengwa na wananchi na serikali iliwaahidi yakifikia linta yataezekwa, yamekaa hivi hivi shida inazidi kuongezeka kwa kuwa serikali masikini. Serikali hii inawajali sana wazee, wapo waliotumikia kazi katika serikali hii na kadhalika. Leo mzee analipwa Sh 5000/- tu kwa mwezi, serikali naamini haitaki kulipa Sh 5000/- lakini kwa sababu hakuna uwezo. Itakuwaje Mheshimiwa tupitishe bajeti ya wastaafu ambayo kiwango chake hata mimi na hesabu yangu yote sizijui naona mahesabu tu yaliyokuwa hayakukamilika.

Mhe. Spika, mimi ushauri wangu hivi sasa hasa kwa sababu tuna Serika ya Umoja wa Kitaifa tuko pamoja tuangalieni namna gani tutaweza kuwakwamua wananchi au kuikwamua nchi hii katika hali ngumu ya uchumi na ikiwezekana hata kufanya Mswada mwengine wa kupunguza hayo maslahi yaliyofutwa mwaka 1988 na 1999 kutokana na hali ngumu ya nchi ilivyo. Sio kuongeza mambo kiasi ambacho hata hayaingii akilini.

Mhe. Spika, kuhusu wakati wa kumpa Mheshimiwa aliyeshika nafasi ya uRais kiinua mgongo asilimia 50 ya mshahara wa juu waliyopokea wakati anasita kuwa Rais tena uzidishe kwa miezi aliyotumikia ya uRais. Sisi uzoefu wetu hapa ni miaka 10, hiyo ni sawa na miezi 120 ni pesa hazina kiasi, wakati hali tunaijua ilivyokuwa ngumu.

Mhe. Spika, kuna posho la kumaliza muda litakalikuwa sawa na kiwango cha mshahara wa juu uzidishe miezi 28 anaongezewa mtu huyo huyo mmoja katika hali hii ngumu ya uchumi tuliyonayo. Si hivyo tu kunapencheni ya kila mwezi ambayo itakuwa sawa na asilimia thamanini ya mshahara wa kila mwazi wa Rais aliyekuwepo madarakani, pia zinaingizwa kwa mtu huyo huyo mmoja. Hii ni hatari kubwa sana. Si hivyo tu kuna posho la mauzo ya kila mwezi ambalo litakuwa sawa na asilimia 80 ya posho la matunzo aliyelipwa Rais aliyekuwepo madarakani. Yote ni mapesa ya mtu huyo huyo mmoja imeendelea tukiyataja

hapa yatachukua muda mrefu sana. Na sio huyu peke yake kuna Makamo wa Kwanza, kuna Makamo wa Pili, kuna Spika mwenyewe.

Lakini Mhe. Spika ameliona hili nashukuru sana, mbali na viongozi wengine wa kisiasa. Hebu tuangalie kwa kipindi cha miaka 20 nchi hii itakuwa na uwezo hata wa kujiendesha kwa kupata fedha za kuwalipa hawa wastaafu tu, achilia mbali shughuli nyengine. Kwa maana hii tuende na wakati, tumewekwa na wananchi tuwatumikie na tusijali maslahi yetu sisi tu na viongozi wetu. Tujali zaidi maslahi ya nchi, nchi yetu tunajua iliyokuwa na tabu.

Mhe. Spika, sisi ni Wawakilishi tupo katika majimbo tumekuwa ni Mawaziri wa Wizara zote. Tumepitisha bajeti ya Wizara ya Afya hapa lakini tumejenga vituo vimeshindikana, kwa sababu serikali haina pesa. Skuli ikitaka kujengwa sasa tunaambiwa sisi, tunatoa pesa. Elimu ilimradi kila kitu sisi wawakilishi wala hatuna pesa ya hivyo kutokana na serikali ilivyokuwa haina uwezo kwamba haina. Kwa maana hiyo isijitafutie mashaka iliyokuwa haiyawezi.

Mimi ningeiyunga mkono kama ingeliandikwa kule mwisho kuwa serikali itatafuta fedha hii nje ya bajeti ya serikali kwa kutafuta misaada kutoka nje. Ikiwa kuna utaratibu wa ku tafuta misaada huko nje wakalipwa watu hawa mimi sina ubishani lakini kwa pesa ya serikali, kodi za wananchi kama zinavyokusanywa kutokana na mahitaji yalivyo, hazisaidii chochote, tumo katika hali mbaya ya uchumi. Mimi hii siiungi mkono na ninakuhakikishieni wananchi wote wanatupigia simu hawaungi mkono na sisi wanatushangaa kuwa ni watu wa aina gani kuendelea kujadili Mswada huu.

Ushauri wangu Mheshimiwa naomba kusema kuwa sio kusema urejeshwe lakini huo uondolewe moja kwa moja mpaka hapo tutakapoweza kujichuma. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa ya kusma machache katika Mswada huu. Kwanza mimi ningesikitika kwamba bado tunaendelea na utaratibu ule ule wa kupeana madadiliko katika wakati usiofaa. Mnatufanya tutie udhu kwenda kukimbilia kusali kati kati mnatwambia twende tena msalani. Tunatumia nguvu nyingi, watu wanakwenda katika Hansard, watu wanakwenda katika Intenet na watu wanakwenda katika library kujiandaa. Lakini matokeo yake subuhi unafika hapa unaambiwa kuna rekebisho hili, kuna rekebisho jengine. Ningeomba masuala haya yakarekebishwa mapema. Tunachokisema tunataka tuwe na uhakika nacho, tukija hapa bila ya maandalizi tutakuwa tunazungumza tu mambo ambayo wengine tunashutumiana bure.

Mhe. Spika, Mswada huu upo zamani na una maalamiko mengi kutoka kwa wananchi na kutokana kwetu sisi Wawakilishi. Wananchi walitoa maoni yao kupitia vyombo mbali mbali. Na sisi Wawakilishi tukatoa maoni yetu kupitia semina na sehemu tofauti. Lakushangaza ni kwamba hadi hii leo serikali haijaona umuhimu wa wananchi hao wakasema kwamba hawa wao maoni yao kwa wengi walisema kwamba Mswada huu haujafika wakati wake.

Sisi tulipendekeza tukasema kwamba Mswada huu wakati wake bado. Sasa sijui hichi kinachong'ang'aniwa hapa ni nini. Wengine wanasema kwamba Mswada huu labda ungewekwa 2014, wengine ingelikuwa hivi, wengine ingelikuwa vile. Lakini tunachokisema ni kwamba kisiasa na kiuchumi Mswada huu haujafika wakati wake. Kwa hivyo tunaomba serikali uurudishe, ili serikali ikae na uangalie tena.

Sisi tupo katika awamu hii, awamu hii ni kama mwezi mmoja na miezi mine, hatujazalisha chochote kile. Sasa sisi tunaelekea kwenda kumtunza mtu au labda niseme tunakwenda kumtunza mwanafunzi ambaye hata mtihani hajafanya. Sisi tunataka kumkama ng'ombe ambaye hata kumlisha hatujamlisha. Tumezalisha nini sisi kiuchumi cha kusema sasa tuanze kugawana. Wananchi watatulalamikia kwa wingi sana. Haya ni lazima tuyazingatie. Leo mimi nikirudi katika jimbo langu kama nitapitisha Mswada huu wananchi nitakachowambia watakuwa hawanikubali Mheshimiwa, wataona mimi tayari nimeshashirikiana na serikali katika kuwanyonya wao Sasa ili kuepusha hii migogoro ya kisiasa katika sehemu zetu tunazotoka tunaomba Mswada huu mukaupitie tena, muulete katika wakati unaofaa.

Mwaka wa 1999 mlipitisha *amendment* na *amendment* hii kuna wengine walisema labda tukija tukifanya karibu ya kufika hapo kutakuwa na malalamiko. Hivyo sivyo tufanye *amendment* katika wakati ambao utakuwa ni mnasaba. Hivi sasa bado hatujafikia wakati huo. Mimi ningelikuwa nina uhuru basi hata hizi sheria za 1984 Sheria Nam. 4 na hii Sheria Nam. 6 1999 ningelisema pia zingelikuwa zirekebishwe upya. Hivi sasa kutokana na hali yetu ya kiuchumi na kisiasa haituruhusu kuwa na Miswaada kama ile. Kwa hivyo naendelea kusema tena kwamba Mswada huu bado wakati wake urejeshwe. Mkauangalie wakati wake ukifika tutaangalia pengine Waziri anayeshughulikia na mambo ya mafuta anaweza akatwambia tayari tumeshachimba mafuta, tutapanga mafao mengine.

Wenzetu Egipty tumewaona wamefanya nini. Kama yule ameshaekewa mafao sijui kama hawatasema turudishe tusimpe, kwa sababu hakutenda mema. Sasa sisi tunataka kumtunukia mtu hatujui kafanya nini, awamu hii bado hatujazalisha kitu. Tuendelee kuusubiria Mswada huu, wakati wake bado.

Waingereza wana msemo wanasema *time an type*, yale maji huwa yana wakati wake wa kupwa na kujaa sio yanajaa tu kila wakati. Kuna wakati yanakupwa na kuna wakati yanakuja juu. Bado wakati haujafika.

Mhe. Spika, sisi tunaelekea katika ujenzi wa Demokrasia na Utawala Bora. Sasa hii haimalizii katika mwenendo wa kisiasa tu, pia ipo katika mwenendo wa kiuchumi. Tutakuwa hatujatenda haki kwamba mtu mmoja tukamuwekea pato kubwa kiasi kama hichi. Huu mgawanyo wa pato la taifa hautokuwa mzuri kama sisi tutamuelekezea mtu mmoja tu. Hapo hatutofanya demokrasia ya kweli na itakuwa huo utawala bora haupo. Tunachotakiwa kukifanya ni kuhakikisha kwamba hili pato la taifa linagawanywa katika mririko uliyo mzuri na kila mmoja aridhike.

Leo hali yetu ya kisiasa ipo nzuri, kila mmoja sasa anajitanua, anaishi anavyopenda na anasema anachokitaka. Sasa tukiikoroge. Wananchi walio wengi hawaungani na sisi katika suala hili. Kwa hivyo tunachokisema kwamba huu Mswada bado wakati wake.

Mhe. Spika, labda nizungumzie jengine la kuzingatia. Katika vifungu 19 na vifungu vya 20 kuna neno limetumika la kuzingatia, Rais atazingatia, Waziri atazingatia. Katika mfumo wa kidemokrasi mambo hayaendi hivyo. Sisi katika bajeti yetu tunasema tuna Vision 2020 ambayo tunakusudia katika kujenga demokrasia na utawala bora uliyo haki. Sasa kama atazingatia, kwa nini azingatie Rais tusizingatie sisi. Sisi ndio watunga sheria hapa *legislature* yule yeye ni e*xecutive*. Sisi tumalize kufanya hapa kwamba tunaweka fomula hii baadaye tunampelekea yeye. Je, kakubali au kakataa, sio tumpe *option*, tumpe upenyo wa kuweza kufanya, tumalize sisi kwanza.

Hapa wenzetu juzi walisema kwamba sasa uhuru wa chombo hichi, tunapokonywa huko ndio tunapoelekea. Kwa sisi tupokonywe uhuru huu. Tuachiwe sisi tutunge hii sheria
tuimalize tukisema atazingatia, atazingatia nini. Tulichokisema sisi au anachokitaka yeye ndicho atakachokiamua na hii mheshimiwa itaninyima mimi fursa *confidence* itakuwa sina mbele ya Rais kwa sababu najua kesho kutwa yeye anakuja kufanya nini.

Mhe. Spika, nikisema mimi leo mswada huu sitoupitisha nauacha hivi hivi au yeye atajenga imani kwamba yule hakuwa na imani na mimi. Kwa hivyo, kwa nini tujenge mihimili hii miwili, hivyo tuyaondoshe haya yote yasiwepo kama kweli tunataka kujenga demokrasia ya ukweli na utawala bora basi haya hatutakiwi tuyaweke tena njiani hivi sasa ndio wakati wa kuyaondosha.

Mhe. Spika, naomba kutoa msemo mmoja wa Waingereza wao wanasema kwamba ikiwa mataka ya ndizi ambayo umeshakula unatupa njiani, mataka ya chungwa unatupa njiani matokeo yake ukilikanyaga utaanguka miguu itakatika mheshimiwa. Kwa hivyo, haya sisi tusiyaruhusu kuwepo katika barabara yetu tunaelekea katika ujenzi wa utawala bora na demokrasia. Mhe. Spika, mimi sijashawishika hata kidogo na mswada huu kwa hivyo ningeomba wanaohusika wakaurudisha, ahsante sana.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante sana Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na uzima pamoja na afya na kufika leo katika Baraza hili kutekeleza shughuli zetu. Mhe. Spika, mimi nadhani mswada huu tangu jana umeshachangiwa kwa upana, ushachambuliwa kila kitu kilichobakia hivi sasa kuna kazi moja tu ambayo kila anayesimama tunaifanya, hapa kuna herufi mbili tu tunazitumia ama ya shada au ya inna. Kwa hivyo, ndio kazi zilizobakia kukaza na kutia msisitizo, kazi mbili hizi nadhani kwa wawakilishi tuliobakia ni kazi kubwa ambazo tunazozitekeleza.

Mhe. Spika, jana Mhe. Asha Bakari Makame alizungumza maneno mazuri hapa kwamba milango yetu wengine iko wazi, mswada huu ulipokuja mara ya kwanza sisi kama ni wawakilishi ambao tunawakilisha wananchi tulipata masuala mengi, masikini ya Mungu wengine hata kuyajibu hatuyawezi. Lakini ulikuwa ukipita njiani wengine saa nyengine unawakimbia watu kwa sababu hujui ujibu nini suala linalokuja kazi yenu wawakilishi kukaa huko mkajilimbikia mapesa huku watu wanakufa na njaa, watu wana matatizo, kusema kweli hizi lugha zilikuwa na wananchi mpaka hadi ya kesho.

Mhe. Spika, hivi leo mkipita sokoni wananchi hawana mazungumzo wanasikiliza kitu gani kinazungumzwa katika Baraza la Wawakilishi, ukipita Darajani hakuna mazungumzo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nasema kwamba sio dhambi hata kidogo kuna jambo utalifanya utapata dhambi na una hakika nafanya jambo hili napata dhambi kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, mimi nasema si dhambi mswada huu kurejeshwa kwanza kutokana na hali ilivyo tukatizama mengine ambayo yanatukabili katika nchi yetu tuna matatizo gani. Mhe. Spika, wenzangu wameshasema hapa kwamba tuna matatizo makubwa sana ambayo yanatukabili katika nchi yetu.

Kwa hivyo, kufanya jambo ambalo baadae tutakuja kuingia katika mitihani mikubwa, basi ni bora kuliacha. Mtume (S.A.W) anasema utakapolifanya jambo lifikiri baadae litakuwaje mwisho wake, likiwa lina kheri jambo hilo basi lifanyeni, likiwa jambo hilo halina kheri basi liwacheni. Kwa hivyo, mimi ningeliomba serikali ikawa na subra kama walivyosema wawakilishi wenzangu, viongozi wetu tunawapenda sana na tunawapenda kwa amri zote.

Mhe. Spika, ni kwamba ipo haja ya kumtii kiongozi wako na tunawaheshimu sana, lakini tutizame ni athari ya baadae na wakati huu tulionao wakati hali yetu ya nchi ni ngumu sana. Kwa hivyo, ipo haja Mhe. Spika, kuona mswada huu tuurejeshe angalau tutizame baadae.

Mhe. Spika, kwa kweli mafao ambayo wamewekewa viongozi kwa uwezo nchi yetu ilivyo haya ni makubwa mno. Mhe. Spika, hivi sasa kuna zile pesa wanazopewa wawakilishi za majimbo na wawakilishi wengi wa majimbo wananchi hawaamini kama wawakilishi hawapewi pesa hizo. Kauli yao wanajua kwamba wawakilishi pesa za majimbo wanatiliwa na wanazila wao. Mhe. Spika, kwa hiyo hali kama hii kama kweli pesa hizo zipo na ndani ya majimbo mna matatizo mengi sana, mimi ningeliomba kwanza hii hali tuione ilivyo.

Kwa kweli mimi nasema huu mswada Mwenyezi Mungu atunusuru kwanza wananchi wanasikiliza mswada huu ukipita basi tutapigwa mawe sote huko majiani. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, kwa hili serikali isituhukumu vibaya tuwapende wananchi wetu, tuwahurumie wananchi wetu tuone hili ni tatizo ambalo wawakilishi na wananchi mswada huu kwa kweli ipo haja yakuvumiliana kuweka angalau kwa siku za mbele. Mhe. Spika, sasa hivi kila siku kukicha hali iko ngumu ya maisha.

Mhe. Spika, serikali yetu hii ambayo wananchi walikuwa na matumaini makubwa sana hivi sasa wananchi wana hoja nzito. Mhe. Spika, mswada huu nadhani umetugusa sote kama ulivyosema wewe jana, kwa hiyo sisi tuko tayari kujichinja huku tukalia wenyewe tunataka tuone wananchi wetu mpaka sasa hivi masikio walivyoyasimamisha. Kwa hivyo, na mimi nashawishika kwamba mswada huu tukubali yapitishwe marekebisho makubwa mno, marekebisho ambayo mimi moja kwa moja nayaunga mkono yaliyotolewa na kamati. Mhe. Spika, marekebisho yale nayakubali tena kwa moyo wangu thabiti katika nafsi yangu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba huu mswada ushachangiwa sana isipokuwa sisi ni kutilia mkazo, lakini vipengele vyote kimoja baada ya kimoja kimeshachambuliwa hakuna kipengele hata kimoja kilichobakia.

Kwa hivyo, mimi nasema kusimama hapa ni kutilia mkazo kwa kuiomba serikali ifanye subra na mswada huu wala isione kwamba itakuwa ina dhambi kurejeshwa mswada huu, sio dhambi hata kidogo. Mhe. Spika, mimi nasema jambo unalolipenda mno basi pengine lina madhara baadae na lile unalolichukia pengine lina heri na wewe. Kwa hivyo, huku kupenda kwetu kwa huu mswada kwamba bado uwepo hapa basi hatujui baadae madhara gani yatatukuta. Naiomba serikali iwe na subra uurejeshe kwanza huu mswada

inshaallah baadae tutizame Mwenyezi Mungu atatupa kheri. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Fatma Said Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kufuta ya Ulipaji Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam.4 ya mwaka 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Nam.6 ya mwaka 1999 na kutunga Sheria mpya ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa baada ya Kustaafu pamoja na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo. Kwa kweli kwanza na mimi nitoe heri za mwaka mpya wa Kiislamu mwaka 1433 hijiria na vile vile nitoe pongezi za mwaka mpya wa kimataifa mwaka 2012.

Mhe. Spika, mimi nataka niungane mkono na wenzangu kuchangia mswada huu wa sheria kama walivyokwishakutangulia wenzangu kwamba bado ni mapema kupitisha sheria hii, kwani bado Wazanzibari wengi ni masikini. Mhe. Spika, jana nilipata mshtuko sana kwamba kila aliyesimama hapa kuchangia ni kuwa hali bado ni ngumu tena sana. Mhe. Spika, jana nilipata simu nyingi kutoka jimboni kwangu na kunambia kama ni mwakilishi wetu basi tumekupeleka pale kwa kututetea sisi wananchi kwa hiyo sisi tunasema kwamba mswada huu bado hatujauridhia.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri kwanza tunathamini kazi yako kubwa uliyoifanya lakini bado kutokana na hali ya nchi yetu kiuchumi, bado sheria hii tunasema irudi na hadi pale tutakapoona sasa maslahi ya wananchi yanaridhisha. Mhe. Spika, tuna wafanyakazi wetu wa serikali ambao bado kima cha chini cha mishahara hakiridhishi na hili ni jambo la msingi la kutizamwa kabla ya kuwatizama viongozi wakuu. Tunaambiwa pale tunapotaka kutizama maslahi yako wewe basi zaidi yaangalie maslahi ya mtu wa chini ili kushukuru zile neema za Mwenyezi Mungu. Mhe. Spika, kuna watu masikini ambao hata chakula cha kutwa basi anakula mara moja, hili ni jambo la msingi na sio vibaya kwamba sheria hii ipelekwe mbele, na tumeona hapa kwamba sheria hii ya mwaka 1999 ambayo ilipitishwa hapa tunasema bado sheria hii irudishwe hadi pale tutakapoona sasa tunaweza kufanya hivyo.

Mhe. Spika, vile vile kwa upande mwengine hili ni suala ambalo hatujaliona, hivyo kila siku tunapiga kelele wanawake wawe mbele, lakini mswada huu mwanamke haukumtaja wala haukuonesha ushiriki wa mwanamke kwenye mambo haya ya uongozi. Kweli tukitizama kwamba mwanamke na yeye yumo katika ushiriki wa uongozi, lakini humu sikuona kwamba atatizamwa hivi na hivi.

Mhe. Spika, hapo Tanzania Bara sasa hivi Spika ni mwanamke basi tungezitizama hizi sheria tunapozitunga tutizame kwa mtazamo wa mbele zaidi, haitokuwa vizuri kila baada ya muda tunafanya mambo haya. Vile vile tumeona kwenye kifungu hiki cha 16 kuhusu huduma za wategemezi endapo Rais, Makamo wa Rais au Spika wa Baraza la Wawakilishi atafariki akiwa madarakani watoto wao watahudumiwa na mamlaka husika hadi watakapotimia umri wa miaka 20 au ikiwa mtoto wa kike pale atakapoolewa.

Mhe. Spika, mimi nasema kama mwanamke bado hajatendewa haki yake, kwa sababu kwa nini akiolewa akatishwe mafao haya, mimi nasema kama ni haki ningeomba itendwe sawa sawa mwanamke na mwanamme. Vile vile mtoto mwanamme anaweza akaoa pengine na siku hizi sisi wanawake huwa tunawasaidia waume zetu. Kwa hivyo, ikiwa ni kwa dhana hiyo hapa nayo isomeke vile vile, lakini isiwe upande mmoja kuna upendeleo kiasi fulani.

Mhe. Spika, kwa vile mengi wenzangu wameshayazungumza na mimi kwa niaba ya Jimbo langu la Amani nasema kwamba bado sheria hii kwetu ni mtihani. Kwa hayo machache nasema Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii.

Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia mswada huu. Mhe. Spika, kwa kweli mimi nilikuwa sina nia ya kuchangia huu mswada kwa sababu mimi ikiwa ni Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii ilikuwa tayari huu mswada tumeshauchangia na nashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili wametuunga mkono. Mhe. Spika, kilichonifanya niuchangie mswada huu kwa mara nyengine ni kwamba kidogo jana nilifikwa na matatizo nilipofika pale Darajani. Mhe. Spika, jana nilipofika Darajani watu walivyonivamia na wakasema kwamba nyinyi tumewachagua leo mnatuletea balaa kama hii, sisi tuliowachagua mnatuachia matatizo kama haya. Je, Mhe. Spika, mimi hili naliona ni tatizo kubwa sana.

Mhe. Spika, mimi sikuwajibu kwa sababu najua wananchi ni kawaida yao kuwalaumu viongozi wao, na ni kawaida yao kutaka ushauri vile vile kwa viongozi wao. Mimi niliwaambia ni kweli sisi tumo katika kuwatetea wananchi wetu. Mhe. Spika, basi ikiwa tutaupitisha mswada huu basi kuna hatari ya kutokea vurugu katika Unguja hii, kwani wananchi wote hivi sasa hawakubaliani na mswada huu kupita na mimi nikiwa ni mmoja wapo ninaekataa kuupitisha mswada huu.

Mhe. Spika, kwa kweli nchi yetu sasa hivi tusishangae hata sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupita njiani ukalembewa jiwe, kwa sababu sasa hivi wananchi wote hawana imani tena. Mhe. Spika, ikiwa ni mafao ya wastaafu

wakati umeshapita miaka 10 waliokaa katika Urais sio kidogo mtu anaweza kufanya kazi zake na anaweza kujipanga na akaweza kuwahudumikia watoto wake. Leo ikiwa tunataka kuzidi kuwadidimiza wananchi wetu kwa kuwaptishia mapesa yaliyokuwa sio kidogo, hili ni tatizo kubwa sana.

Mhe. Spika, na ikiwa ni wajane pia na wao kila watakachopewa hawana haja ya kutumia kwamba na watoto wao wapate mafao tena, hili ni tatizo kubwa sana kwa sababu mtoto yule utakapompa pesa hizo hata ile hamu ya kuolewa itakuwa hana kwa sababu atasema mimi bado natumia mafao inabidi sasa hivi siwezi nikaolewa. Mhe. Spika, sisi wajumbe ikiwa tutaupitisha mswada huu basi tutabeba dhima kwa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, sasa hivi serikali inasema kwamba haina pesa lakini pesa hizi za kuwapa hawa viongozi wastaafu zinatoka wapi? Hivi sasa tuiangalie serikali hata meli ya kusafiria haina, hivyo vimeli tunavyokwenda navyo basi hata hujaanza kuingia humo ndani ya meli basi unakuwa tayari umeshakuwa na gamu. Leo badala ya kutafuta mambo ambayo yataitengeneza nchi yetu, leo tunatafuta mambo yakuwarundikia viongozi mapesa ambao tayari wao wameshatumikia nchi hii. Kwa hivyo, mimi naiomba serikali hili suala kwanza liliweke upande kwa sababu watu wetu waliotuchagua hawatokuwa na imani na sisi. Mhe. Spika, mimi baada ya hapo nasema nakushukuru sana mheshimiwa.
Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii adhimu asubuhi hii ya leo na mimi kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kupata uzima wa afya na kuweza kutoa mawazo yetu katika mswada huu wa sheria uliowasilishwa jana asubuhi hapa Barazani.

Mhe. Spika, kwanza naunga mkono marekebisho yote yaliyofanywa na kamati hii na jana yakasomwa hapa na Mwenyekiti wa Kamati, lakini bahati mbaya marekebisho hayo hayakuingizwa katika mswada huu. Kwa kweli tumeona sisi wajumbe kwamba kama waziri aliyafuata yale marekebisho basi mswada huu ungeliturahisishia kazi sana.

Mhe. Spika, mimi binafsi nataka nitie baraka zangu kidogo katika mswada huu, nije katika ukurasa wa 294-295 suala la mwisho kabisa linaloelezea kiongozi wa kisiasa. Mhe. Spika, jana hapa paliogelewa sana, lakini na mimi nasema niingize na mimi fikra zangu hapa kuna suala zima la mshauri maalum wa Rais. Mimi kilichonifanya nitilie nguvu hapa ni kuhusu kifungu cha Katiba 5 (a) kwa hivyo Katiba tumeandika wenyewe kwa mikono yetu wakati tumeiandika basi ni vyema kuiheshimu na Katiba ikaweza kuchukua mkondo wake.

Kwa hivyo, suala hili Mhe. Spika, tusilipige mgongo tujali sana maandiko yetu, lakini katika kifungu hicho cha 58 cha Katiba pia kimeeleza kuhusu huyo

mshauri. Mhe. Spika, jana kilisomwa kifungu hiki lakini bado ni vyema kabisa kujali maandiko tulioandika wenyewe na kama tukiona kwamba ni lazima hawa washauri wawe ni viongozi wa kisiasa basi tungelimtaka Waziri wa Katiba na Sheria aandae mabadiliko ya Katiba hii ili kuweza kuyapitisha kwanza halafu na hawa wakaingia kisheria na kikatiba.

Mhe. Spika, sasa nije katika ukurasa wa 298 sehemu ya nne kuna mafao kwa viongozi wengine wanaoshika ofisi za kisiasa, kuna neno limeandikwa asilimia maalum. Mhe. Spika, hapa mimi nasema sheria imejifunga haikutoa tafsiri ya asilimia maalum. Kwa hivyo, tunakokwenda ni wakati wa ukweli na uwazi kwa hiyo ikiwa kuna mambo tunayabana huko mbele basi sheria itakuwa kutuhukumu. Kwa hivyo, mimi hapa siko radhi kabisa na neno hili la asilimia maalum, hivyo ni vyema kabisa Mhe. Waziri akatamka bayana ni asilimia fulani.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nije katika ukurasa wa 300 katika jadweli, hapa pia nina wasi wasi kwa sababu mambo ambayo kutokana na upya wangu sijayafahamu kuna mtu aliyeshika nafasi ya Rais wa Zanzibar atakaposita kuwa Rais anastahiki kulipwa. Mhe. Spika, Katiba inasema kwamba Baraza la Wawakilishi ndio wanaopanga mshahara wa Rais, lakini hapa sisi tunatakiwa tupitishe asilimia hizi, asilimia ambazo hatujui Rais analipwa vipi. Kwa hivyo, pengine inawezekana mshahara wake ukawa ni mdogo kwa hivyo inabidi tukija tukipitisha asilimia hizi itakuwa tunaidhlilisha nchi na wananchi. Kwa hivyo, nasema tunakokwenda ni wakati wa ukweli na uwazi, namuomba sana Mhe. Waziri aweke bayana tufahamu Wajumbe wa Baraza namna gain analipwa rais na tuangalie asilimia hizi je, rais wetu tutakuwa tunamdhulumu au tutakuwa tunamuweka katika hali halisi ya mafao haya.

Lakini pia suing mkono kifungu (d) posho la matunzo ya kila mwezi kuwa sambamba kwa asilimia 80 kutokana na rais aliyepo madarakani. Rais aliyepo madarakani Mhe. Spika, juzi nilisikia Mhe. Bi Asha alimuomba rais kwamba Baraza hili lina haki ya kuja kukutana naye, kwa hivyo, tukijaaliwa kama Baraza zima litakwenda kuonana na rais basi ni ugeni mkubwa huo, lakini rais atakaekuwa nje ya madaraka si rahisi kupata ugeni mkubwa kwenda kuonana naye.

Sasa ikiwa yeye yuko nje lakini kapewa asilimia 80 rais aliyeko madarakani pengine ana asilimia 100 basi itakuwa huyu tumemrundikia pesa nyingi hatimaye anaweza kuja kupata uchizi. Kwa hivyo, ni vyema asilimia hii 80 kwa rais aliyestaafu au Makamu wa Rais basi kufupishwa ili kabisa ili iende na wakati wake mheshimiwa huyu.

Katika kifungu cha (h) watumishi wane wa ndani na walinzi wawili. Kwanza huyu rais bwana ana watoto huyu na watoto wanatakiwa sana waitumikie familia, lakini ikiwa kuna watumisi wane tu watoto pengine watakuwa hawana hata nafasi ya kuonana na baba yao. Kwa hivyo, mimi sioni kwamba tumuwekee watumishi wane staff wetu, ni vyema kifungu hiki kikafanyiwa mabadiliko baada ya wane angalau wawili.

Mimi naunga mkono suala hili kwamba hatuna haja ya kurundika maofisi Mhe. Spika. Sisi wajumbe wa Baraza lako la Wawakilishi tuko 50 lakini toka lianze Baraza hili Zanzibar hakuna mwakilishi hata mmoja aliyejengewa ofisi, hebu kwanza serikali iwajengee hawa wawakilishi wa majimbo angalau wawe na ofisi.

Kwa sababu Mhe. Spika, kila mwakilishi yeye ni Waziri wa Elimu, Waziri wa Fedha, Waziri wa Afya ni rais, kila mwakilishi huduma zote sasa hivi anazifanya Mwakilishi wa jimbo, lakini ukitafuta angalau hiyo ofisi ya mwakilishi watu wakifikwa na matatizo haipo, lakini mtu keshastaafu wajengewe ofisi hebu kwanza serikali iwajengee hawa wawakilishi wetu. Kwa hivyo, siko tayari kwamba viongozi hawa wajengewe ofisi maalum ni vyema kama walivyoshauri wenzangu kwamba kutafutwe katika nyumba yake japo chumba kimoja iwe ndio ofisi yake.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, kuna kifungu (j) wasaidizi wa karibu wawili, huu ukaribu hapa sijaufahamu, ukaribu wa familia, wa uongozi au ukaribu wa nini? Namuomba Mhe. Waziri huu ukaribu hapa atueleze na kama ni ukaribu wa familia basi watoto wake wanamtosha, labda ichukuliwe kwamba kuna kingozi mstaafu hakujaaliwa kuwa na watoto atafutiwe watu hawa na iainishwe hasa kwa yule kiongozi ambaye hakubahatika kuwa na familia kuliko kusema viongozi wawili wa karibu. Lakini kama atakuwa na watoto nahisi kwamba watoto wake wanatosha kuwa wasaidizi wake wa karibu.

Mhe. Spika, ukiangalia haya mafao yote tutakayowatilia viongozi wetu wa kisiasa tutakwenda kwa uchumi gain, ina maana kodi zilizopo ndani, nyumba za serikali wanazolipa kodi watu itafika kipindi iwe tumelipa kiongozi mmoja viongozi wengine wanasubiri maposho yao. Mimi ningeishauri sana serikali kwamba kila siku tunapiga kelele kuwa Zanzibar tuna mafuta yamerundikana tu, lakini suala hili la mafuta ambalo ni suala moja la kuinua uchumi linazungumzwa lakini halifikishwi mahali tukajua maendeleo yake nini. Kwa hivyo, kwa nini kwanza serikali haipambani na suala hili tukayatafuta mafuta, tukayachimba tukanyanyua uchumi na baada yake tukapigiana mahesabu haya. Nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, kwana namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kunipa fursa hii leo kuchangia mswada wetu huu. Mhe. Spika, wenzangu wengi wameshachangia, wameshasoma vifungu lakini na mimi kwa vile haki yangu kuchangia na mimi nitapiga hivyo hivyo lakini nitazungumza kwa jumla jumla.

Mhe. Spika, mswada ni mzuri lakini kutokana na hali yetu na nchi yetu ilivyo na sisi tulivyo mswada huu bado ingali mapema. Kwa sababu huu mswada unazungumzia viongozi wastaafu wapewe mafao, wajengewe maofisi. Tukizungumza neno kustaafu maana yake ni mapumziko sasa ikiwa rais tunamjengea ofisi bado hatujampumzisha tunamuwekea matatizo, ilivyokuwa tunamuwekea matatizo itakuwa bado rais hajawa mstaafu. Kama tunataka kumjengea ofisi basi ajengewe ofisi kwake inamtosha na ninaamini marais wote wana majumba na vyumba vyao vinamiliki ofisi. Kwa hivyo, maoni yangu naishauri serikali kwamba marais wastaafu wasijengewe maofisi itakuwa ni hasara.

La pili katika mswada wetu huu tunasema kwamba rais mstaafu apewe posho linalosema 80%. Je, uchumi wetu unaturuhusu kwa hivi sasa kuwapa marais wastaafu na kwa nchi yetu tunayoweka kila baada ya miaka kumi tupate rais mstaafu kwa muda wa miaka 20 tutakuwa na wastaafu wangapi? Kwa hivyo, mimi naishauri serikali kwana hili liwekwe.

Mhe. Spika, serikali naiomba hivi sasa ikajipange kutizama uchumi wa nchi kuangalia uchumi wa nchi baada ya kuhakikisha tumepata uchumi wetu mzuri huko mbele tunaweza tukafanya hivi, lakini hivi sasa bado hali yetu ni mbaya. Tuna wananchi wetu hivi sasa wengi hawana ajira serikali imefuta ajira kwa sababu haina fedha sasa hawa wastaafu zitapatikana wapi za kuwalipa kila baada ya mwezi? Serikali yeti hivi sasa ina jukumu la kujenga skuli kuna mabanda mengi sana hayajaezekwa kwa sababu serikali haina pesa je, wastaafu hao watapewa kitu gani na ofisi zao zitajengwa na nini.

Tumejenga hospitali zetu nzuri lakini hivi sasa ukienda malalamiko ya dawa kwamba hakuna serikali haina fedha nab ado tunasema kwamba viongozi wastaafu wapewe fedha nyingi wajengewe maofisi. Mhe. Spika, naiomba serikali ikajipange kwanza kuboresha uchumi angalau wananchi wetu wawe na hali nzuri. Kuna watu masikini hivi sasa kama walivyosema wenzangu kuwa kuna watu hata cha kukila hawana sasa tunageuka mabuku kwa sababu buku anakusanya ndani ya shimo lake tu, ukiweka nazi yako ndani ya nyumba huioni buku ameshaitia ndani, sasa na huu uchumi wetu tunafanya uchumi wa buku wananchi wetu tunawalaza na njaa lakini mapesa tunayo. Mhe. Spika, tusifanye uchumi wa buku.

Kuna wafanyakazi bado tunasema wamezidishiwa mshahara lakini bado hata hiyo asilimia yao hawajaipata. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwanza tujipange katika hali ya uchumi, tutafute nyanja za uchumi, serikali itafute nyanja za uchumi, uchumi utapokuwa mzuri sisi rais tunaweza tukampa kila kitu. Kwa hivyo, sisi viongozi baso tusiwe na uroho wa kutaka fedha nyingi wakati nchi yetu ni nchi ya kimasikini kwanza tuangalie nyanja za uchumi.

Nchi yetu mpaka sasa hivi barabara hatuna, umeme hatuna, viwanda hatuna, lakini tunatafuta uwezo wa kuwapa marais fedha nyingi na kuwajengea ofisi nyingi, bila ya uchumi mzuri tutakwenda? Nyanja tunayotegemea sasa hivi ni ya utalii basi ukianguka utalii tumeanguka. Naiomba serikali na ninaishauri kwanza tuboreshe uchumi, uchumi wetu ukiwa mzuru mambao yetu yatakwenda, wananchi wetu hivi sasa hali ya mchele tunaoutegemea mapembe shilingi 1,600/2000, kuna wengine uchumi wao ni Mungu mkubwa tu, sasa Mungu mkubwa mpaka jioni hana chochote kalala, hana kazi ya kufanya, hana ajira, hana chochote.

Mhe. Spika, naisisitiza serikali kwanza tuboreshe uchumi nchi yetu masikini, wananchi wetu wengi sana wanyonge, tuangalie matatizo yetu tuyaboreshe kwanza ndipo tuweze kufanya makisio ya marais, mawaziri kuwapa pesa nyingi lakini hivi sasa bado Zanzibar hairuhusu tunasema haina fedha, mabarabara yetu mabovu.

Mimi Jimbo langu la Matemwe kule kuna barabara hazipitiki, hakuna umeme, wananchi hawana ajira, sasa wakisikia mimi Mwakilishi napewa shilingi milioni 30 kwa mwezi si watanipiga mapanga? Kwa hivyo, naiomba serikali kwanza tujipange katika hali ya uchumi, twende katika uchumi, tuwasomeshe vijana wetu. Kuna vijana ambao wanataka kusoma bado hata ule mkopo wa elimu ya juu hawajapewa fedha na tunataka tuwasomeshe.

Kwa hivyo, naisisitiza serikali, naiomba sana tena naishauri kwamba tuangalia hali ya uchumi wetu, tuboreshe hali ya uchumi wetu uchumi wetu uko chini.

Mimi Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba mimi ni mtu wa mwisho au kichinja mimba sitokuwa na mengi sana ila naishauri serikali iangalie sana wananchi wa Zanzibar Unguja na Pemba wamo katika mashaka makubwa ya dhiki hasa mchele. Mhe. Spika, mchele umepanda bei watu hawawezi kuununua sasa serikalia si vibara kufikiria kupunguza bei ya mchele huu wananchi wako taabani.

Mswada wende ukafikirie maslahi ya wananchi kwanza bila ya kufikiria maslahi ya marais wastaafu, marais wastaafu tutawafikiria baadae baada ya kuhakikisha uchumi wetu umekuwa mzuri sio hivi sasa, sasa hivi bado serikali yetu ya Umoja wa Kimataifa ndio kwanza inatambaa mwaka mmoja haijafika hata kudatua maana yake ile kusimama haijafikia angalau ifikie miaka miwili itakuwa haijambo. Lakini ndio kwanza mwaka mmoja tunampa rais maofisi, asilimia 80 tunazipata wapi Mheshimiwa?

Mhe. Spika, kwa kumalizia dakika zangu mbili naiomba serikali hivi sasa iangalie kuna vijana wengi sana Zanzibar hawana ajira, kuna mabarabara hayajajengwa, kuna sehemu maji hazina. Mimi huamini kule mjini kote kuna maji, lakini nimetembea sehemu za mjini kuliko kwetu Matemwe. Sasa tatizo kubwa linalotukabili ni kwamba tutafute nyanja za kuwaboresha wananchi wapate maslahi mema.

Kwa kumalizia mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe nitaunga mkono mswada huu pindipo maslahi yetu yakiboreshwa vizuri. Ahsante.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu Subbhanahu Wataala aliyetujaalia uhai, uzima tukafika hapa katika Baraza lako hili tukufu tukiwa wazima na kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Pia sina budi kukushukuru na wewe Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika mswada ulioko mezani wakati huu.

Mhe. Spika, kabla sijaanza na mchango wangu nianze kidogo na kutoa historia, naomba uniruhusu kufanya hivyo. Mhe. Spika, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu yaliyofanyika basi alilenga fikira na mawazo yake yote kwa wanyonge, alitangaza wazi wazi elimu bila ya malipo kwa wanyonge wasiokuwa na uwezo, alisema matibabu bure kwa wote, aliboresha makaazi ya wanyonge kwa wote.

Baada ya kuyasema hayo Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa matumaini ya Wazanzibari katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya kutimiza mwaka mmoja inatuletea mswada wa sheria wa mafao ya viongozi wastaafu uliokithiri maajabu.

Mhe. Spika, hali hii ya kuletwa mswada huu mbele ya Baraza lakjo tukufu ningesema kwamba wakati wake bado haujafika, unapohitaji kupika au

kutengeneza jambo basi maandalizi ni suala la msingi, ilikuwa ipo haja ya maandalizi haya kwa utaratibu ulio mkubwa ambao umepima na kufanya utafiti katika kukuza uchumi wetu au pato la taifa letu.

Nikiendelea na hili nadhani sote ni mashahidi usiku wa tarehe 9 kuamkia tarehe 10 Septemba, 2011 taifa hili lilitandwa na msiba mkubwa ulio mzito sana kwa kufiwa na rasilimali watu ndugu zetu Wazanzibari pamoja na Watanzania kwa kuzama kwa Meli ya *MV Spice.*

Mhe. Spika, hata ripoti ya kamati ambayo imeteuliwa haijaja Barazani kwa masikitiko makubwa serikali inatuletea mswada huu wa kuwalipa mafao viongozi wastaafu hali ya kwamba ndugu zetu waliotutoka hawana usafiri wa uhakika wa meli na hilo lilitamkwa wazi wazi kwamba hakuna fedha za kununulia meli hiyo. Hii ni kuwavunja moyo Wazanzibari ambao wamejenga matumaini katika taifa lao serikali ambayo ni ya Umoja wa Kitaifa.

Mswada huu Mhe. Spika, unanipa mashaka makubwa ya kujiuliza serikali hutupangia mipango mbali mbali ya kusema inataka kuboresha afya za kinamama na kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto, hali ambayo kwa kweli kwa sasa ipo na imekithiri kwa kukosa kula za kutosha kwa wanawake.

Huduma hizi zimekuwa duni mno wanaoishi mjini labda wenzetu tuwaambie wana unafuu fulani, lakini sisi tunaotoka vijijini tunashuhudia wenzetu ambao ni wajawazito na ndio wazazi wa taifa hili wanashindwa hata na mlo mmoja kwa siku, kilo ya mchele imepanda kiasi cha kupanda, sote ni mashahidi ushuru haukuongezwa lakini tayari mchele unapanda bei siku hadi siku sisi tunajipangia malengo haya.

Mhe. Spika, nisingependa niuanze mswada huu kifungu kwa kifungu, lakini baada ya kuupitia na kuuona kipengele baada ya kipengele na kuwaangalia Wazanzibari walio wengi jinsi walivyo wanyonge na walivyojenga matumaini unakatisha tama. Mswada huu ukitekelezeka kama utapitishwa na hali ya uchumi wetu ilivyo naamini kwamba njaa haitovumilika na hao ambao tunawatungia sheria hii ni watu wenye akili timamu wanatusikia, wanatuona kwenye vyombo hivi watajua kwamba kweli sasa umefika wakati wa mtawala na watawaliwa. Tutawagawa watu wetu katika matabaka ya kujua kuna watu wenye uwezo na watu ambao wataishi katika maisha ya kudhalilika jambo ambalo tuliliondoa katika kipindi cha miaka 48 iliyopita.

Mhe. Spika, hali hii si ya kawaida katika nyakati zetu hizi tulizonazo, huu ni wakati wa ukweli na uwazi, sheria na utawala bora. Hivyo, wananchi

wanatupima na wana vigezo mbali mbali vikiwemo huu mswada ambao tunautangaza hapa na tunauchangia. Wanajiuliza tuna wataalamu wangapi ambao wameihama Zanzibar kwa kukosa mshahara tu unaowakidhi haja tumewapoteza na hospitali zetu zimekaa bila ya madaktari wazuri na ma-*specialist* wamehamia kwa wenzetu.

Mhe. Spika, hebu turudi kwanza tuanze kuliangalia hilo, tuone kwamba madaktari wetu wale wazuri waliyoondoka kwa ajili ya kutafuta maslahi basi kwanza tuwe tunawagaiya wao kwanza waweze kubaki nchini kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa taifa hili. Tuna walimu wangapi wa sayansi wazuri wamehama katika taifa hili kuwatumikia Wazanzibari wenzao wamekwenda Tanzania Bara na kwengineko duniani kwa ajiliu ya kutafuta maslahi. Zanzibar serikali lazima kwa wakati huu ifikirie utaratibu wa kuweza kuwadhibiti watu hao na kuweza kubakia kwa ajili ya kuwatendea wenzao haki za kuwapatia elimu pamoja na afya inayostahiki.

Mhe. Spika, nikiendelea katika huu mswada nimeona wametajwa wengi ambao watapata mafao hayo ya wastaafu viongozi wa kisiasa. Lakini kaka yangu, jirani yangu wa Mfenesini Naibu Spika sikumuona yeye nadhani sijui yeye si kiongozi wa kisiasa, hili nalo pia nimelikuta humu. Hii inaonesha wazi kwamba kumbe kuna mambo maalum yaliyoteuliwa kwa ajili ya watu maalum

Mhe. Spika, wanawake wa Zanzibar ambao wamejikita katika kujiajiri katika vikundi vya ushirika sote ni mashahidi, waziri punde tu alisema akijibu swali, vikundi hivyo vimedhoofika na wanashindwa kupata mitaji ya kufanyia shughuli zao kwa nini tusiviboreshe hivyo na kuona kwamba wanazalisha mali kukidhi haja zao. Hayo ndio matumaini ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, mimi kama nilivyosema sina mengi najua unajitayarisha kunambia, lakini kwa niaba ya wanawake wenzangu wa Zanzibar mswada huu sitokuwa tayari kuupitisha mpaka pale ambapo hali ya uchumi wa taifa hili utaruhusu. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia machache katika mswada huu. La kwanza kabla sijaanza na mswada huu naomba kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri husika jinsi alivyokaa na kutafakari na kuzaa fikra ya kutafuta mafao ya viongozi wastaafu tukiwemo na sisi wenyewe wawakilishi. Lakini katika hilo naomba niseme kitu kimoja kwa Mhe. Waziri kwamba mswada huu ni mzuri sana na ni makini na tunawapenda sana viongozi wetu wastaafu tukiwemo sisi wenyewe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Lakini mswada huu ungekuwa mzuri

katika nchi zilizoendelea nchi tajiri, sio katika nchi maskini kama hii yetu ya Zanzibar kwa sasa.

Mhe. Spika, naomba nimwambie Mhe. Waziri katika hali tunayokwenda nayo Wazanzibari wanaishi katika maisha ya kubahatisha, hakuna mwenye uwezo wa kula, kunywa, kuvaa, kusomesha au kujitibu. Kwa hivyo, kwanza kabla sijaendelea niunge mkono ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, katika hali hii tunayokwenda nayo hivi kweli wananchi wa Zanzibar wa visiwa hivi watatuelewa vipi tutakapoupitisha mswada huu wakati kuna watu wana maisha magumu kupindukia na sote ni mashahidi. Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuliomo humu kila mmoja anaonekana yeye ni zaidi ya serikali, dakika chache tunazopumzika na hizi tunazokuwemo kwenye Baraza nayo kwa muda mfupi. Tukiwepo huko ndani ya majimbo yetu matatizo tunayoyapata ni makubwa mno na tokea jana Mhe. Spika, nataka nikuthibitishie mbele ya ukumbi huu simu tunazozipokea za matusi tunazotukanwa na wapiga kura wetu huko vijijini ni makubwa mno tunaona aibu tunaambiwa sisi kazi yetu ni kukaa hapa na kujilimbikizia maslahi.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Wete naomba kusema kwamba sitoupitisha mswada huu kwa sasa mpaka pale ambapo vipengele vitakavyopitishwa vifanyiwe marekebisho makubwa ili tuone uchumi wetu tayari ushakua vizuri ndani ya nchi tutaupitisha bila ya matatizo lakini kwa sasa ni mapema mno.

Mhe. Spika, wewe ni shahidi katika kikao kilichopita hapa kulikuwa na foleni kubwa ya wanafunzi walioomba mikopo na kukosa mikopo ya kuendelea na elimu ya juu jambo ambalo serikali inapigia kelele kila siku kuwashajihisha wanafunzi mambo ya elimu. Leo wanafunzi wamesoma wameshafikia viwango vya juu lakini ile pesa ya kulipia inawashinda na serikali pia imeshindwa kuwalipia mikopo ile kwa hiyo bado kuna tatizo.

Mhe. Spika, naiomba sana serikali hili lililodhamiriwa katika haya mafao ya kuwapa maslahi viongozi wote wa kitaifa wastaafu pamoja na sisi wenyewe wawakilishi, basi pesa hizi kwanza zitengwe katika maeneo muhimu ikiwemo elimu, afya, barabara, maji na mambo mengine yanayohusu jamii. Kila mmoja ana haki ndani ya nchi hii ya kuishi vizuri, hata Mwenyezi Mungu hatokuwa pamoja nasi tukiupitisha mswada huu katika kuwaboresha wachache ilhali wananchi walio wengi wanakufa na matatizo.

Mhe. Spika, kwa kuwa wenzangu wameshauchangia sana mswada huu kipengele baada ya kipengele sina haja ya kukuchukulia muda wako mwingi lakini bado naendelea kusema sitounga mkono mswada huu mpaka pale ambapo nchi yetu itaonekana tayari imeimarika kiuchumi ndio hapo nitaunga mkono.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba niulize swali moja. Hivi hii sheria nani anatunga, tunavyoelewa sisi sheria zinatungwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Sasa kama ni hivyo, imani yangu ni kuwa tokea juzi tulipokaa hapa au ni mara ya kwanza mswada huu umeletwa na umerudishwa. Kwa hivyo, naomba sana mswada huu urudi ukafanyiwe marekebisho pale ambapo tayari wakati utakuwa umeshafika nchi yetu inakwenda vizuri tutaunga mkono lakini kwa sasa hatuungi mkono mswada huu. Ahsante.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia japo kidogo Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ulipaji Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam. 4 ya 1988 uliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ilivyoelezwa hapa. Kwa sababu naona ndio kamati ambayo kweli imeleta ripoti mwanzo na yote wameyamaliza katika mswada huu kueleza yale yote waliyoyakataa na ni maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, kusema kweli mswada umechangiwa sana takriban na wajumbe wote wa Baraza hili. Mimi naungana nao kwa yale yote waliyoyachangia na kusema kwamba kama wenzangu walivyochangia wakakataa kupitisha mswada huu kwa mambo yaliyomo ndani ya mswada huu, basi na mimi sitokuwa tayari kuukubali mswada huu au kuupitisha kwa maslahi ya Wanzibari.

Mhe. Spika, sisi hatukatai maslahi ya viongozi wetu, sisi tunawapenda viongozi wetu sana na kila mmoja katika dunia hii anapenda hatima yake kuwa nzuri, iwe ni hatima ya hapa duniani au iwe ni hatima ya akhera. Sisi tunajua kama viongozi wetu wanatumikia nchi yao kwa nguvu zao zote lakini sio kwa hali hii iliyoorodheshwa katika mswada huu wa mafao haya ambayo yanastahiki kupewa wao.

Mhe. Spika, kama utakumbuka ingelikuwa serikali hii inayadumisha kweli kweli Mapinduzi ya mwaka 1964 kwa yale mafanikio yaliyopatikana basi kungelikuwa hakuna dhiki. Kwa sababu matatizo yote yaliyopo kwa raia wetu kwanza ni mambo mawili makuu ambayo yanachangia sana umaskini. Watu hawaathiriki kwa kula kwa sababu tukitazama kula matunda mengi tu yapo

katika kisiwa chetu lakini linalowaathiri wananchi zaidi ni kila kitu wanapokwenda kuchangia.

Mhe. Spika, tutazame katika suala la elimu mtu anapopasi mwanafunzi wake mmoja wa darasa la saba katika nyumba basi hali tena anashughulikia mwanawe tu mpaka atakapofika pakufika. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa matatizo hayo tuliyonayo hatuwezi kuupitisha mswada huu.

Mhe. Spika, mfano mwengine ulio hai twende katika suala la afya. Suala hili limekuwa gumu sana ambalo watu wengi hawana uwezo wa kulikabili, lakini bado serikali haijakaa ikatafakari ikaona ni hatua gani ichukue katika masuala hayo mawili makuu mazito na ndio masuala ambayo yanachangia watu umaskini.

Mhe. Spika, mimi sitaki niendelee sana masuala mengi yameshachangiwa nilisema na mimi tu nichangie ili nisije nikaonekana kuwa mswada huu naupitisha. Mhe. Spika, mswada huu siuungi mkono wala sitounga mkono kwa asilimia mia.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema. Pili kwa kuwa mswada huu tangu jana Waheshimiwa Wajumbe wamo katika kuuchangia na wamechangia vya kutosha. Mhe. Spika, kilichonisimamisha hapa ni kuipongeza Kamati kwa marekebisho yake.

Mhe. Spika, kwa kuwa matatizo mengi yanatukumba sisi akinamama mswada huu ningeiomba serikali iurejeshe ikaufanyie marekebisho tena. Ikiwa serikalini kuna mapesa mengi ningeomba mapesa haya wapelekewe akinamama hususan hospitali sehemu ya operesheni kwa sababu suala hili linatukera sana.

Mhe. Spika, kwa kuwa mswada huu umeshachangiwa sana naunga mkono iwapo utafanyiwa marekebisho vya kutosha na mimi nitakuwa pamoja na wenzangu nitaunga mkono.

Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, awali ya yote naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na amani katika nchi yetu. Lakini pili naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji na mimi katika mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ulipaji Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam. 4 ya 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Nam. 6 ya 1999 na Kutunga Sheria Mpya.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwasilisha mswada huu kwa wakati. Lakini pia nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa mchango wake wa jana jioni na niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia kwa kutoa mawazo yao.

Mhe. Spika, niseme kwamba hapa Barazani tupo Waheshimiwa Wawakilishi wa aina tatu, kuna wawakilishi kupitia majimboni, kuna wawakilishi wa viti maalum na kuna wateule wa Mhe. Rais, lakini sote ni wawakilishi na humu ndani sote tuna fursa na haki ambazo zinalingana.

Mhe. Spika, mswada huu bahati nzuri umepata wachangiaji wengi sana na wengine walisema hatuungi mkono, lakini ilivyo mtu anasema haungi mkono kwa sababu kila mmoja anatakiwa ajisemee mwenyewe. Mimi nianze kwa kusema kwamba nikiwa mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia. Kwa nini naunga mkono, naunga mkono kwa hoja.

Mhe. Spika, sheria hii tunayotaka kuitunga sio mpya kwa maslahi ya viongozi wastaafu, ni marekebisho ya sheria ambazo zilikuwepo. Bahati nzuri jana ama sijui Afisi ya Baraza la Wawakilishi au Mhe. Waziri alitupatia sheria zilizokuwepo hapo nyuma.

Mhe. Spika, kwanza kuna Sheria ya Maslahi ya Viongozi wa Kisiasa hii ilikuwa ya mwaka 1988. Sheria hii nayo inazungumzia maslahi ya viongozi wetu wakuu lakini baadae ikafanyiwa marekebisho mwaka 2003 na kuingizwa Waziri Kiongozi na mambo mengine nayo pia imezungumzia maslahi ya viongozi. Ukiangalia mambo ambayo yanazungumzwa leo na ukichukua haya marekebisho ambayo Mhe. Rais aliweka saini mwaka 2003 utakuta mambo ambayo Rais Mstaafu alitakiwa ayapate. Nawaomba ndugu zetu waandishi wa habari wapate muda wazisome wazipitie hizi sheria waone yale maslahi na mambo ambayo yamezungumzwa wakati ule na mambo ambayo hayatakiwi sasa hivi.

Mhe. Spika, hii sheria inazungumzia kwamba Rais Mstaafu kwanza atapata kiinua mgongo asilimia 50 ya mshahara wake wa juu lakini pia atakuwa na *wining allowance* yake ambayo itapewa kwa asilimia hiyo hiyo kwa miezi 24 ya kazi. Lakini atapata pencheni yake kwa asilimia 80 ya mshahara wake ambao anaupata wakati anaondoka madarakani yaani ule uliokuwa wa juu wa kiongozi.

Halafu kuna huduma nyengine asilimia 80 anapata nyumba au asilimia 50 kama anayo nyumba mwenyewe, matibabu bure, maji bure na umeme, watumishi wanne na walinzi wawili. Hiyo sheria inasema pia atapewa na ofisi wakati huo, atapewa na wasaidizi wawili, sekretari mmoja, atapewa na laki nne za matumizi ya simu kwa mwezi. Mwaka 2003 laki nne lakini leo 2012 laki tano tufikirie hebu tupime. Kama wakati ule laki nne mpaka sasa hivi laki tano ninahakika hata sisi Waheshimiwa Wawakilishi wakati huo wa 2003 mshahara na sasa umebadilika sana kiwango chake. Kwa hivyo, hivi tupime tusiangalie upande mmoja hilo la kwanza.

Lakini lile la washauri wengi wamesema si wanasiasa. Ukiangalia sheria ambayo ilitiwa saini na Dk. Salmin Amour Juma tarehe 2 mwaka 2000 ya maslahi ya viongozi inasema wanasiasa ni nani, ni Mawaziri, Naibu Mawaziri, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Washauri wa Rais sheria ipo. Hapa mara hii aliyeondolewa ni Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kwa sababu tumewaondoa kwamba si wanasiasa kwa mujibu wa Katiba mpya ya Zanzibar lakini mshauri hakuondolewa.

Kwenye Katiba ya Zanzibar kifungu Nam. 58(1) kinasema rais atachagua washauri, lakini 58(2) kinasema mara tu rais aliyewachagua washauri akiondoka madarakani na wao nafasi yao ya ushauri inakwisha pale pale. Hakuna mtumishi wa umma ambaye anaondoka kiongozi na yeye utumishi wake ukaisha, lakini washauri akiondoka rais aliyewateua siku ile ile na yeye ushauri wake unakwisha bila ya kuambiwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nahisi pengine hili ndio kubwa zaidi na nitalizungumza haraka haraka kidogo. Katika hii niliyosema kwamba sheria ambayo imefanyiwa mabadiliko, katika sheria ya 1999 kifungu Nam. 4(2) na 4(3) ambacho sawa sawa na kifungu kipya cha 19 na 20 cha sheria hii. Sheria ile ya 1999 kifungu Nam. 4(2) na 4(3) kinazungumzia kwamba hawa wanasiasa watalipwa viinua mgongo kwa miezi 60 ya kazi pamoja na *wining allowance* ya miezi 24. Kwa hivyo, ni miezi 84 kwa asilimia 100 ya mshahara wao hili ndio ambalo serikali imesema. Tusiangalie asilimia 100 tumruhusu Mhe. Rais kwa kushirikiana na Makamo wa Pili wa Rais na Spika waangalie asilimia ngapi itatoka kwa Waheshimiwa Wawakilishi badala ya 100. *(Makofi)*

Kwa mfano kama sasa hivi mwakilishi anapata laki nne mshahara, kwa miezi 84 atapata milioni 33,600,000/= kwa asilimia 100. Lakini mfano viongozi hawa wakae waseme watupe kwa asilimia 80 atapata milioni 26,880,000/=. Kwa hivyo, kila mwakilishi atapungukiwa na milioni 6,720,000/= ukifanya wawakilishi 80 ni milioni 537,600,000/=, bilioni 500,700,000/= zaseviwa na serikali hili ndio tatizo lenyewe lilipo.

Mhe. Spika, siamini kwamba sheria hii imekuja kuwadhalilisha wananchi, wala siamini kwamba tukiiitisha sheria hii tunaongeza matumizi ya serikali. Kwa sababu mfano hili la watoto wa viongozi hii ni sheria lakini hebu tufikirieni tuna viongozi wangapi ambao watoto wao hawajafikia miaka 18. Mhe. Dk. Amani Abeid Karume nafikiri hana mtoto wa chini ya umri wa miaka 18, Mzee Ali Hassan Mwinyi hana mtoto wa chini ya umri wa miaka 18, Mzee Aboud Jumbe Mwinyi hana mtoto wa chini ya umri wa miaka 18, sijui Dk. Salmin Amour Juma sina uhakika na watoto wake kama wako chini ya umri wa miaka 18. Waliobakia wote ni sheria tu lakini hakuna viongozi ambao tunakwenda kuwakabili.

Halafu haya ya kusema kwamba viongozi wengi wastaafu sio hoja. Kwa sababu Katiba yetu ya Zanzibar ndio inaruhusu hawa viongozi wastaafu kila miaka 10 lazima tupate kiongozi mmoja tukiona wengi tutabadilisha katiba. Lakini nahisi mimi katiba ni nzuri kila baada ya miaka 10 kuwa na kiongozi na viongozi wanakuwa na busara na bahati nzuri huwezi kuwa Rais wa Zanzibar kama hujafika miaka 40 ambapo wengi wanaacha kuzaa tena huko. Kwa hivyo, nafikiri hili halisumbui sana.

Mhe. Spika, mimi niwaombe wenzangu Waheshimiwa Wawakilishi wote kwanza tujue kwamba rais ni taasisi tusifikirie kwamba rais ni mtu tu, ni taasisi ambayo inaendeshwa kwa utaratibu, taasisi ambayo ina heshima, mamlaka na taasisi ambayo haiwezi kwenda kinyume. Tuna bahati kwamba viongozi wote tunaowapata wanakuwa ni wema sana kwa sababu rais ndio mwendesha nchi lakini bado wanatoa mamlaka kwa watu wengine kutengeneza sheria, kutengeneza taratibu na sisi tunaishi kutokana na maagizo yao na tunakwenda vizuri.

Sasa hii kazi ya urais ni kazi ngumu sana jamani na katika nchi ndio kama hivyo miaka 10 anakuwa ni mtu mmoja tu lakini wawakilishi tunakuwa wengi kwa pamoja. Tupo 80 kwa sababu pia ni kazi nzuri inasaidia watu lakini rais hawawezi kuwa wawili katika nchi moja, rais ni mmoja kwa wakati mmoja.

Halafu haya mafao tunaposema leo kwamba zingechukuliwa hizi zikanunuliwa madawati hizi tunazungumzia leo lakini sheria hii itafanyakazi baada ya kustaafu rais hawalipwi kila mwaka kwamba mafao yao ya kustaafu, rais akipewa mafao yake ya kustaafu ameshalipwa. Kwa hivyo, waheshimiwa wenzangu nafikiri hapa tueleweshane tukubaliane na hakuna kitakachoharibika, si kwa Waheshimiwa Wawakilishi lakini si kwa viongozi kwa sababu hii sheria imezungumza mambo mengi na ya maana sana.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba hata jana nafikiri alizungumzia Mhe. Ismail Jussa Ladhu akasema Uingereza wanazo sheria lakini hawaziandiki, lakini hiyo Uingereza mfalme wao wanamheshimu na familia yake na wanalipwa mambo mengi sana, sisi hatwendi huko kwa sababu hatuna ufalme na wanayoyafanya wao sisi hatuyawezi. Kwanza wao wana ufalme, lakini wao ni matajiri, sisi kwa umaskini wetu tuliunda sheria hizi tena sheria ya mwanzo nimeiangalia hapa ya mwaka 1990 imerekebishwa sana, imefanyiwa mabadiliko sana tumefikia hapa. Lakini hata ukiangalia jirani zetu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sheria hii wanayo na iko kama hivi ilivyo yetu.

Kwa hivyo, nafikiri hili tusione kwamba sisi dunia nyengine, nafikiri sasa wananchi wetu wanasikia tu lakini hizi sheria bahati mbaya hazijasomwa. Mimi nawaomba tena hawa waandishi wa habari wa redio, magazeti wazitafute hizi sheria zipo na sheria hazifichwi wazisome za kuanzia mwaka 1990, waisome ya mwaka 1988, wakaisome ya mwaka 1999, wasome na marekebisho ya mwaka 2003 halafu wajiulize jambo gani ambalo jipya limeongezwa katika sheria hii ambalo lilikuwa halimo na ambalo linapigiwa kelele na Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Spika, Mhe. Asha Bakari Makame kwamba linalopigiwa kelele ni x, hilo mimi nakubali kama ni hiyo sawa, kama Waheshimiwa Wawakilishi wanaipigia kelele x inawaumiza hapo sina tatizo lakini nahisi kwamba tusizunguke mbuyu twende moja kwa moja tuseme kwamba x inatuumiza, iwekwe moja kwa moja kama asilimia 90 au 70 ijulikane sawa au 50. Lakini tusiseme sheria hii mbaya inaumiza watu nafikiri tatizo letu ni dogo na linaonesha dhahiri kwamba ni jambo moja tu la x.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi kwamba sheria hii tuipitisheni jamani, sheria hii haikutengenezwa leo na Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame kwa kinyemela tu, sheria hii imeangaliwa vizuri na wataalam wetu tunaowaamini, serikali nayo ikajipa muda.

Mhe. Spika, jana nilisikia hapa watu wanasema kwamba rais anashauriwa vibaya, hapana rais anashauriwa lakini rais ana mamlaka ya kukubali na kukataa jambo lolote kwa mujibu wa katiba. Kuna mwengine alisema kwamba wanaotaka hii sheria ndio hawataki Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mimi naona hilo pia silo kabisa, serikali hii wala isibebeshwe mzigo kwanza inaanza kujitafutia maslahi hapana, hapa tunajali maslahi ya wananchi wetu wote na ndio inapobidi kuangalia kila sehemu.

Mhe. Spika, Mhe. Rais alianza kuangalia maslahi ya wafanyakazi wote wa nchi hii kwa kiwango kikubwa ingawa pesa haitoshi kwa kila mmoja. Lakini kajitahidi sana kaangalia maslahi ya wakulima kuanzia bei za karafuu mwanzo, lakini serikali hii hii imeangalia bei za pembejeo za kilimo na kuwasaidia wananchi, serikali hii inafanya shughuli za kimaendeleo. Inajenga barabara, vituo vya afya, hiyo *ICU* nayo. Kwa hivyo, haya mambo lazima tuyaangalie upande wa kulia na wa kushoto, tukiangalia upande wa kushoto peke yake tutapata hasara.

Mimi naomba jamani Mhe. Spika tunamuamini, Makamo wa Pili wa Rais tunamuamini na Rais wetu tunamuamini. Tulipotaka mikopo ya magari hawa hawa tuliwatumia na tukafanikiwa, kwa nini leo kwa jambo x tuwe hatuwaamini na viongozi ndio hawa hawa tunaowaamini. Mhe. Spika ni mtu mkubwa na ndio maana yupo katika viongozi wa kitaifa. Makamo wa Pili wa Rais na yeye ni mtu mkubwa, jamani waacheni hawa watuwakilishe vizuri, mimi naamini kwamba tutafanikiwa na sheria hii itapita kwa wawakilishi wote kuiunga mkono. Mhe. Spika, naomba nimalizie hapo. *(Makofi)*

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, kwanza na mimi niseme kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, sababu kubwa ya kuunga mkono hoja hii hata nisingekuwa Waziri ni moja kwamba mimi Haji Faki Shaali ambaye natoka katika Chama cha Wananchi *(CUF)* naogopa sana wananchi wangu wa Mkanyageni wakaja wakasikia kwamba mimi napinga sheria hii ambayo itampa nafasi Maalim Seif Shariff Hamad akistaafu aje apate gari na mambo mengine.

Leo wananchi wa Mkanyageni wanategemea Maalim Seif Shariff Hamad anazeeka kesho kutwa anastaafu, leo mimi napinga angalau aje apatiwe kigari na nyumba ya kukaa niipinge sheria hii. Kwa hivyo, nasema mimi lazima niunge mkono sheria hii kwa sababu sina ugomvi wala uhasama na Maalim Seif ambaye ndio Katibu Mkuu wa chama changu.

Mhe. Spika, naomba unilinde. La pili naomba nirudi katika Katiba ya Zanzibar ambayo nimeapa kuilinda naomba niisome. Mhe. Spika, Katiba ya Zanzibar ibara ya 38 inasema hivi: “itakuwa ni jukumu la serikali kulinda hadhi ya mtu yeyote atakayeacha kiti cha urais kwa sababu ya kutochaguliwa tena muda wake kumalizika, kujiuzulu au kwa sababu nyengine yoyote iliyo chini ya misingi ya katiba hii kama itakavyokubaliwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.” Katika *marginal note* inasema “Hadhi ya Rais aliyepita.”

Mhe. Spika, Katiba inatutaka kulinda hadhi ya Rais wetu, Katiba inatutaka kulinda hadhi ya Makamo wa Rais wetu, tunatakiwa tulinde hadhi ya Spika wetu. Sasa Mhe. Spika, wananchi wa kawaida maslahi yao yanalindwa na Sheria ya Utumishi wa Umma ambayo tumeipitisha hapa, viongozi nao wana sheria yao. Kama ingekuwa wafanyakazi wengine hatujaambiwa utaratibu wa kupata haki zao ikawa sisi tunajadili viongozi tu ingekuwa tunafanya dhambi, lakini hapa tumepitisha Sheria ya Utumishi wa Umma ambayo imetoa maslahi mazuri. Hivi juzi tumeongeza mishahara ya wafanyakazi kutoka laki tatu mpaka laki saba, sasa iwe dhambi kwa viongozi wetu hao kwamba wakistaafu tusiwaenzi.

Mhe. Spika, mimi siko tayari kumuona rais wangu Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein anastaafu anakwenda kuuza njugu. Siko tayari kumuona mzee wangu Balozi Seif Ali Iddi anastaafu Makamo wa Pili wa Rais anakwenda kuuza madoriani Kitope. Wala siko tayari kumuona Spika wangu wa muda mrefu Mhe. Pandu Ameir Kificho anakwenda Makunduchi kulima viazi vikuu analala njaa. Ndio nikasema hata ningekuwa *backbencher* mimi hili ningeliunga mkono wenzangu kama wangenisaliti potelea mbali lakini lazima sheria hii ningeiunga mkono.
(Makofi)

Mhe. Spika, hili suala la ushauri kwa daraja yetu ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa haamini Mshauri wa Rais mwanasiasa haya ni mabishano tu ya kisiasa hakuna asiyemini. Mhe. Spika, mtu yeyote aliyefika daraja ya kuitwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi anajua kwamba Mshauri wa Rais ni mwanasiasa. Yeye ndio hayumo katika Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mhe. Haji Omar Kheir, kwa hivyo *automatic* huyu ni uteuzi wa Rais na akiondoka Rais na yeye anaondoka.

Mhe. Spika, alisema Mhe. Machano Othman Said hapa kwa hivyo wewe bado unasema huyu si mwanasiasa, mwanasiasa si lazima uwe chama cha CUF wala CCM wala mwakilishi, hata Washauri wa Rais wanakuwa wanasiasa.

Wenzetu Marekani wamekwenda mbali zaidi, Marekani rais siku anayoingia White House wote washauri waliomo wanahama siku ile ile anaingia na wapya wote. Jamani hatulijui hilo tunaitwa wawakilishi hatulijui hilo jamani.

Mhe. Spika, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kamchukua Walter Rodney Guyana kuja kuwa mshauri wake, hatuyajui hayo jamani wawakilishi sisi. Kwa hivyo, lazima tujaribu kusoma vitabu japo vidogo vidogo vya Civics tuelewe mambo kama haya, lakini mwanasiasa kuwa hujui mambo haya aibu.

Mhe. Spika, jengine ni haya malipo ya mafao ya rais wenzangu wameyazungumza kama majadweli. Mhe. Spika, yale majadweli kama alivyozungumza Mhe. Abubakar Khamis Bakary jana yale majadweli ndio yale yale ya zamani. Sasa je, uchumi wa Zanzibar ulididimia hii miaka iliyopata kwa marais hawa wastaafu kulipwa mafao haya. Maana mambo mengine akilini ni udhanifu kabisa, ni *utopia,* hivyo uchumi wa Zanzibar hata tuseme marais wastaafu na Spika wasilipwe ndio kweli tutaweza kutatua matatizo yote katika nchi.

Kwa kweli haya mimi nafikiri tuwe ni watu wazima na ni watu wazima sisi tumeaminiwa na wananchi tukubali dhamana tulizopewa na wananchi tuwe makini. Itakapokuja kuwa jambo la kupinga tupingeni lakini la kukubali tukubalini. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe hili naomba sana lisipingwe liwe ni mjadala wa kuridhi.

Mhe. Spika, jengine hili la gharama, wachangiaji wengi wanazungumzia habari ya uchumi, lakini kumbe Mhe. Abdi Mosi Kombo kaja kaeleza vizuri sana, kasema kama ile x itarekebishwa tutaunga mkono hoja. Sasa waheshimiwa x ikibadilishwa ikiwa asilimia 100 uchumi hautaboreka, sifikirii kama tutalipwa maslahi yetu kwa asilimia moja kwamba tutaboresha uchumi wa Zanzibar, isipokuwa tutaboresha uchumi wa Haji Faki Shaali, uchumi wa Mhe. Machano Othman Said, uchumi wa Mhe. Rashid Seif Suleiman, nakusudia wawakilishi.

Lakini kama tutazungumzia hili nafikiri tuwe wawazi, tuwe wakweli na ndio kitu kitakachotusaidia. Mhe. Spika, hofu yangu sasa mwakilishi akisema mimi sipitishi mswada huu kwa sababu nitapungukiwa na mafao yangu hiyo ndio watapigwa mawe majimboni. Kumbe anakataa sheria kwa sababu ya ubinafsi wake, sheria na kanuni za nchi zinatukataza kuchukua sheria kwa maslahi yetu ya viongozi tusomeni kanuni vizuri. Hapa hatutakiwi tutunge sheria kulinda maslahi yetu, tunatakiwa tuangalie maslahi ya umma. Lakini ukisema siungi mkono mswada kwa sababu nitapungukiwa na kiinua mgongo changu sasa wewe ukipinga humu utapigwa mawe.

Mhe. Spika, mimi jana nimepita Darajani na dereva wangu sijapigwa mawe wala sijatukanwa. Kwa hivyo, mimi nafikiri atakayepigwa mawe ni huyu atakayekataa kuwaenzi viongozi wake kwa sababu tu kwamba yeye hajapatiwa asilimia 100 ya maslahi yake. Nawaomba waandishi wa habari hapa mtuelewe vizuri, mmepotosha taarifa ya habari kidogo naomba hapa mfanye marekebisho vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa mnayonipa pamoja na wasaidizi wangu mnatusaidia sana kuendesha shughuli zetu vizuri. Muda sasa umefika ili tukapumzike kwa ajili ya kuja jioni.

Kabla ya kuahirisha kikao nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Mawaziri, bila shaka inachanganywa na wale Mawaziri ambao hawana Wizara maalum nafikiri na Manaibu Mawaziri tubaki ndani ya ukumbi. *(Makofi)*

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Mhe. Haji Faki Shaali, Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, malizia dakika zako kama 10 hivi.

Mhe. Haji Faki Shaali: Nakushukuru Mhe. Spika. Mhe. Spika, mimi nilibakisha kiporo kidogo sana.

Utaratibu

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuzungumza jambo dogo kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika, Mhe. Haji Faki Shaali alipokuwa akichangia wakati wa asubuhi au mchana alitumia lugha kidogo sio nzuri kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Alizungumza kwamba, kwanza alizungumza lugha ya kejeli kwa wajumbe kwa kusema kwamba namna waheshimiwa walivyokuwa wanazungumza ni kama watu ambao kama lugha ya *antopia*. Sasa ile lugha ya *antopia* sisi wengine hatukusoma sana hatujui, lakini tunavyojua kama ni lugha za *stone age*, yaani watu wa zamani ambao hawakusoma, hawajui kile kitu ambacho wanakizungumza.

Sasa Mhe. Spika, lugha hizi kidogo za dharau hapa Barazani, sio nzuri na uhuru wa maoni kwa mheshimiwa basi kila mmoja ana uhuru wa kutoa maoni yake kama vile anavyohisi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba tu mheshimiwa arekebishe ile lugha yake ya kuwafanya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hawajui au hawakielewi kile wanachokizungumza, wakati kile walichokizungumza kiko sahihi na wala hakina matatizo.

Mhe. Spika, sisi ndio tuliopitisha katiba, sisi ndio tuliopitisha sheria na labda kwa kuwa sheria nyengine tunazozipitisha wananchi hawazikubali, labda ndio akatumia ile lugha ya *antopia*. Sisi ndio tuliopitisha sheria na katiba ambayo inamruhusu Mhe. Rais kuteuwa mawaziri na wengine hata waliokuwa hawana kazi yoyote na wakawa wanalipwa mishahara. Wananchi sio kwamba wameridhika, wananchi hawaridhiki, labda ndio *antopia* yenyewe, labda tunapitisha mambo ambayo wananchi hawaridhiki.

Sasa mimi nadhani mheshimiwa awe muungwana anapozungumza hizi kauli. Kweli mambo mengi tunayoyapitisha wananchi hawaridhiki nayo. Sasa sisi sote ndio *antopia*. Mimi nadhani mheshimiwa atuombe radhi kwa kauli yake ya kejeli kwa kutudhalilisha na kutudharau, kwa sababu maneno tunayoyasema kwa niaba ya wananchi waliotuleta hapa, ahsanate.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuweka sawa hili neno alilotumia Mhe. Haji Faki Shaali (MBM) Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum.

Mhe. Spika, neno hili sio antopian ni utopian, na ni neno sahihi la Kiingereza. Maana yake kwa Kiswahili ni *your are two theoretical your not practical*. Yaani hayo unayoyasema hayatekelezeki sio ukweli. Kwa hivyo, ni neno sahihi na halimtukani mtu kwenye *dictionary* kaliangalie liko wazi kabisa nini maana ya *utopian*, sote tumesoma siasa hapa. *Utopian theory* tizama wale ma-*politician* kina Kalimax na wengine ndio huko lilikotokea, ni neno sahihi la Kizungu ni *utopian* na sio *antopia.* Mhe Spika, ahsante sana.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, sina la kuongeza zaidi ya aliyozungumza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Spika, neno hili mimi sioni kama ni matusi, hili neno *utopian* maana yake ni mambo ambayo yasiyotekelezeka, *two theoretical* ndio maana yake. Hata kama mtu ni mwanafalsafa aliyekuwa na mazowea ya kuita *utopian* ndivyo wanavyoita, sioni kama ni matusi au kejeli kwa kadiri ninavyofahamu. Labda sijui mwenzetu ni *dictionary* gani alilotumia atuambie, lakini kwa haya ma-*dictionary* mengine tunayoyafahamu sisi na tulivyosoma hili neno sio matusi kabisa Mhe. Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, sisi tuliyoyazungumza yote tunauhakika nayo na tuliyoyazungumza tumeyajengea hoja. Kwa hivyo, yeye azungumze ya kwake asizungumze dharau kwa wenzake. Kama anasema hayo

tuliyozungumza sisi hayatekelezeki au hayaeleweki, sasa hayo ni mawazo yake, lakini asitumie lugha sasa ya kutudhalilisha sisi. Sisi kitu tulichokizungumza kila kitu tumetoa na ushahidi na ndio maana tumenukuu kifungu kwa kifungu. Hatukuzungumza tu mambo ya jumla, tumekwenda kwa kifungu, ndio maana tukasema hiki hatukuridhika na hiki hatukuridhika na hiki hatukuridhika.

Mhe. Spika: hoja ya kwamba amewadhalilisha wajumbe kwa kutumia neno utopia, baada ya kutolewa tafsiri hii, vipi inaridhisha, Mhe. Hamza Hassan.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kama nilivyosema tuna uhuru wa kila mmoja kuchangia. Hii tafsiri aliyoizungumza mheshimiwa hapa, hiyo tafsiri bado mimi kwangu sio sahihi. Kwa sababu yeye lugha aliyoizungumza ya kutufanya kwamba sisi tunazungumza vitu ambavyo havina mashiko, wakati hilo suala sio kweli. Sisi kila tulichokizungumza kina mashiko, ndio maana tunakamata kanuni na ule mswada unakwenda kifungu kwa kifungu. Kwa hivyo, kitu ambacho tunakizungumza tunazungumza kwa uhakika.

Mhe. Spika: Kwa hivyo, bado neno utopia kwa tafsiri iliyotolewa haijamdhalilisha mtu, kwa tafsiri iliyotolewa na ndio maana nikakuuliza je, kuna maana nyengine ambayo unaifahamu juu ya neno utopia ambayo unahisi imemdhalilisha mtu yeyote. Kama unayo kutoka kwenye *dictionary* yoyote unaweza kuileta na tunaweza tukaichukua hoja hii baadae ili tukaona ni kwa kiasi gani inamdhalilisha mtu. Lakini tumsikilize Mhe. Abubakar Khamis Bakar, Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, mimi nilikuwa sipendi niingilie katika suala hili, lakini naomba nikupeleke katika kifungu cha 62 cha kanuni zetu. Kifungu hiki cha 62 kinazungumzia kwamba

Kifungu cha 62

"mtu ambaye anatoa utaratibu".

Ingawa Mhe. Hamza hakutaja kifungu na wakati mwengine kama mheshimiwa atanyanyuka bila kusema kifungu, itabidi tunyanyuke na tuseme utaratibu, kwa sababu utaratibu ni lazima utaje ni kifungu gani. Lakini tumemuachia kwa urafiki tulionao. Lakini katika kifungu hiki cha 62(2) yakishakutolewa hayo basi ni wewe Mhe. Spika, unaotakiwa uamuwe, haina haja tena kumwambia mtoa utaratibu kwamba aende akafikiri akachukuwe *dictionary*, hapana. Ni ofisi yako na katibu, katibu unaweza kumwambia aende akachukuwe *dictionary* likaletwa hapa likatizamwa, halafu wewe ndio utowe uamuzi.

Kifungu hiki pia kinatoa mamlaka ya kwako kuahirisha hata Baraza kuweza kulifikiria hili jambo.

Sasa Mhe. Spika, naomba sana utowe maamuzi yako wewe bila tena kurudisha huku, kwa sababu tutaendelea kuzungumza na kulumbana tu na wala hakuna maana. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Sikusudii niahirishe Baraza kwa sababu hili jambo tumeshapeana tafsiri. Lakini wacha tupate nafasi ofisi yangu na mheshimiwa pia aliyetoa hoja, haidhuru hakunukuu kifungu, akatizame *dictionary* halafu tufanye maamuzi baadae, lakini hivi sasa tuendelee na shughuli iliopo mbele yetu.

Mhe. Haji Faki Shaali endelea kutumia dakika 10 kutoa mchango wako.

Mhe. Haji Faki Shaali: Nakushukuru Mhe. Spika. Kwanza Mhe. Spika, ningependa kuwaomba wanasiasa wenzangu tukajenga ustahamilivu wa kisiasa. Kwa sababu tokea jana wajumbe wamekuwa wakitoa hoja kali na sisi tunacheka, hakuna aliyekasirika. Sasa nashangaa kwamba leo mheshimiwa ndugu yangu akaanza kukasirika na hii ni hali halisi ya kisiasa.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, utulee vizuri, tuwe na ustaamilivu wa kisiasa na pale utakapoliona jambo halikufurahishi basi ujaribu kuvumilia na hiyo ndio sifa ya uanasiasa. Wanasiasa wako wa makundi mawili. Kuna *traditional politicion* na kuna *scientific politicion*, lakini wote wanatakiwa bado tuelewe umuhimu wa uvumilivu wa kisiasa. Jambo hili nilikuwa Mhe. Spika, naomba kabla ya kuendelea.

Mhe. Spika, sasa nije katika mchango wangu. Mhe. Spika, nataka nisaidie kidogo na mimi kueleza ufahamu wangu kuhusu hoja ambayo kaizungumza Mhe. Mjumbe mmoja kwamba mswada huu ni wa kibaguzi, unabagua. Kwa sababu kwa nini Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri ni wawakilishi, lakini katika sheria hii hapa wanahudumiwa mbali mbali.

Mhe. Spika, nadhani mantiki ya kuwekwa hapa, ukiangalia katika kifungu cha 6 kuna mamlaka imetajwa pale, mamlaka husika. Kweli utakuta waziri na naibu waziri ni wawakilishi, lakini katika suala la maslahi yeye mshahara wake anachukulia serikalini, kwa hivyo hawezi kimaslahi tena yeye akajakuhudumiwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi, ni hivyo hivyo Rais na Makamu wake, hawa wametajwa hapa katika mamlaka husika wanahudumiwa na Katibu Mkuu Afisi ya Rais. Waheshimiwa wengine kila mmoja aliyehusika ameelezwa Katibu Mkuu gani atamuhudumia.

Sasa nadhani hapa Mhe. Spika, malengo sio ubaguzi. Dhamira ya hapa ni kuonesha tu kwamba kila mtu anahudumiwa na nani. Sasa hiyo nadhani sio ya kibaguzi, kwa sababu hata mishahara Mhe. Spika. Walimu mishahara yao inatoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, wafanyakazi wa kilimo mishahara yao hivyo hivyo inatoka kwa Katibu Mkuu wizara ya kilimo na kadhalika. Sasa huo hauendi kibaguzi, lakini huo ni utaratibu tu wa kugawana majukumu ya kazi. Hilo nilikuwa naona nilieleze, kwa sababu wananchi nje wanakotusikiliza wanaweza wakajenga hisia mbaya kwamba hata sisi humu ndani tunabaguana wakati hilo sio kweli.

Halafu Mhe. Spika, hii hoja ya kwamba viongozi tunajipangia maslahi. Pia hii mimi nasema sio kweli. Mhe. Spika, mswada huu unasawazisha mapungufu ya nyuma. Mhe. Spika, sio siri kwamba Rais aliyestaafu Mhe. Abeid Aman Karume kapata milioni 10 kiinua mgongo chake, sisi wawakilishi tumepata zaidi ya hicho. Sasa huwezi kuacha mapungufu kama haya Mhe. Spika. Mimi katika Jimbo langu moja la Mkanyageni lina watu kiasi 12,000, lakini Rais anaongoza watu milioni 1,200,000 kweli mimi nimshinde kiinua mgongo chake. Sasa ndio utakuta huu mswada umekuja kurekebisha mapungufu ambayo yalikuwepo, wala sio dhamira yake kwamba kututika viongozi maslahi makubwa.

Vile vile Mhe. Spika, nizungumzie huu mpango ambao ndio kiini cha nabishano, katika mpango huu Mawaziri hawamo ni Rais, Makamo wa Rais lakini mawaziri hawapo, sasa kama ingekuwa dhamira kwamba viongozi wanajilimbikizia mali na Mawaziri wangeingizwa hapa lakini hawamo. Mawaziri wao kabisa ndio tunakuja katika mpango huu wa *passent* lakini mawaziri ndio hivyo hivyo sawa sawa na wenzetu hawa Mhe. Spika, hatuna *passent* tumewekwa katika mpango maalum.

Kwa hivyo ile hoja ambayo viongozi walioko serikalini wanajipangia madaraka wananchi wamepoteza imani, serikali dhalimu nadhani hapa itakuwa hoja haina msingi sana, hii ni kwa viongozi wachache sana napa ndio pa kuiga Mhe. Spika, kama waheshimiwa Mawaziri ambao wote katika Baraza la Mapinduzi ndio wanaojadili mambo haya kwa nini basi wao hawakujipangia maslahi yao. Wapo katika lile lile kundi la pamoja na wawakilishi nadhani hiki ni kigezo kizuru kwamba na sisi katika Baraza tusilitumie Baraza kupanga maslahi yetu binafsi, tuige mifano ya Mawaziri wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kukaa wakasema na sisi tuingie katika mfumo huu wa viongozi. Mhe. Spika, baada ya ufafanuzi huo nimekuwa nimesaidia sana katika suala hilo.

Lakini pia jengine utamaduni wa Zanzibar Mhe. Waziri tunausahau kidogo, utamaduni wa Zanzibar juzi nilikuwa na Makamo wa Pili wa Rais jimboni

kwangu tarehe alikuja kufungua banda la skuli, pale alipokuja kwa sababu ni kiongozi wao zawadi kapewa mpaka madafu mimi sikupewa wala mtu mwengine hakupewa. Lakini ndio heshima ya Wazanzibari wale viongozi wao kuwazawadia na kuwatunza hili sio geni, siku zote viongozi hata mashehe siku zote shehe atakapokwenda pahala hata awe tajiri lakini lazima yeye anawekwa pahali ambapo ni *high table* na anapewa huduma maalum, hilo lipo pahala popote katika shughuli za kijamii.

Mwalimu hata kama uwe na uwezo wa kiadi gani basi wakikuta wanafunzi wako watakukirimu sasa haya mambo kidogo ndio utamaduni wetu unavyotuelekeza, kwamba tuwe tunawaenzi wazee wetu, tunawaenzi viongozi wetu, tunawaenzi mashehe wetu na tunawaenzi walimu wetu huo ndio utamaduni wetu Mhe. Spika, kwa hivyo hili jambo sio geni.

Mhe. Spika, jengine ambalo ni nasaha mimi nataka nirudie kwa kuwanasihi wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi wote, najua tofauti za mawazo lazima ziwepo na ndio binaadamu hiyo hatuwezi kuiepuka, lakini naomba kwa hili basi tuunge mkono mswada huu sote mia kwa mia, kwa sababu mbili Mhe. Spika, kwanza kwa madhumuni ya kuwaenzi viongozi wetu, lakini la pili kulinda heshima ya baraza letu. Mhe. Spika, hatutoeleweka na wananchi wala tusijidanganye hatutoeleweka na wananchi kwamba hatukuupitisha mswada huu kwa sababu ya visingizio vyengine vyovyote, wananchi watatufahamu kwamba hatukupitisha kwa maslahi yetu binafsi jambo ambalo itakuwa ndio kaburi letu kisiasa, kwa hivyo nawanasihi sana wanasiasa wenzangu tusijichimbie kaburi la kisiasa kwa wananchi.

Mwisho nataka niseme kwamba hii ni haki yetu kikatiba na niwajibu wetu kwa hivyo naomba tuitumie vizuri na wananchi wajenge imani na chombo hiki, kwamba wawakilishi wanapitisha jambo lenye maslahi na taifa lao na viongozi wao na sio tu hawapitishi jambo kwa sababu halina maslahi na wao. Lakini zaidi nataka tujenge taswira kwa vyama vyetu serikali hii ya umoja wa kitaifa inaundwa na vyama viwili, Chama cha Mapinduzi yaani CCM na chama cha Wananchi CUF hamna muwakilishi wa chama chengine. Ni haki wawakilishi wakosoe waelekeze kwenye marekebisho yafanywe, lakini tusije tukajenga taswira kamba vyama hivi havifai sasa kije Chadema au Chausa, kwa hivyo hilo mimi nalimba sana Mhe. Spika, kwa sababu tuko tutakakoelekea baadae huko, kwa hivyo naomba ishaalla Mwenyezi Mungu atujaalie tuupitishe.

Mhe. Spika, nakushukuru sana Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana na mimi

kunipa nafasi angalau kwa muda mchache kuchangia suala hili ambalo limetukabili hivi sasa, kwa hivyo nianze na kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwasilisha kwa utaratibu ambao sote tumeelewana.

Pia niwashukuru wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote ambao walipata nafasi ya kuchangia na kila mmoja alichangia kwa jinsi alivyohisi kwamba inafaa achangie na ndio demokrasia, kila mmoja anachangia kwa jinsi anavyohisi mwenyewe achangie. Nia zao wote walikuwa na ni ya kuhakikisha kwamba mambo haya yanakwenda vizuri mimi siamini hata mara moja kwamba suala hili lililokuwa mbele yao, kwamba hawaliungi mkono, wanaliunga mkono lakini kuna hili na lile pengine wangetaka wafafanuliwe ili wafahamu, ishaalla mpaka tukimaliza kutoa ufafanuzi huu basi yale makofi ambayo alipigiwa Mhe. Haji Faki Shaali asilimia mia moja yatapigwa tena kwa kuunga mkono.

Mhe. Spika, suala hili halikuanza leo au jana limekuwa likifanyiwa marekebisho kila wakati unapofika mafao ya viongozi wa kisiasa na mengineyo, lilianza zamani sana tokea wakati wa Marehemu Mzee Idrissa Abdullwakil likaendelea mpaka likafika wakati huu, kila lilipofika wakati wake lilifanyiwa marekebisho. Kwa hivyo sio kwamba suala hili limekuja mbele yetu likiwa ni suala jipya kabisa na lazima tuelewe kwamba Viongozi wetu hawa wakuu wanafanyakazi kwa kujituma, kwa kujiamini na tumewachagua sisi wenyewe wakati mwengine unaweza kutaka miadi ya kumuona Mhe. Rais unaweza kuchukua siku mbili au tatu sisi Mawaziri, sio kwa sababu hataki kutuona lakini kwa sababu ya majukumu aliyokuwa nayo mengi sana, kutwa nzima Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais kila wakati utasikia ving'ora vinakwenda huku na kule yote hayo kwa sababu wanatumikia wananchi.

Kwa hivyo lengo la jambo hili ambalo lipo mbele yetu Mhe. Spika, ni kuleta ufanisi na kuzingatia kwamba wenzetu hawa wamekuwa wakifanya kazi kwa kujituma sana kama wanavyofanya wajumbe wako wa Baraza lako fukufu wanavyojituma majimboni, wanafanya kazi majimboni usiku na mchana na alhamdulillahi mambo yao sio mabaya na yataendelea kuwa mazuri.

Mhe. Spika, kuna mambo mengi yamezungumzwa lakini kuna suala zima hili la asilimia ndio kidogo limeleta mjadala wa hapa na pale, Mhe. Rais katika hotuba zake ambazo amekuwa akizungumza kwamba atajitahidi kadri ya hali ya uchumi inavyoimarika kuweka maslahi ya wafanyakazi kuwa mazuri zaidi, yaani kwa lugha nzima ni kuongeza mishahara. Kwa mwaka wa kwanza alhamdulillahi ameshaanza mwaka huu tumeshuhudia sote mwaka jana,

tunatarajia na mwaka huu hali ya uchumi ikiimarika tutaendelea na mwakani mpaka ikifika mwaka 2015 basi hali hiyo itakuwa ni ya kuendelea.

Sasa ile kauli aliyoitoa Mhe. Rais ni kauli nzito sana yaani kuna *commitment* ya serikali na yake mwenyewe, hakusema kwamba atajiongezea yeye isipokuwa amesema atoongeza maslahi ya wafanyakazi, Rais hawazi kusema niongezeni lakini huyu ni biaadamu na sisi ni viongozi lazima tufikirie viongozi na wenzetu hawa. Kuna wakati Mhe. Omar Ramadhan Mapuri alikuwa na utaratibu pale Wizara ya Elimu hutoa zawadi kwa wafanyakazi bora, basi Wakurugenzi na walimu wakuu na hata mimi nilibahatika mara mbili tatu nikachaguliwa kuwa mfanyakazi bora, nikiwa mwalimu Mkuu wa Haile Selassie wakati ule nilipata zawadi ya Tanzania kwa usafi kwa hivyo mimi nikapata bahati ya kuchaguliwa kuwa mfanyakazi bora ngazi ya taifa na ngazi ya taifa huipati mpaka ufanye jambo nje ya mipaka ya Zanzibar au Tanzania, kwa sababu walifurahi basi mimi sio peke yangu lakini na wakurugenzi wengi na katibu wakuu na hata kiongozi Mkuu Kiongozi wakati yupo pale Wizara ya Elimu na wengine wote walipata nafasi ile.

Suku moja tuliweka kikao tukasema jamani huyu Waziri kama hatujamfikiria sisi huyu yeye hasemi kwa hivyo tujitahidi na sisi tuamue safari hii katika sherehe za Elimu bila ya malipo nae tumzawadie, tumefikia sisi yeye mwenyewe hawezi kujifikiria. Ingawa mambo yalikuja kuharibika mwisho kwa sababu tulikubaliana kwamba ile siri tusiitoe mpaka siku itakapofika lakini mambo yakawa mazito kwa mwenzetu mmoja ilibakia nusu saa siri ile akaitoa, akasema nimejitahidi lakini nusu saa iliyobakia mtanisamehe siwezi kujizuia kwa hivyo akatangaza kwamba Waziri atapewa zawadi hii nah ii.

Kwa hivyo na sisi tujitahidini kuzuia hili lakini sasa Rais mwenyewe hawezi kusema nipangieni hiki na hiki lazima tufikirie wenyewe suala hilo, na sio yeye tu wastaafu hawa wote tumezungumza, Mhe. Spika, tumemzungumza na miongoni mwa mambo ambayo Kamati ilipendekeza na tumeikubali hiyo katika serikali kwamba Spika, aweme katika watu ambao watashauriana na Mhe. Rais. Mimi naamini kabisa mia juu ya mia wakati Mhe. Rais atakapokushauri jambo hili naamini kabisa waheshimiwa hawa utashauriana na Rais vizuri na wote watafurahi pamoja na wengine watafurahi, hiyo nina imani kubwa kwa sababu unatupenda na ishaalla uendelee kutupenda kama tunavyokupenda wewe vile vile.

Lakini pia tukamuongeza na Mhe. Makamo wa pili wa Rais ili wote watatu wazingatie wakiwa na heshima na busara kwa suala hili, kwa hivyo isionekane kwamba kuna tatizo la kuweka hii *passentage* hii ikiendelea kuwekwa kwa asilimia mia moja, baada ya miaka mitano tukija tukiongeza mishahara mitatu

kupita hapo hakika tutakuja kufika pahali ambapo wananchi hawatotuelewa. Lazima tufikie pahali tutumie mpango ambao unakubalika vizuri, mimi nadhani ni jambo zuri tulikubali, ninachoamini kwamba hakitopungua kile ambacho tumekipata huko nyuma, lakini masuala haya ya mafao yanatuhusu mpaka sisi Wajumbe wa Baraza la wawakilishi.

Sasa tunaposema kwamba tulirejeshe tunafanya dhulma, tupige kura mmoja mmoja ili wananchi wajue nani anamdhulumu mwananchi, hee! *(Makofi)* mimi nadhani ahsanteni sana kwa kunifahamu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, haya masuala sisi wenyewe kama ni wawakilishi kila baada ya miaka mitano alhamdulillahi tunaondoka na fungu letu, tumekuwa tukifanya hivyo na wenzetu hawa vile vile wana wajibu huo kwa nini tusiwafikirie. Kwa hivyo mimi ninachoamini kwamba wana jukumu zito lakini sio wao tu, kabla hujawa Muwakilishi tofafuti ya mambo unayopata nyumbani tofauti na unapokuwa muwakilishi. Ukishakuwa muwakilishi na pengine umebahatika kuwa Waziri wageni wanaongezeka na sasa hivi jama wanakuwa wanakukumbuka kweli kweli kwamba wewe ni jamaa yao, matumizi yanazidi na kuongezeka.

Je, leo ukiwa Rais wageni wataongezeka mara kumi mpaka kumi na tano kwa sababu tayari umeshatanua wigo ule, kwa hivyo mimi nadhani jambo hili la kuliangalia vizuri familia zao zinahitajika pale wanapostaafu kuziangalia vizuri hakuna matatizo jambo kama hilo tuliangalieni vizuri. Pamoja na watoto wao lakini hebu tuangalieni na tujiulizeni Marais wote hawa ambao wamestaafu sasa hivi nani ambaye ana mototo ana umri chini ya umri ambao tumeutaja hapa, hakuna mimi siamini kwamba kuna mwenye mototo mwenye chini ya umri wa miaka kumi na nane au ishirini wote hawa. Sijui huko mbele ikija kutokezea hivyo lakini kwa sasa hivi huyo aliyeanza mwanzo mpaka sasa hivi hakuna mwenye mototo mwenye umri chini ya miaka ishirini.

Kwa hivyo ni kitu ambacho kimewekwa tu mfano kikitokezea sio kwamba ndio kipo hiki lakini imewekwa kwa sababu ineweza kutokezea na baadae mambo yakawa ni hivyo, lakini sidhani kama itaruhusu.

Mhe. Spika, kila hali ya uchumi inapoimarika ndipo maendeleo ya nchi yanapopatikana na sisi kila tukishirikiana kuijenga nchi hii kwa nguvu moja kama ilivyo sasa hivi katika nguvu za serikali ya umoja wa kitaifa mimi nina hakika tunaweza kufika mahala pazuri zaidi, kwa sababu nimeeleza hatari iliopo na kiwango ambacho kimewekwa kwa kutumia *formula*. Mhe. Spika, nadhani Waheshimiwa Wajumbe wakikaa na kufikiri basi hilo nawaweza kufika pahala wakakubaliana na sisi.

Lakini tusijenge *impression* kwamba jambo hili linadhalilisha wananchi, tunafanya dhulma, madeski skuli hakuna, mabuku, dawa hospitali hazipo. Sasa haya yamekuwa yakitendeka kila baada ya miaka mitano na *Alhamdulillah* kila baada ya miaka mitano ikifika haki zetu zile kama Waheshimiwa kisheria, kwa sababu zipo kisheria lazima serikali ifanye kila njia tuzipate haki zile.

Mhe. Spika, tume-*notice* awamu iliyopita vipindi viwili vyote hakucheleweshwa mtu, yaani ilipofika wakati tunamaliza Baraza nadhani na mambo yetu yakawa mazuri. Kwa hivyo, *Inshaallah* tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu kwamba mambo yaendelee kuwa mazuri, ili mambo yetu yaende vizuri zaidi.

Kwa kweli suala hili naliona moja kwa moja kuwa halina matatizo na tuendelee kulichangia sote tuliobakia, wafahamu Waheshimiwa Wajumbe wetu kwamba hakuna nia mbaya.

Sasa mawazo yao waliyotoa mimi ninahakika wakati tutakapokuwa tunapitisha vifungu, basi tutapatiwa ufafanuzi mzuri na wala tusiwe na mashaka na hayo. Kwa maana hiyo, kama ni binadamu palipokosewa patarekebishwa na palipokaasawa, basi tufahamishe nao watuelewe kwamba hapa pamekaa sawa, isiwe unakataa kwa sababu ya kukataa tu na hivyo itakuwa bado hujatusaidia wala hujaisaidia serikali.

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali sikuwa na mengi ya kuzungumza sana, isipokuwa nilisema nizungumze hayo machache, niunge mkono kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi. Kwa bahati nzuri sijapigiwa simu hata moja kutoka Jimbo la Makunduchi kusema kwamba hawakubali na jambo hili. Kwa hivyo, kwa niaba yao na wewe Mhe. Spika pamoja na wananchi wa huo tunaungana pamoja kuunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, na mimi jioni ya leo nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa miongoni mwa wachangiaji wa mswada huu ambao mjadala wake unaendelea hivi sasa.

Kabla ya yote kabisa Mhe. Spika, nataka nitoe heri ya mwaka mpya kwako wewe binafsi, Wajumbe wote wa Baraza lako hili tukufu, wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Wazanzibari wote. Mwenyezi Mungu ajaalie mwaka huu wa 2012, uwe mwaka wa mafanikio makubwa na heri kubwa kwa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba katika Baraza lako tukufu ni haki ya kila mjumbe kuchangia akitaka, yanayochangiwa hapa ni mawazo ya kila mjumbe. Kwa hivyo, inawezekana mawazo yale si mazuri au ni mazuri, lakini anayo haki ya kuchangia, uzuri na ubaya ama kufaa na kutofaa maamuzi yake yatajulikana baadaye. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika nawapongeza wote ambao wamechangia. *(Makofi)*

Sasa katika kuchangia huku hasa siku hizi, maana yake zamani Baraza hili wakati kuna mjadala kama huu lilikuwa halionekani pamoja na kwamba kulikuwa na wapiga picha wakati wote, lakini ilikuwa adimu kumuona Mhe. Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi akisikika pale wakati anaongea, yaani *live*. Lakini siku hizi si ajabu hivi ninavyozungumza kila ambaye anaangalia *Zanzibar Broadcasting Corporation television*, basi siajabu kuwa wananisikia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni umati mkubwa wanasikiliza haya tunayozungumza hapa, kwa kweli hapa ndipo pahala ambapo kile chakula unachokipika, basi watu ndicho watu watakachokula. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawasihi sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wakati tunapojadili hapa, basi tuzingatie hilo. Kwa bahati mbaya au nzuri ni kwamba kila mtu anao ufahamu wake, lakini likeshatoka Baraza hili kila mtu atachukua aliyofahamu mwenyewe. *(Makofi)*

Katika mjadala huu nilichokigundua ni kuwa wengi wa Waheshimiwa Wajumbe sisi wakati tunachangia mswada huu ama hatukuwa na habari kwamba kuna sheria mbili, yaani Sheria Nam. 4 mwaka 1988 na Sheria Nam. 6 mwaka 1999 na hata ile *amendment* yake iliyofanywa kwa Sheria Nam. 4 mwaka 2003. Sasa kama hilo hulijui au hukulisoma ndipo hapo tena jazba unazungumza mambo ambayo tayari yapo na wala si ya kuzungumza.

Mhe. Spika, wakati Mhe. Mjumbe anaposema kwamba mswada huu unapendekeza mpaka ofisi. Kwa kweli si mswada huu Ofisi ya Rais aliyestaafu umeelezwa mapema. Vile vile mtu anasema posho la simu kwa mwezi 400,000/=. *Amendment* ya *Act No*. 4 iliyofanywa mwaka 2003 posho la Rais ni 400,000/=. Sasa mwaka 2003 mpaka 2012 *almost* 10 *years* na gharama za simu mnaona zinavyopanda, hivi kweli katika miaka hii kuongeza 100,000/=, tutakwambia apewe 300,000/=.

Kutokana na hali hii, ndio inasema kwamba tatizo ambalo nimeliona ni kwamba Waheshimiwa Wajumbe sisi wengi hizi sheria mbili pamoja na

amendment yake hatukuzisoma au pengine tulikuwa hatuzijui kabisa tumeona kwenye *Act*.

Mhe. Spika, si Wajumbe wengi tunaosoma hata hiyo miswada wachilia mbali kutafuta kazi ya kwenda kwenye *library* pamoja na sehemu nyengine kwa ajili ya kuangalia miswada hii. Kwa hivyo, nilichokiona ni kwamba wengi hatukusoma katika sheria hizi mbili.

Sasa Mhe. Spika, jana wewe hukuwepo, lakini Mhe. Naibu Spika alikuwepo wakati Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria anachangia mswada huu una-*consolidate* sheria mbili na kuna vifungu zaidi ya asilimia 60 vimechukuliwa kama vilivyo katika sheria hizi mbili viko humu.

Kwa hiyo, leo ukivipinga na kusema vitolewa mswada huu kwamba uahirishwe kidogo inakuwa tabu mtu kufahamu. Kwa kweli watu wengi wanafahamu kuwa mswada huu ni mpya na wala jambo kama hili hakuna, yaani wanashangaa hasa kusikia kwamba Rais au Makamu wa Rais anapewa mafao, kumbe vitu vipo siku nyingi.

Lakini kama hilo halitoshi Mhe. Spika, inawezekana wapo Waheshimiwa Wawakilishi waliopata mswada huu kabla ya jana kujadiliwa, mswada huu uligaiwa kwa Wawakilishi wote. Kwa hivyo, nasema inawezekana wapo na kama wapo ni wachache mno waliotoka na mswada ule wakaenda jimboni wakakaa na watu wa jimbo si wote, isipokuwa wapo kikundi cha wataalamu kama vile walimu wa skuli pamoja na watu wengine kwa ajili ya kujadili na kupata mawazo.

Sasa mtu anaposema maana yake Wawakilishi tunayo tabia hiyo vile vile, kwamba mimi watu wangu pengine jimboni mwezi wa tatu hajapita ndio wawakilishi ni sisi na hizo kauli tunatoa, kwamba watu wangu wanaukataa hawataki, hawafanyi hivi na wengine tunawasingizia na kuwasemea. Kwa kweli wanasema kuwa huyu Mhe. Mwakilishi anayetuambia hivyo amekuja lini hapa kwetu.

Kwa hiyo, tatizo jengine ni kumsemea mtu jambo ambalo pengine hata hana habari nalo ndio mwanzo amelikuta Baraza la Wawakilishi siku ile. Mhe. Spika, tabia hii pia kuna siku watakuja kutusuta watu wetu, lakini nafikiri ile ni mkazo pamoja na jazba ionekane kwamba sisi ni Wawakilishi makini tunajadili na watu wetu, wao ndio wanaotupa mawazo. Lakini Mhe. Spika, si wengi wenye tabia kama hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wakati tunajadili ni vizuri kuwa wakweli wa nafsi zetu. Kwa mfano, nimuulize Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hii ni mara ya ngapi kuwa mwakilishi? Ni mara ya tatu. Amechukua kiinua mgongo mara ya ngapi? Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wewe ni mstaafu mwakilishi? Kwa nini ukachukua kiinua mgongo, yaani mshahara wako mara 84.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri juzi kabla ya kuingia kwenye Baraza jengine alipewa shilingi milioni 42, ulipewa kama nani? Mwakilishi Mstaafu, sasa umestaafu, mbona umo tena. Kwa hivyo, kwa nini hatuzungumzi kwamba ili Mwakilishi awe mstaafu. Mhe. Spika, na mimi ni hivyo hivyo nimepokea hizo na Mhe. Spika umepokea kuliko hizo. Je, umestaafu Mhe. Spika?

Kwa kweli Maspika waliostaafu nawakumbuka na mmoja ni marehemu Mwenyezi Mungu amrehemu huko aliko na mwengine yuko hai, ambaye alikuwa ni Spika wa pili wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Ali Khamis Ali na huyo ambaye tunaye hivi sasa ni Spika wa tatu. Kwa hivyo, maspika waliostaafu ambaye huko hai ni mmoja tu. Sasa Mhe. Spika wetu bado hajastaafu na kiinua mgongo ameshachukua mara ngapi? *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunapozungumza jambo hili tufafanue vizuri zaidi. Mhe. Spika, hivi ni kweli kuchukua kiinua mgongo mara tano bado ni mwakilishi mbona hili huliseme kwamba na hili tulitoe.

Kwa kweli maana yake hapa tunawatetea wananchi kuwa hali ni ngumu hospitali pamoja na skuli hazijengwi na serikali inabeba mizigo ambayo hawaiwezi, yaani wanabeba gogo wakati chanja ndogo ndogo hawaziwezi mifano ni hiyo, ili wananchi wetu tuwasaidie, basi kwanza tusioneshe mtu kidole kuwa anauchafu kwenye jicho kumbe jicho lake limeoza. Kutokana na hali hii hatutakuwa tunafanya utaratibu mzuri hata kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kusema kwamba ninachokiona katika mswada huu ni kwamba tunakataa mambo, ambayo tukikubali kukataa na tukikubali kukataa maana yake mswada huu usipite.

Sasa mambo ninayoyaona na wala sisemi kama utapita au hautopita, kwa sababu tunajadili, lakini nasema kwamba mambo ninayoyaona endapo mswada huu usipite ni haya yafuatayo:-

Wawakilishi sisi tutaendelea kupokea *hundred percent* na sio asilimia 80 au ile ambayo tunajadili, kwa sababu hapa tunajadili nini? Rais ataweka *percentage* maalum, sasa hii maalum haitakiwi.

Kwa hiyo, hii inaletwa kwa makusudi kwamba hivi sasa tunapata *hundred percent*, sasa hii maalum maana yake nini? Kwa kweli ni hayo ambayo wenzetu wanasema tufanye kwamba maslahi ya viongozi yasiwe makubwa kiasi ambacho wananchi hawapati hizo huduma, ndio maana yake.

Sasa unapokataa *percentage* X Rais aiweke pale, unataka maana yake hii iliopo iendelee ya *hundred percent* na ikiendelea hii bila ya shaka gharama za mwisho kwa mwakilishi na wengine wote ni kubwa kuliko mswada huu ambao tunaujadili, hiyo ni kihesabu kabisa.

Kwa mfano, Mhe. Rais atasema sikupeni *hundred percent*, sasa kama hakupeni *hundred percent* hatokupeni *two hundred percent* kwa kuzingatia hayo, kwamba hizi fedha nyengine zitumike kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, kama atakupa *less than hundred percent* ndiko tunakokwenda sisi kuwa hizo fedha zitatumika huko.

Mhe. Spika, unaposema kwamba lazima iwe ile ile hakuna X *percent*, ina maana kuwa hicho unachokijadili ni *contradiction*, kwamba fedha nyingi zimepelekwa kwa viongozi na mmoja kati ya viongozi wenyewe ni wewe unayejadili hili. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, ndio nasema kwamba tuwe wakweli wa nafsi zetu, vyenginevyo tunawalisha watu chakula ambacho kina miba, watakila.

Mhe. Spika, naamini kwamba kwa hoja ninazozisikia huko nje ni kwamba kuna upotoshaji mkubwa na amefanya nani sijui, kwa sababu hizo *comments* unazopewa na watu haziko humu. Kwa mfano, Rais mnataka kumpa mshahara mara tatu, hivyo kuna mshahara wa mara tatu uliotajwa na yule wa nje ameipata vipi, kwa kweli kuna upotoshaji mkubwa ambao umefanyika.

Sasa chombo hiki moja kati ya kazi zake kubwa ni kuhakikisha kwamba hawapotoshi, ndio maana tunasema kuwa kila unachosema hapa kiwe ni kweli tena unahakika nacho. Mhe. Spika, mimi sisemi kwamba Baraza au Wajumbe wamepotosha, lakini nasema upo kaitka hizo *comments* pamoja na hao wanaopiga simu, kama vile wale waliosema kuwa wamepigiwa simu mara tano, ni upotoshaji huo na nani amefanya, wanajijua wenyewe. Kwa kweli upotoshaji mkubwa sana umefanyika katika mswada huu.

Mhe. Spika, unaposema kwamba wakati huu mswada urudishwe na uje wakati mwengine, sasa tayari imepo miswada miwili au sheria mbili sasa unarudisha nini. Kwa hivyo, ukirudisha ni kwamba unayataka yale yale yaendelee ambayo

ni gharama zaidi kuliko mswada huu unavyopendekeza, urudishwe na uje lini kusemi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria jana alisema kwa nini mswada huu uje hivi sasa, tena *very clear*, yaani ukiangalia upande mmoja unaona upande mwengine bila ya matatizo yoyote. Kwa nini kipindi hiki mswada huu unaletwa na kwa nini hautoletwa mwaka 2014 au 2015 na alieleza sababu za msingi kabisa.

Kwa kweli hapo ndipo wananchi wanapoona kwamba Baraza na serikali ina busara katika maamuzi yake. Mhe. Spika, hapa tunajenga hoja kiasi ambacho hao wanaotusikiliza wafahamu na kuwa na mvutano au mabishano na kupelekea kuwa na *debate* kubwa baina ya *backbenchers* na serikali ndio kawaida. Lakini mnafika mahala katika kuelimishana kila mtu kutoa hoja zake, yaani mtu anajua kabisa kuwa hoja hizi zina msingi na hizi hazina msingi na wanatusikiliza.

Mhe. Spika, ukitaka kukataa kitu maana wengine sababu yao kubwa ni tu. Kwa mfano, kuna mzee wangu mmoja aliniambia alishikwa sana na mkewe amuache ndio, yaani kila akiingia ndani ya nyumba hamkaliki, utanipa talaka yangu, siku hiyo mzee akaona mm! Hili kero bora lishe, akakaa kitako juu ya meza nusu saa nzima anaandika, yaani aliandika upande mmoja wa karatasi, akageuza upande mwengine, ah! Yule mwanamke akasema anaandika talaka au kombe. *(Makofi)*

Kwa bahati mbaya Mhe. Spika, yule mwanamke hajui kusoma hata a, b, c. Kwa hivyo, yule bwana akachukua barua akaitia kwenye bahasha na kuifunga vizuri, alimuuliza unasemaje, mwanamke akasema unipe talaka yangu siondoni, basi akasema *Bismillah* akampa.

Sasa yule mwanamke furaha akatoka pale mpaka kwao na kusema *Alhamdulillah* unajua tena, alipofika pale akamkabidhi, nini tena mimi nimeshaachwa furaha, kuna mdogo wake wa kike alimuuliza umeachwa vipi? Alimwambia hii takala yangu, ah! Kama talaka mbona hii ni karatasi nyingi, kwa sababu mara nyingi talaka ni karatasi moja tu.

Mhe. Spika, yule ndugu yake alipoisoma kurasa zote tatu limeandikwa neno moja tu, lakini limerejewa zaidi ya mara mia mbili ah! Sasa baada ya kuisoma akamwambia yule dada yake kwamba ndio umeachwa, akamwambia ndio. Kwa kweli ndugu yake akacheka sana na kumwambia hii si talaka kuna neno moja ambalo limeandikwa na wala siwezi kulitaja maana yake ni matusi. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini yule mwanamme anasema huyu sababu yake kubwa anayotaka kuachwa hajaniambia, kwa nini nikuache? Aa! Mimi niache tu, sasa sababu hizo zipo vile vile. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nasema kwamba mswada huu kupita au kutokupita ama hautopita kwa sababu ya tu pia ni sababu. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tumpe nafasi Mhe. Waziri apate kumalizia.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nimalizie lakini hadith imekwisha ambayo ni ya kweli. *(Makofi)*

Sasa kama kuna sababu za msingi na hoja za msingi zimeelezwa hapa na watu wanatusikia, basi watu wataamua nani wana hoja nzito katika hili. Lakini kama sababu ni kukataa tu, yaani ile sababu yenyewe ni ile tu, basi *Bismillah* tufanya nini na vile vile wataamua watu, kwamba ala kumbe siku hizi Baraza sababu yake kubwa nit u.

Mhe. Spika, umeniambia nimalizie hivyo nataka nimalizie kwamba mswada huu mpya tena amesema Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyewizara Maalum) Mhe. Spika wewe umo, Rais wastaafu wamo, Wawakilishi tele, Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais hawamo. Kwa hivyo, jambo jengine ni kwamba ikiwa mswada huu usipopita hawa wawili hawamo.

Sasa kama tunaamua na ndio maana Mhe. Mjumbe mmoja alisema kwamba mswada huu ni wa kibaguzi, hivyo kama tusipoupitisha huo ubaguzi utakuwa mara kumi, yaani tunaufanya wenyewe hapa. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais wasiwemo, ikiwa tunafanya maamuzi hayo sawa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba niunge mkono hoja hii na kuukubali mswada huu mimi mwenyewe binafsi pamoja na ninaowawakilishi watu elfu 22 wa Jimbo la Ole. Nakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu, katika mjadala huu wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ulipaji wa Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam. 4 mwaka 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Nam. 6 mwaka 1999 na Kutunga Sheria Mpya ya Maslahi

na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Baada ya Kustaafu pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, pia nichukue fursa hii kuwapa Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza hili pamoja na wananchi kwa jumla heri ya mwaka mpya, vile vile kumuomba Mwenyezi Mungu atujaalie mwaka huu uwe ni mwaka wenye masikilizano makubwa sana kuliko miaka yote iliyopita.

Kwa kweli tukiwa hivyo Mhe. Spika, ndio tutafanya mambo yetu vizuri na kusema kweli wananchi wetu watafaidika na uongozi wetu. Kwa hivyo, tumuombe Mwenyezi Mungu atujaalie hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimekuwa nikisikiliza mjadala tokea jana michango iliyokuwa ikitolewa na Waheshimiwa Wajumbe ni mingi. Lakini nimelazimika kusimama baada ya hoja iliyoeleza kwamba serikali hii inawafanya wananchi watakuwa masikini na baada ya miaka kumi sijui watakuwaje. Hili limenigusa Mhe. Spika na nimeona ni vizuri nisimame.

Kwa hivyo, ninachotaka kusema Mhe. Spika katika hili na kabla ya kwenda kwenye huo mswada wenyewe ni kwamba katika nchi hii tunayo makundi maarufu matatu ya watu, mawili ni wazalishaji na la tatu nalo ni la uzalishaji lakini linategemea sana haya makundi mawili ya mwanzo.

Kundi la kwanza ni la wakulima, pili ni wafanyakazi na hawa ni wazalishaji na tatu ni wafanyabiashara na hawa pia ni wazalishaji, lakini linawategemea sana wakulima na wafanyakazi.

Mhe. Spika, hivi serikali hii tunayokwenda nayo inawajali watu hawa au haiwajali ndipo pahala ninapotaka tupatizame. Lengo ni kuondoa ile dhana ambayo pengine wananchi huko nje wameshaona kwamba hii serikali iliopo madarakani haitujali hata kidogo kutokana na michango iliyozungumzwa katika Baraza hili.

Mhe. Spika, ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kushughulikia makundi hayo matatu amezitoa wazi katika mikutano mingi tangu amekamata Kiti hiki cha Urais. Kutokana na hali ya uchumi baadhi ya watu waliona hayatatekelezeka yale ambayo Mhe. Rais aliyokuwa akiyasema.

Kwa mfano, kwanza wakulima na Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyewizara Maalum) ameshasema kwamba Mhe. Rais amewajali sana wakulima katika kipindi hiki.

Kwanza amewatembelea kwenye maeneo yao, yaani awaone namna wanavyoishi na jinsi wanavyofanyakazi. Kwa kweli ameamua kuwapatia ruzuku kwenye pembejeo za kilimo na hili amelifanya Mhe. Rais, pia amepunguza bei ya matrekta. Mhe. Rais, amepandisha bei ya karafuu kama walivyosema wenzangu na hayo ni mazao ya wakulima. *(Makofi)*

Vile vile anatilia mkazo yale aliyoyakuta kama vile kupeleka umeme vijijini na kuendelea kufanya hivyo, pia kupeleka maji vijijini na kuendelea kufanya hivyo na huko ndiko kwenye wakulima. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ukiupeleka umeme Matemwe, basi umemuwezesha kweli mwananchi wa Matemwe katika kujenga maisha yake. Kwa mfano, zamani mvuvi wa Matemwe akifika juu magharib amechoka basi lazima samaki atawauza kwa bei ya kutupa au akatafute mibano achome na kulala saa 7 za usiku. *(Makofi)*

Sasa ukimpelekea umeme na kufika nyumbani kwake, maana yake ananunua friji na samaki kuwaweka kwenye friji na bei yako ataikataa na anaweza kukaa nao hata siku nne na wala bei yako haitaki. Kwa hivyo, umemsaidia kujenga maisha yake na serikali hii imefanya hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ukimjengea barabara mwananchi wa kijijini, maana yake umemuwezesha mwananchi yule kufika mjini asubuhi mapema na kuuza bidhaa zake na kurudi tena kule shamba, kwa ajili ya kufanyakazi nyengine kwa lengo la kujenga maisha yake. *(Makofi)*

Kwa hivyo, haya yote waliofanyiwa wananchi, hivi ndio kweli serikali hii imewatupa na inawapeleka kwenye umasikini baada ya miaka kumi. Mhe. Spika, sikubaliani na hoja hiyo. *(Makofi)*

Kuhusu wafanyakazi pia Mhe. Rais ameahidi kwamba atatizama maslahi ya wafanyakazi na ametizama maslahi ya wafanyakazi. Katika Baraza hili muda mrefu tunazungumza juu ya nyongeza za mishahara na inapozungumzwa serikali inatekeleza nyongeza ya mishahara kwa ajili ya wafanyakazi. Na inapandisha hata masuala ya viinua mgongo na pia inalipa penchini kwa wakati. Serikali hii ndio inawadharau wananchi hao katika jitihada hii wanayoifanya.

Wafanyabiashara na wao wameruhusiwa kufanya biashara katika nchi hii. Leo Zanzibar inageuka Dubei ndogo kwa biashara ya magari. Watu wanafanya biashara wanakwenda wakirudi wanaleta magari hapa. Hii ni jitihada ya serikali hii ya kuona kwamba maisha ya wananchi yanakuwa afadhali.

Kilichobakia ni kujituma. Mwananchi mwenye nguvu yake, mzima, haumwi, ajitume, ima awe mkulima au mfanyakazi, iwe ya serikali iwe katika sekta binafsi au ajiajiri mwenyewe. Ndio maana tumeleta hii sera ya wajasiri ambali wadogo wadogo ili na wao wajiajiri. Tumeanzisha mifuko chungumzima ya kuwasaidia hao wananchi katika masuala haya. Mbali ya wafanyakazi waliosaidiwa kupata makopo ili kufanya maisha yao yawe mazuri zaidi. Wafanyakazi wangapi sasa hivi wanamiliki majumba kwa sababu ya mikopo.

Hii ni jitihada inayofanywa na serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wafanyakazi wote wanapata mikopo, mpaka mikopo inawazidi hata mshahara hawawezi kupokea tena. Hizi ni fursa ambazo serikali hii inazitoa. Tena hiyo miaka kumi watakaokuwa masikini iko wapi, katika jitihada zote hizo? Tumekuwa tukizungumza nyongeza za mshahara, tumefanya nyongeza za mshahara pengine inafika mara nne, hata mara moja hatujamuingiza Raisi. Tunajipa siye tu nyongeza za mishahara. Leo tumekaa kitako tunafikiri ah! Na huyu mwenzetu na yeye ni binaadamu tumuongeze kidogo mshahara kama tu navyojiongezea siye kidogo kidogo. Lakini binaadamu huyu kuna siku atastaafu.

Mhe. Spika, na demokrasi ni gharama, bwana, midhali umeamua kutekeleza demokrasi ujue ni lazima utagharimika. Lakini hata hivyo ikaonekana kwamba mwanya usiwe mkubwa. Ndio maana sheria hii tunayoingunga leo inapunguza mianya ya kufanya mtu atakavyo na kumpa nafasi ya yule tunayempa uongozi atizame hali halisi ya uchumi wetu atekeleze vipi. Hili ndio suala tunalolifanya hivi sasa hivi katika Baraza letu hili. Yale mengine wenzangu wameshayataja, yamo katika sheria tuliyoirithi. Lakini ile sheria ilikuwa wazi sana kiasi ambacho leo ile sheria tumeizuia, isiwe wazi kiasi ya vile ilivyokuwa.

Mhe. Spika, Mswada huu badala ya kuwatizama watoto kwa muda wote basi tumeweka miaka maalum ahudumiwe mtoto mpaka miaka hiyo, ikifika miaka hiyo basi, mwenyewe atafute mipango ya kujitegemea. Kwa yule mtoto ambaye mzee wake ameshafariki na ameondoka katika madaraka. Ni kama kumpa kifuta machozi tu ajiwahi kwa miaka mitatu ile ajirekebishe kidogo ili aweze kujitegemea katika maisha. Ndio Mswada huu ulivyosema Mhe. Spika. Hakuna kitu chengine zaidi.

Mhe. Spika, mimi Mswada huu nauunga mkono, na wala siwaungi mkono waliosema kwamba Mswada huu tuuhairishe au tuupeleke mbele, mpaka wapi. Tuahirishe tatizo, huu tusiupeleke mbele na tukijaaliwa uhai na uzima tuupitishe leo au kesho. Huu Mswada umezingatia na umetomwanya kufanya maamuzi kwa mujibu wa tulivyoiyandika hii sheria.

Waziri wa Katiba na Sheria alisema hapa, unapoandika kwamba anaweza kufanya atakavyo isipokuwa kama kuna maagizo mengine, maagizo mengine ndiyo hizi sheria ambayo hatoweza kuvunja sheria, akivunja sheria maana yake anavunja Katiba. Hili ndio tatizo na Rais hatakiwi kuvunja Katiba.

Mhe. Spika, Rais mstaafu, anastaafu. Katika lugha za kawaida Rais anastaafu, lakini katika ukweli wa mambo Rais hastaafu. Raisi ni mtu aliyepata uzoefu, akistaafu kuacha Uraisi wa Zanzibar mataifa mengine wataendelea kumtumia kama Raisi kwa kupata *experience* aliyeipata katika uongozi wake aliofanya kazi. Tunawaona Marais wetu wanaitwa katika foram za Kimataifa, ku- *present paper*s. Wanaitwa katika mikutano mbali mbali kutoa maoni, wanaitwa kufanya shughuli hizo. Hii ndio kazi ya Rais mstaafu anakuwa anaendelea kuifanya. Juzi tu hapa Mhe. Amani Abeid Karume amestaafu, keshakwenda mikutano mingapi na keshatoa *statement* ngapi. Kastaafu lakini bado anaendelea kufanya kazi na bado mataifa yanamtumia kwa *experience* yake aliyonayo kama Rais.

Sasa lazima awe na uwezo wa kuyafanya yale. Atapewa tiketi ya kwenda nchi za nje, ikitokea kuchelewa, asende hio safari. Tatizo hilo, lazima na yeye mwenyewe awe na uwezo wa kwenda kufanya kazi kule. Lakini Rais Mstaafu keshaambiwa kwamba leo bwana tunakwita Nairobi kunamkutano wa Maraisi Wastaafu na wewe umetayarishiwa *paper*. Akaekitako mwenyewe kwenye kompyuta apige hotuba yake. Si, lazima awe na msaidizi wa kumpigia chapa mambo yake yale na kumbuwekea vizuri kumbukumbu zake, si lazima awe nazo. Ndio maana sheria hii ikasema apewe msaidizi. Na kinakuwa kile ni kiyoo cha nchi yenu.

Mhe. Spika, Mwalimu Nyerere hapa alikuwa kiyoo cha nchi yetu kwenda katika nchi mbali mbali. Ndugu Mkapa kawa kiyoo cha nchi yetu kwa kwenda nchi mbali mbali. Mzee Mwinyi ni kiyoo cha nchi yetu anakwenda katika mikutano mbali mbali. Sasa atapiga mwenyewe mambo haya ya hotuba na nini, atakaa kitako bila hata ya msaidizi. Maana ukishakustaafu kumbu kumbu yako inakuwa ina matatizo, lazima uwe na kijana kidogo mwenye umri mzuri akusaidie, kutengeneza halafu wewe kazi yako iwe ni kutizama aah! Hili nililisahau lakini sasa nakumbuka. Mzee Mwinyi anatwambia sikuhizi hata lile jina lake ukimuuliza basi hawezi kukujibu ghafla, kwa sababu keshakuwa mtu mzima. Inabidi angojee kidogo halafu ndio anakwambia eeh! Ali Hassan Mwinyi, kwa sababu ya umri. Sasa Rais huyu ili aendelee kubakia na sifa zake tumuwekee msaidizi. Ndio maana hii sheria imezungumza masuala ya kuweka wasaidizi. Watu wa kumpigia chapa na awe na *full office* aweze kuendesha mambo haya.

Mhe. Spika, Rais akistaafu amestaafu hapa lakini hajastaafu ulimwenguni, bado anaendelea kumwita kama Rais. Ndio maana anapewa jukumu la kupatanisha kama nchi fulani ina ugomvi anaambiwa nenda ukapatanishe, ukazungumze nao huko, anakwenda. Sasa mambo haya atafanya mwenyewe hana msaidizi yeyote, itakuwaje mambo haya.

Mimi naunga mkono Mswada huu ambao unamlinda Rais mstaafu na anakuwa kweli anaendelea kuonesha ile hali ya Uraisi katika dunia ambayo anaishi nayo. Naunga mkono Mhe. Spika, hii hoja. Nategemea wenzangu watalifikiri hili pamoja na yote waliyokwisha kuyazungumza. Mswada huu una umuhimu sio wa kuuahirisha, huu Mswada ni wa kuupitisha ili tuweze kutekeleza hayo, tuwape imag maraisi wetu hawa. Tusiamue maamuzi tukafikiri kwamba tunafanya vizuri.

Mhe. Spika, huko nje kuna watu wanafahamu huko, kuna wasomi wazuri huko wanajua kazi za Maraisi, anapostaafu anafanya nini, watatuona sisi watu wa ajabu kweli kweli hasa, hatutaki kumtunza Rais aliyokwisha kufanya kazi ngumu. Kazi ya Urais ni ngumu sana hivyo! Wenzangu wameshasema hapa sina haja ya kurejea rejea. Na ukishakuupata Urais haukutoki tena mpaka unazikwa, unaondoka kwenye madaraka ya ile nchi tu.
Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii.

Mhe. Waziri wa Biashra, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na miye kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ulipaji Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam. 4 ya 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Nam. 6 ya 1999 na Kutunga Sheria Mpya ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Baada ya Kustaafu pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Mtoni ni Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Hili kofia la uwaziri nimeveshwa leo ni Waziri na kesho naweza kuwa sio waziri. Lakini uwakilishi ni jukumu nimepewa na wananchi wa jimbo la Mtoni kwa muda wa miaka mitano mwaka mmoja umeshapita na imebaki miaka mine. Lakini uwaziri sina uhakika kama nitafika hata siku tatu kuwa waziri tena.

Kwa vyovyote vile mimi napenda kuona haki za wananchi walionipigia kura na haki za Wazanzibari wote zinathaminiwa na zinalindwa. Wala siwezi kuona kwamba kuna baadhi ya watu au wenzetu wanajaribu kupotosha kwa makusudi ili kwa kuwepoteza lengo wananchi. Mimi ningeomba kila kitu kiwe *black and white*, hakuna kufichana hakuna kustahiyana, tunzungumze ule ukweli ulivyo.

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi, anaposimama akaanza kuwapotosha wananchi mimi hili kubaliani nalo na hii ndio hoja yangu nzito nitakayoizungumza hii leo. Tunapowapotosha wananchi kwa makusudi tunajaribu kuzua jambo ambalokwamba hatujui huko mbele litaleta taathira gani.

Kwa mfano watu wengi wamesimama hapa wamesema kwamba bei ya mchele kilo moja Sh. 1,600/-, Mimi nasema si kweli, data hiyo si kweli na sasa nakupeni data sahihi. Katika nchi yetu kuna mchele aina nne, mchele wa basmati ndio mchele ghali wao hapa kwa jumla kigunia ni laki moja na nusu mpaka laki moja sabini na tano elfu na kwa reja reja reja ni Sh. 4,000/- kwa kilo, mchele wa aina ya jamii wa *supper falcon*, *white rose* na *red rose,* bei yake ni Sh. 53,600/-kwa kigunua mpaka Sh. 56,000/-, bei ya reja reja ni Sh. 1,200/-, mchele wa aina ya *supper* kiyelar unaotoka Tanzania Bara unauzwa gunia moja lenye kilo 100 Shilingi laki na sitini elfu mpaka laki moja na thamanini elfu. Reja reja umeanzia Shs. 1,600/- mpaka Sh. 2,000/-.

Bei zote za unga, mchele, sukari, ukipanda, ukishuka, mimi naelewa. Sasa anasimama mtu hapa akazungumza kwa jazba kwamba mchele wa hali ya chini kabisa kwamba bei yake ni 1,600/- kaipata wapi, bei tunayoijua ni Sh. 1,200 kwa kilo na sio 1,600. Kwa hivyo huu ni upotoshaji wa makusudi.

Mwakilishi anasema kwamba wananchi wanakopwa huko karafuu zao. Nani kakopwa hapa? Serikali imetumia jumla ya shilingi bilioni 61 mpaka jana, zote zimeingia katika mikono ya wananchi wakulima Pemba. Unguja hapa tumetumia bilioni 4 tu lakini Pemba tumelipa bilioni 61. Ukenda Benki ya Pemba hakuna hata bilioni 3, bilioni 2 hakuna, zote hujui zimekwenda wapi, kila mtu pesa zake kaziweka mkononi au pengine kapelekea Dar-es.Salaam. Uchumi hauendi hivyo. Uchumi unakwenda ikiwa wananchi Pesa watazitia Benki kwa hivyo ule uchumi utapata kuzunguka. Lakini uchumi umeganda. Kila siku ukitaka pesa Pemba ukodi chata hapa upeleke pesa Pemba za kwenda kununulia karafuu.

Mhe. Spika, inapotokezea katika kinu cha karafuu sasa hivi saa 10:00 jioni au saa 9:00 mchana amakuja mtu kauza karafuu zake ukamwambia kwa usala wako na usalama wetu sisi, njoo kesho uchukue pesa zako. Mkulima anakubali, hana matatizo yoyotea kwa sababu anajua kwa mudawa miezi mitano kalipwa keshi, imetokezea matatizo ya muda mfupi anakubali anakuja kesho anachukua fedha yake. Mpaka sasa hivi ninavyozungumza hapa hapana mtu hata mmoja anayeidai ZSTC, watu wato wameshalipwa.

Serikali imejidhatiti bei ya karafuu ilipanda, tukapandisha bei ya karafuu. Bei ya karafuu imeshuka mpaka chini sisi bei hatukuteremsha. Tumefunga mkanda

tumenunua karafuu kwa bei ile ile, wakati bei ya kuuzia karafuu imeshuka chini kabisa. Kila mtu alikuwa taabani hapa, sote taabani kwa sababu bei ya karafuu ni chini na bei tunayowalipa wananchi ni kubwa na ndio maana mtu yoyote hapeleke karafuu Mombasa kwa sababu karafuu Mombasa haitakiwi. Karafuu Mombasa walikuwa wakinunua kilo moja Sh. 1,200/ ya Kenya wakafika kununua bei ya Sh. 700/- nani atapeleka wakati sisi tunanunua zaidi Sh. 1,200/-, tunanunua Sh.15,000/- kwa kilo.

Leo mtu anasimama hapa anaupotoa umma anawambia kwamba watu wakopwa. Nani akopwae, tumelipa *cash 61 billions* unasema watu wanakopwa. Wanaokopwa sisi tunawajua, wanakwenda kuuza bidhaa zao msimu huu unakaa katika maghala wanapewa stakbadhi mpaka msimu mwengine unakuja pesa zao bado hawajalipwa. Kwa hivyo jamani tusipotoe wananchi. Mtu kwa makusudi na anajua kila kitu lakini anasema Afisi ya Faragha ya Mhe. Rais inatumia shilingi bilioni 1.6. ina maana hizo ndizo anazoondoka nazo Rais akistaafu. Hakuna asiyejua kwamba Afisi ya Faragha ni kitu mbali na maposho na mshahara wa Rais ni kitu mbali. Lakini ni upotoshaji wa makusudi. Wananchi hawa wana akili timamu na wala hawakubali kupotoshwa.

Mhe. Spika, wananchi wangu wa jimbo la Mtoni mimi wamenifata wakaniuliza kuna nini Baraza la Wawakilishi mbona kuna ugomvi. Mimi sikuwaficha kwamba ugomvi uliokuwepo pale Wawakilishi kwa mujibu wa sheria ya nyuma, sheria kongwe ya 1988 na 1999, mwakilishi akitoka pale inabidi alipwe mafao yake kwa asilimia 100. Sasa hivi Rais kaa kitaka akaangalia hali ya uchumi kama nzuri atawapa asilimia100, kama mbaya atawapa asilimia 70, posho zao Wawakilishi wakistaafu zitapungua. Ndio ogomvi huu uliokuwepo.

Mhe. Spika, kwa mshahara uliowekwa na kwa fomula hii Mwakilishi ataondoka hapa na milioni 66 hataki zipungue anataka zile zile milioni 66 hataki alipwe milioni 50. Tena huyo ndiyo anasema anawahurumia wananchi, wananchi watafilisika, serikali haina imani na wananchi kwa sababu gani? Anataka apate milioni 66 sio chini ya hapo.
Wananchi wangu wa mtoni nimeshawambia kwamba msihadaike, wanacholilia posho yao isipungue. Mswada huu utawapunguzia Wawakilishi posho yao inawezekana ikawa isiwe 100% ikawa ni 50% pengine wakaondoka na milioni 50 au 45 au 30. Huo ndio ugomvi uliopo. Kwa hivyo Wawakilishi wasikubabaisheni bwana wanaangalia mslahi yao na sio maslahi ya wananchi. Huu ndio ukweli niliowaambia wananchi wa Mtoni. Mimi mmenipigia kura siwafichi kitu. Wawakilishi wanapigania posho zao, hawapiganii nyinyi, kabisa kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Rais ambaye amestaafu, ameondoka madarakani, kaondoka na kiinua mgongo cha shilingi milioni 10, lakini mwakilishi hapa kaondoka na kiinua mgongo cha shilingi milioni 42. Rais wa awamu ya 6 kaondoka katika cheo kile kiinua. Ndio huo ndio ukweli.

Mhe. Spika, tofauti ya posho na mshahara wa Raisi mzima wa Zanzibar, na Mwakilishi ni shilingi milioni moja. Kweli Rais ambaye tumempa mamlaka na dhamana kubwa ya nchi hii tofauti yake yeye na mwakilishi iwe ni shilingi milioni moja tu. Lakini kwa sababu hali yetu ya uchumi ni ndogo ndio maana Rais anapokea kima hicho. Leo sisi wa kukaa tukapiga kelele hapa. Rais kapewa majukumu makubwa sana, majukumu ambayo kwamba ni ya dunia na ya Akhera. Madhambi yote tu nayofanya sisi hapa atakwenda kujibu Rais. Na keshokutwa akenda akhera kule siku ya kiyama anahojiwa kila alilofanya mwananchi katika nchi hii. Ana dhamana kubwa sana kwa Mwenyezi Mungu na kwetu sisi. Tunalia lia nini? Nani hajui? Nyote mnajua kwamba Rais mshahara anaopata ni mdogo sana.

Mhe. Spika, mimi nilikutana na rafiki yangu mmoja anafanya kazi TRA akanambia Mheshimiwa haijambo umekuwa Waziri sasa hivi mambo mazuri, mambo gani. Nikamwambia kwani huo mshahara wangu mimi kukwambia naona haya. Akanambia nambie tu. Nilivyomwambia, akanambia yeye anapata mara tatu yake kuliko miye. Mfanyakazi wa TRA tu huyo. Lakini tumekuja hapa kuja kujituma kwa ajili ya kujenga nchi yetu, sio kuja kuchukua maposho wala kuja kuchukua mishahara. Tumekuja hapa kuja kuwatumikia wananchi.

Tena nataka niwambie wananchi wenzangu pamoja na wananchi wote kwamba sisi tunatunga sheria hii kwa kuthamini michango ya viongozi wetu wa siasa. Mchango wa Spika wetu tunaujua, mchango wa Makamo wa Kwanza tunaujua, Makamo wa Pili tunaujua, mchango wa Rais unajulikana wazi wazi, ni mchango mkubwa. Na Maraisi wastaafu kwa nchi za Nje huko ni rasilimali ya nchi. Huwezi kuwaacha hivi hivi tu wakababaika. Huwazi kuwa na utawala bora katika nchi ikiwa Rais anadharauliwa, Rais hashughulikiwi na hawajui mustakbali wake. Halafu tunanung'unika ooh! Kunauzwa hiki, kinauzwa hiki, kinauzwa kile. Sisi hatutaki mambo hayo. Hatutaki mtu yeyote au kiongozi yoyote kuanza kuingizwa katika shutuma.

Kwa hivyo kiongozi ajue mimi ninapoacha kazi hapa nina mstakbali gani mbele yake, asije mtu akambabaisha babaisha. Kwa hivyo nasema kabisa kwamba suala la waraka huu hakuna suala la kumnyima mwananchi haki yake wala kumdhulumu mwananchi, bali ni upotoshwaji wa makusudi ambayo wananchi wanapotoshwa, waone kama Serikali yao haiwajali. Serikali inawajali sana wananchi wetu na tunawajali sana maana tumeacha kazi zote

tunafanya kazi hii kwa ajili ya kujenga mustakabali mzuri wan chi yetu na kujenga maslahi ya wananchi wetu.

Ndugu zangu Wawakilishi, tuwacheni jazba, tuwacheni kuwapotosha wananchi, tusijifikirie sisi zaidi, tuwafikirie wananchi. Kama kweli tuna nia ya dhati ya kuwasaidia wananchi wa nchi hii basi Mswada huu tuupitishe. Mishahara yetu imeongezwa, hatukusema sisi kwamba jamani wananchi wataumia huku sisi msituongezee. Tumenyamaza kimya, hapana asemaye. Mshahara ulikuwa laki tano hapa sasa hivi umekuwa lakini nane hajasema mtu bwana msituongezee mshahara sisi, kwa sababu wananchi tutawadhulumu huko. Aaah! kimya kila mtu kaubana anatia mfukoni.

Tumeamua kwa dhati kabisa tunaongeza mishahara ya watu wote kwama tulivyosema sisi hapa. Wanasema Wawakilishi kwamba watu hawajaongezwa mishahara. Watu mishahara wameongezwa bwana. Hili leo unakaa hapa na hansard inaandika kwamba wewe unasema kwamba watu mishahara hawajaongezwa. Wakati watu mishahara wameongezwa kwa mujibu tulivyozungumza hapa. Wananchi wote mishahara wameongezwa kuanzia mwezi wa Oktoba. Lakini wawakilishi hapa wanataka walipwe *area* tangu za Julai. Hawasemi wao kwamba wananchi hawa sisi tunawapenda kwa. hivyo wao wameanza kuongezwa mishahara mwezi wa Oktoba na sisi tuongezwe mwezi wa Oktoba, wanasema hapana, sisi tunataka kuongezwa kuanzia mwezi wa Julai kwa sababu ndio mwisho hapa.

Mhe. Spika, nimewaahidi wananchi wa Mtoni nitakwambieni ukweli, ukweli lazima usemwe hapana kufichwa kitu hapa. Kwamba sakata hili la mswada huu baina ya wawakilishi wetu ni mafao ya wawakilishi basi, na ushahidi yuko mwakilishi mmoja alisimama hapa mwisho akasema kama mafao yetu sisi hayajatizamwa hapa basi sipitishi mimi mswada huu. Mhe. Spika, huu ndio ushahidi dhahiri kwamba sisi wawakilishi tumekuwa wabinafsi tunajaribu kuwadanganya wananchi, wananchi tusiwadanganye wananchi hawa hii ni Serikali yao ya Kitaifa inataka iwajenge maisha yao yawe mazuri na uchumi wao uwe mzuri tusing'ang'anie maposho hayatupeleki pahala. Mhe. Spika, sisi wengine tumeacha kazi huko zina tija zaidi tumekuja katika siasa kuja kusaidia nchi yetu sio kuja kutafuta maposho hapa. Kwa hivyo, naomba tushirikiane kwa pamoja ili tuweze kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni naunga mkono hoja ya mswada huu na naomba wawakilishi wote mtafakari mumuogope Mwenyezi Mungu muupitishe mswada huu ili wananchi wetu wapate manufaa, na wale viongozi wetu ambao kwamba ndio

wenye usukani wapate manufaa ambayo yatakuja kuijenga nchi hii. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Uvuvi na Mifugo: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuchangia katika mswada huu muhimu ambao nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi jana kwa kuuleta kwa ufasaha sana. Mhe. Spika, mara moja Mhe. Haji Faki Shaali alisema hapa kwamba mtu akishapiga zumari basi ukipiga kiperenge huwa watu hawakuelewi vizuri. Maana yake ni kwamba michango iliyoanza kutoka kabla nikiri kwamba ni mizito sana.

Mhe. Spika, mimi kwanza naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao tangu jana, mimi niwapongeze na nimejifunza sana.

Mhe. Spika: Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tumsikilize Mhe. Waziri kama na sisi walivyokuwa wanatusikiliza sisi. Waheshimiwa Wajumbe nimeletewa taarifa na mafundi wetu wa mitambo wananiambia kwamba tukipiga sana makofi basi mitambo yetu inaweza ikafeli, kwa sababu *load* inakuwa ni kubwa sana ya sauti kiasi cha kwamba mitambo hii inaweza isifanye kazi. Mafundi wanasema kwa heshima zote naomba uwaambie Waheshimiwa Wajumbe wapunguze kupiga sana meza kwani *microphone* zitaharibika. Kwa hivyo, nimekuwa naendelea kuhimiza Waheshimiwa Wajumbe tupige makofi kwa nidhamu ili tudumishe meza hizi pamoja na *microphone* zetu, nawashukuru sana.

Mhe. Waziri wa Uvuvi na Mifugo: Mhe. Spika, nilikuwa nikisema kwamba mfumo huu wa Serikali ya Umoja ya Kitaifa kwa kweli umetusaidia sana kuongeza demokrasia katika Baraza la Wawakilishi. Nilikuwa namkumbuka swahibu yangu Mhe. Ali Mzee Ali wakati alipokuwa mbele katika suala hili alitabiri kwamba ule wasi wasi waliokuwa nao baadhi ya watu kwamba mfumo huu ungeweza kuvidha demokrasia ya Baraza watakuja jua huko mbele. Kwa kweli ni hakika kwamba demokrasia katika Baraza kiwango chake kimepanda sana.

Mhe. Spika, ni vizuri demokrasia ambayo tumeipata tukaitumia vizuri, tukaitumia kwa kutoa michango ambayo itawaelimisha zaidi wananchi sasa mimi michango ya Waheshimiwa Wawakilishi wengi nilipoisikiliza hata kama ni mimi kama nisingepata nafasi ya kuipitia miswada ambayo ilipitishwa kabla, basi ningelikuwa na mtazamo ambao wao wanao leo.

Mhe. Spika, mimi nilijituma kidogo mswada huu chanzo chake ni mwaka 1988 Mzee wetu Marehemu Idrissa Abul-wakil ndio mwanzo ambaye *Act to provide*

*for the granting retirement benefit to be society to specify state leaders upon chairman from specified State Office and other matters connected therewith n*diye wa mwanzo niliyeipata. Mwaka 1999 Mzee wetu mwengine Dokta Salmin Amour Juma akafanya marekebisho ya sheria ile, Mzee wetu mwengine mwaka 2003 Dokta Amani Abeid Karume naye akafanya marekebisho ambayo yalifanya awali.

Mhe. Spika, mswada huu ambao Dk. Mwinyihaji ambaye aliuwasilisha jana nao unafanywa marekebisho ambayo yalifanywa mwaka 2003. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nayazungumza haya kwa sababu yakupata nafasi yakuelimishana na Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu katika suala ambalo liko katika meza yetu, awamu kwa awamu imekuwa ikifanya marekebisho kulingana na mazingira yake. Mimi naunga mkono marekebisho haya kwa sababu mbili. Kwanza kuna umuhimu wa kufanya marekebisho baada ya mabadiliko ya viongozi wakubwa wa kisiasa katika Katiba yetu. Sheria hii ya mwaka 2003 inatambua viongozi wakuu wa kisiasa kama ni Rais wa Zanzibar na Waziri Kiongozi, Katiba tuliyoipitisha mwaka 2010 inafuta Waziri Kiongozi inaweka Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais badala yake.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa maana hiyo lazima mabadiliko katika sheria yaje kwa sababu lolote litakalotokea hapo mbele ni kwamba Waziri Kiongozi hatunae tena, tuna Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais. Kwa hivyo, lazima mabadiliko haya yaje.

Mhe. Spika, sababu ya pili ni kwamba tumeamua serikalini kuwa tujitahidi kila mwaka mishahara ya watumishi ipande ikiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hayo ndio maamuzi ya serikali. Kwa hivyo, kwa maamuzi hayo mshahara wa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi utakuwa ukipanda mwaka hadi mwaka. Mhe. Spika, sababu hizo ni muhimu kufanya marekebisho ili kwenda sambamba na hali itakayokuwa hapo baadae.

Mhe. Spika, nilipojaribu kusoma yale ambayo yalielezwa mwaka 2003 na yale ambayo yameelezwa katika mswada huu, nikiangalia yale ambayo amewekewa Mhe. Rais Mstaafu *pension granted monthly over equal to eight percent of monthly salary of* ***incur bent*** *president* na humu ndimo munamozungumza kwa hivyo hapa hakuna marekebisho baina ya sheria ile na hii ambayo imefanywa. Kuna *housing accomodation of fifty percent* katika sheria ya mwaka 2003 na sheria hii ambayo tumebadilisha. *Free medical care* kwa mwaka 2003 na hii ya mwaka 2012, na ofisi ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wengi bahati mbaya wameizungumza iko katika sheria ya 2003 iko na katika sheria ya 2012.

Mhe. Spika, sasa Mhe. Mwakilishi akisema mutampaje Rais mshahara marupurupu ya asilimia 80? Mhe. Spika, haya si matakwa ya marekebisho ya hivi sasa hii ndio sheria ambayo ipo, nakusudia kusema nini? Nakusudia kusema kwamba hata kama wawakilishi hawatapitisha huu mswada basi bado Dk. Shein atakapostaafu atapata marupurupu yale yale ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wameyakataa leo, hiyo itakuwa haijawasaidia kabisa. Kwa sababu marupurupu haya yamo katika sheria ya mwaka 2003 kwa hiyo hata kama tutaikataa hii bado atakapostaafu atalipwa haya haya ambayo leo yamekataliwa. Mhe. Spika, atakayeathirika hasa ni watu wawili, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Kwa sababu katika sheria ya mwaka 2003 haitambui Makamo wa Kwanza Rais na Makamo wa Pili wa Rais, inatambua Waziri Kiongozi na hivi sasa hayupo. Kwa hivyo, hao ndio watakaoathirika kwa kuukataa huu mswada.

Mhe. Spika, hili ni jambo la msingi kulifahamu na mimi nasema kwa maana hiyo ningewaomba na kuwasihi sana wenzangu kwa heshima kubwa mimi ni mwenzao sana, mimi ni *backbencher* wa siku nyingi wanaelewa. Katika hili naomba waupitishe mswada huu kwa muhtadha wa kumuwekea mazingira mazuri Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Spika, sababu yake ni kwamba sote hapa tunaelewa hasa sisi tunaotoka katika Chama cha CUF Maalim Seif alipoacha Uwaziri Kiongozi alipanga nyumba ya vyumba viwili Mtoni. Mtu amefikia pahali yakuwa Waziri Kiongozi akapanga katika nyumba sijui ya Shirika la Umeme ina vyumba viwili, kwa kweli ni mtihani mkubwa. Mara moja pale mimi nilikwenda kumuamkia akaja mgeni kutoka nje basi ilikuwa ni aibu pakumuweka hana. Mhe. Spika, marekebisho haya yanalenga kusema anapostaafu huyu mwenzetu angalau apate pahali kidogo palipo chuchuka, basi hili mheshimiwa nalo ndio linawaumiza wananchi kiasi hicho.

Mhe. Spika, hili mimi ningewaomba wenzangu waliangalie sana na viongozi wetu hawa Mhe. Rais wa Zanzibar, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais kwa kweli Mhe. Spika, mimi nawaheshimu sana kwa sababu si watu ambao wanajivutia makubwa hata kidogo. Namuelewa Maalim Seif alivyo namna maisha yake yalivyokuwa na alivyo hadi leo, yeye si mtu wa makubwa hivyo tusipomfikiria sisi itakuwa mtihani. Mhe. Makamo wa Pili pia tunamjua alivyo maisha yake, hivyo tusipomfikiria kesho kutwa hali itakuwa mbaya. Mhe. Spika, Dk. Shein amekuwa Makamo wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka 9 alipoombwa kuja Zanzibar kuwatumikia Wazanzibari wenzake marupurupu yaliyoko katika nafasi ile na ambayo tunampa leo sisi hayafiki hata nusu. Mhe. Spika, mshahara wa Rais wa Zanzibar na marupurupu yake ukilinganisha na ule wa Makamo wa Rais wa Jamhuri haya hayafiki hata nusu, yeye analijua hilo lakini alisema nirudi

nyumbani wenzangu wananihitaji. Mhe. Spika, mtu kama huyo lazima tuangalie namna ya kumuenzi kwa mujibu wa Katiba.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ni muhimu tuliangalie ni lile ambalo nimesema kabla kwamba sisi haitowezekana kuwa wafanyakazi wa umma wa serikali waongezwe mishahara sisi tufunge mikono. Wawakilishi tutasema hapana tuongezeni, sasa tutafika pahala kwa asilimia ya mia moja ya marupurupu ya *formula* ilivyo sasa serikali itakuja shindwa kutulipa na huko nyuma ishatokea hii. Mhe. Spika, kuna wakati nakumbuka mwaka 2000 kipindi cha uwakilishi kimemaliza tunataka marupurupu hakuna hata senti moja, tunakwenda pale unapewa shilingi mia mbili, unafika unasema hali mbaya unapewa mia tano, unakwenda kidogo unapewa elfu moja. Hiyo ni kwa sababu serikali ilifika pahali ikawa haina uwezo wa kulipa marupurupu ya wanaostahiki.
Kwa hivyo, kuzuia hilo mheshimiwa tukubaliane suala hili la asilimia maalum ya marupurupu yetu sisi wawakilishi tuipitishe katika sheria. Mhe. Spika, hii imefanywa makusudi kuangalia hali ya uchumi itakavyokuwa hapo baadae, kama hali ni nzuri naamini sana Mhe. Rais akishauriwa na Makamo wa Pili, akishauriwa na Spika wetu kama uchumi ni mzuri basi watatupa japo asilimia mia mbili. Lakini kama hali ni mbaya mheshimiwa lazima mazingatio yafanywe ama tulipwe asilimia 25, asilimia 50, asilimia 70, asilimia 80 kulingana na hali ya uchumi wa nchi utakavyokuwa, na hivyo ndio namna bora ambavyo serikali inawajali wananchi wake.

Mhe. Spika, kwa hayo machache mimi ni mwakilishi kama wawakilishi wengine nina wananchi nawakilisha hapa katika Baraza maslahi yao na hali yao inaniuma kama wanavyoniuma wengine, basi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando naunga mkono mswada huu moja kwa moja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, awali ya yote niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha jioni hii ya leo na mimi kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa miongoni mwa wawakilishi wa wananchi waliochaguliwa na nina imani Mwenyezi Mungu ataniongoza kuendelea kuwaongoza vyema katika kipindi cha miaka 4 iliyobakia, na wenzangu wote walioingia kwa njia zote zile Mwenyezi Mungu awaongeze waweze kuwaongoza vyema wananchi wao. Mhe. Spika, waislamu tunahimizwa kuombeana neema na sio kutakiana mabaya, Mwenyezi Mungu asinijaalia kuwa watu wanaopenda kuwaombea mabaya wenzao. Mhe. Spika, ukipigiwa makofi maana yake unasema vizuri, ahsanteni sana kwa kunipigia makofi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, na mimi nataka niwe mkweli katika kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ulipaji Mafao ya Viongozi Wastaafu Nam.4 ya mwaka 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Nam.6 ya mwaka 1999 na kutunga Sheria mpya ya Maslahi ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa baada ya kustaafu pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwa taratibu zetu za kikanuni yale ambayo wenzangu wameshayazungumza nadhani kwa sababu ya kuokoa muda nitajaribu sana nisiyazungumze. Lakini sote tumeingia hapa kwa nia ya kuja kuwawakilisha wananchi, wale ambao tumetokea majimboni, wale ambao wameingia kwa nafasi zao na wale ambao wameingia kwa kuteuliwa na Mhe. Rais, sote nia yetu ni moja.

Mhe. Spika, nataka niseme vile vile si vizuri kuleta tuhuma nzito ndani ya chombo hiki, lakini vile vile tukiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa sehemu moja serikali humu ndani na sehemu ya pili ni *backbencher*s sisi sote tunatakiwa tuzungumze mambo kwa maslahi ya wananchi wetu na sio kuwapotosha wananchi wetu. Mimi tokea jana nilikuwa nikishuhudia kusikia kwamba watu wanatishwa, lakini mimi kama serikali ni wajibu wangu kuhakikisha agenda ambayo imewasilishwa Barazani na serikali kuwa inapita. Vile vile ni haki yangu kumtafuta Mhe. Jussa nikamfahamisha, nikafanya *lobbing* aikubali sheria iliyopo si makosa kwa ustaarabu wa Mabunge ya kidunia. Mhe. Spika, Mhe. Jussa akinikubalia atafuata ushauri wangu asiponikubalia atafanya maamuzi kwa mujibu anavyoona yeye ni haki yake ya kisheria kabisa ya kikanuni na ya kikatiba.

Mhe. Spika, lakini tukijenga mazingira kwamba tukija na *issue* kama hii ya sheria ya serikali mimi niogope kuzungumza na Mhe. Jussa nadhani hiyo haijengi mazingira mazuri yakuwakilisha wananchi. Lakini mimi kufanya *lobbing* kwa Mhe. Jussa, samahani natoa mfano kwako sana si ruhusa, lakini mtu mwengine akionekana kasimama na mimi anaambiwa tushakujua ushachukuliwa na mawaziri, utakiona. Kwa hivyo, nani anatisha kati ya hao watu wawili. Mimi nadhani utaratibu wa kawaida katika mabunge serikali kufanya *lobbing* kwa *backbencher* ni jambo la kawaida na *backbencher* vile vile kufanya *lobbing* kwa serikali ni jambo la kawaida. Kwa uzoefu wangu Mhe. Spika, wa kipindi cha nne kuingia hapa hivyo ndivyo mabunge yanavyofanya kazi.

Mimi nilipokuwa *chief weep* nilikuwa nikifanya hiyo kazi, sasa mwenye uwezo wa kutisha ni *weep* kwa upande wa Chama cha Mapinduzi humu yumo Mhe. Salmin Awadh Salmin na kwa upande wa chama cha *CUF* yuko Mhe. Rashid Seif Suleiman. Hao wakibeba bakora za vyama vyao wanaweza wakatisha,

ndio utaratibu, kwa hivyo mimi nadhani zile tuhuma mimi nadhani wenzangu kidogo sijui niseme nini, lakini nataka niseme utaratibu wa kufanya *lobbing* serikali kwa *backbencher* na *backbencher* kwa serikali ni utaratibu wa kawaida katika mabunge na sio kioja hata kidogo.

Lakini ikiwa mimi kwa sababu ni serikali nisinong'one sasa na Mhe. Ali Salum Haji mimi nadhani tutakuwa tunaonesha picha gain kwa wananchi wetu. Huo ulikuwa ni utangulizi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, yamezungumzwa mambo mengi likiwemo suala la washauri maalum wa rais kuwa ni wana siasa au si wanasiasa, washauri wa rais ni wanasiasa kwa sababu washauri maalum wa rais sio wasaidizi wa rais. Katibua wa rais ni msaidizi wa rais, mwandishi wa habari wa rais ni msaidizi wa rais na wengi wengineo, mshauri maalum tofauti na mshauri mkuu wa rais ndio maana katiba hii inatambua kuwepo kwa washauri wakuu wawili wa rais, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Hawa ni washauri wakuu hakuwapa sekta maalum ya kumshauri, washauri maalum anawapa sekta maalum kama mshauri wa rais masuala ya kimataifa na uwekezaji amewapa maeneo maalum na kama walivyokwishasema wenzangu kwenye kikao cha asubuhi kwamba rais leo akiondoka na wao wanahama Ikulu, lakini watumishi, wasaidizi wa rais, rais anayekuja anawakuta wanampokea, sasa akipenda kuwabakisha anawabakisha asipopenda atawaondosha. Kwa hiyo hii ndio maana washauri maalum wa rais na wasaidizi wa rais.

Mhe. Spika, imesemwa huku katika Katiba ya Zanzibar ukurasa wa 41 kifungu cha 58 (1) (2) kinafafanua, Waheshimiwa sina haja ya kupoteza muda tulipoapa tulipewa katiba na kanuni bila shaka tunajisomea na tutakuwa tunaelewa. Haya tukisema kuna watu wanaonesha nini hii, sawa lakini lazima tuseme hatuna pahala pengine pa kusema isipokuwa hapa.

Mhe. Spika, eneo langu la pili ninalotaka kulizungumza humu kuna kifungu ambacho kinapendekeza kumpa mamlaka Mhe. Rais kupendekeza *percentage* kwa kushauriana na Makamo wa Pili wa Rais na Mhe. Spika. Watu wanakuwa na hofu wanasema tutamuaminije mtu mmoja, lakini tunasahau kwamba huyu mtu tumempa nchi, huyu ni kiongozi wa hata hiyo mihimili yote inaendeshwa chini ya usimamizi wake ndiye kiongozi wa nchi.

Lakini jengine tunasahau kwamba Baraza hili la Wawakilishi lina sehemu mbili kwa mujibu wa kifungu cha katiba cha 63(1) Baraza lina sehemu mmbili, sehemu moja ni sisi tuliomo ndani na sehemu ya pili ni Mhe. Rais kwa maana

haya yote ambayo tunayaamua sisi hapa lazima na yeye akayape mkono wake. Sasa na huu ni utaratibu wa kuwaongoza wanadamu ulivyowekwa na wataalamu wa kiutawala na kutunga sheria duniani.

Sasa na mimi naogopa Mhe. Spika, kwamba tunapofika sasa sehemu hizi mbili za Baraza tukafikia pahala tukashindana sisi watunga sheria tukasema hatufanyi Mwenyezi Mungu asimjaalie kwa mfano Mhe. Rais na yeye akasema waliyoniletea sifanyi tunaipeleka wapi nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi nikiwa mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Tumbatu naogopa sana hilo, naogopa. Kwa sababu kila mmoja atakuwa kashika mpini tukifikia hapo nadhani itakuwa hakuna salama matokeo yake tutafika katika hali isiyokuwa ya kawaida.

Mhe. Spika, limezungumziwa suala la hali ya uchumi kuwa uchumi wetu mdogo kwa nini tunafanya hivi, mimi sijui usemi mzuri wa yule mamba unajua natoka mbali natoka Tumbatu, sijui anasema msemo wa Kiswahili kwamba, “Mamba akiamua kumla mtu huku anatokwa na machozi’, huruma za mamba mimi sijui.

Mhe. Spika, hali ya uchumi ni kweli na tulipokuwa tukipitisha bajeti kuu ya serikali tulisema sote hapa tulipenda au tungependa kila kitu kifanikiwe kwa asilimia 100, lakini hali ya uchumi ni sahihi ndio maana serikali hata ilipoamua kupandisha maslahi ya wafanyakazi tuliamua kupandisha kwa mujibu wa hali yetu. Kigezo cha kwanza cha kupandisha mshahara watumishi wa umma na watumishi wa kisiasa ni kuzingatia hali ya uchumi wa nchi ulivyo, serikali hilo tunalijua na Wajumbe hawa wa Baraza la Wawakilishi wanalijua.

Sasa mimi nadhani wanaojua hesabu au wataalamu wa hesabu unaposema asilimia 80 unataka ufanye shughuli zako kwa asilimia 80 yaani unataka mtu umlipe mafao yake kwa asilimia 80 na mwengine umlipe kwa asilimia 100, wale wataalamu wa hesabu kina Maalim Haroun kubwa ni ipi? Hiyo ya thamanini itakuwa ya pocho, mtu aliyekuwa hajui ndio atasema asilimia 80. Lakini Mhe. Rashid Seif nina imani anaelewa kati ya asilimia 100 na asilimia 80 ipi kubwa.

Mhe. Spika, juzi tulikuwa na *briefing* aliyoyasema Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko mpaka tukakutuma wewe wende ukaonane na Mhe. Rais kwenda kuomba *area* hizo ni huruma za mamba. Serikali kutokana na hali ya kutaka usawa wa wananchi wetu tulisema tuna uwezo wa kulipa mshahara kuanzia Oktoba, Wawakilishi sisi tukasema tulipwe kuanzia Julai, hivyo kweli tunawapenda wananchi wetu? Ugomvi Mhe. Spika, ni kweli inaonekana kuna

tag of war kati ya serikali na *backbencher*, ugomvi uko hapa kwamba sisi tunataka tulipwe *hundred percent* wawakilishi serikali tunasema uwezo hatuna kwa kuwaonea huruma wananchi.

Mhe. Spika, kwa mshahara tunaolipwa sasa Waheshimiwa Wawakilishi serikali inaseama haiwezekani kulipa *hundred percent*. Wananchi na wapiga kura wetu waelewe hilo, naunga mkono wale wote waliotaja marekebisho ya sheria ya mwaka 1988 ambayo marekebisho yalifanywa toka kipindi cha Dr. Salmin Amour Juma (*commando*), yakaja yakafanywa na Mhe. Amani Abeid Karume.

Lakini Mhe. Spika, haya ambayo Mhe. Karume aliyafanya mwaka 2010 inatokana na yale yale masuala ya mashauriano kati ya muhimili mmoja na muhimili mwengine kama serikali. Sote hapa tuna Spika Mstaafu Mhe. Ali Khamis Ali ambaye alikuwa Spika kabla ya Mhe. Pandu Ameir Kificho, sote kwenye Kamati ya Uongozi ya Baraza la Wawakilishi tukasema jamani mheshimiwa wetu huyu, mzee wetu anaishi katika mazingira magumu, tukawatuma viongozi wetu wakenda wakaonana na Mhe. Rais kwa ajili ya kuweka mazingira ya kuheshimu utumishi wa Spika Mstaafu aliyepita, wazo lilitoka hapa Barazani.

Sasa inapokuwa kwamba jambo lolote lazima tupendekeze sisi peke yetu wengine wakipendekeza inakuwa mashaka mimi nadhani sio utaratibu mzuri.

Mhe. Spika, kwa sababu mengi yamesemwa na yameshazungumzwa mimi vile vile si miongoni mwa mwakilishi wa wananchi niliyechakuliwa niliyepigiwa simu, ila kama kawaida yangu nilipofika ofisini nikakuta wananchi wangu wanakuja kunieleza yao wanayotaka mimi niwasaidie, hao nimewakuta, wametaka niwasaidie hawajanambia mambo mengine. Kwa sababu hiyo na kwa sababu ya kuuelewa vyema mswada huu, na kwa sababu pendekezo la kuweka *percentage* ya kumpa uwezo rais inazingatia masuala ya kuangalia hali ya uchumi wetu, mimi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa na kutuwezesha kuendesha mijadala yetu kwa salama na afya.

Mhe. Spika, chombo chetu hiki cha Baraza la Wawakilishi ni chombo kikubwa chenye hadhi, chenye kuheshimiwa, chenye sifa kubwa ndani na nje. Hayo yote Mhe. Spika, yanatokana na vitendo, nidhamu na mijadala inayoendeshwa na Wajumbe wa Baraza hili tukufu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, heshima hiyo inabidi tuienzi na tuiendeleze, tutakapofanya vyenginevyo tutakishushia hadhi chombo hiki kitukufu, tutaondosha imani ya wananchi juu ya chombo hiki. Wananchi wetu wanatutumainia sana, wanalitegemea sana Baraza hili litoe muongozi kwa uongozi wa nchi hii. Kwa hivyo, kitendo chochote kitakachodhalilisha Baraza hili tutakuwa tumerudisha nyuma hadhi na heshima ya Baraza hili.

Hivyo basi, ni vizuri sote kwa umoja wetu matendo yetu, maneno yetu, na kila tunachokisema katika Baraza hili tuwe waangalifu tukijua kwamba ndio kioo cha nchi yetu na matumaini ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, linalotoka hapa linakuwa ndio muongozo wa nchi yetu na watu wetu wako makini sana na kwa utulivu mkubwa wanatusikiliza, wanatupima, wanatutazama tunayoyafanya hapa. Naomba sana Mhe. Spika, tuendelee kukipa heshima chombo hiki, tuendelee kuwa na lugha zitakazowapa matumaini wananchi wetu, zitakazojenga nchi yetu, tukikosea lugha zetu Mhe. Spika, tutasababisha malimbano kati ya serikali na wananchi kitu ambacho kitasababisha matatizo makubwa sana katika nchi yetu.

Kwa hivyo, ni vyema sana tunayoyasema katika chombo hiki tukayatambua na yawe ndio dira na mwelekeo na matumaini ya watu wetu. Hivyo Mhe. Spika, nakuomba wewe nawaomba na wawakilishi wenzangu wote wakati wote tuwe na hadhari na nia njema ya kuwatumikia watu wetu kwa maslahi ya nchi yetu. Hakuna jambo muhimu kama kuwepo maelewano makubwa kati ya serikali na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Watu wetu wanaelewa kwamba kutakapotokea mvutano wowote au mgongano wowote kati ya serikali na Wajumbe wa Baraza lako tukufu basi huo ni mtihani mkubwa kwa nchi yetu.

Kwa hivyo, serikali inapoamua kuleta mswada wake Barazani kwa nia njema kabisa unahitajika kuchangiwa kwa nia njema na huo ndio utamaduni wetu na ndio uliotufanya tukafika hapa tulipofika leo Mhe. Spika. Hivyo nawaomba sana Wawakilishi wenzangu tuendelee kukaa pamoja kati yetu Waheshimiwa Wawakilishi na serikali yetu na kila jema ambalo serikali yetu imekusudia kulileta mbele ya chombo hiki kitukufu basi tukiunge mkono kwa nia ile ile njema na pale penye kukosolewa tukosolewe kwa hoja za msingi ili tujenge taifa letu kwa ajili yetu na vizazi vijavyo.

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya mswada huu ni kuwasilisha mapendekezo ya kufuta sheria Nam. 4 ya mwaka 1988 inayohusu malipo ya kustaafu kwa viongozi maalum wa kitaifa na sheria Nam. 6 ya mwaka 1999

inayohusu malipo ya kustaafu kwa viongozi wa kisiasa na kuweka sheria moja inayozingatia mafao ya viongozi wa kisiasa.

Mheshimiwa sheria hii singeni kwetu, wenzangu wengi wameeleza. Wale wenzangu tuliokuwa pamoja mwaka 2003 ambao wengi wetu leo tupo hapa tuliipitisha sheria hii. Tuliipitisha tukiamini kuwa ina maslahi kwa taifa letu na inajenga utamaduni wetu wa Wazanzibari wa kuwa na nidhamu kwa viongozi wetu na kuwahakikishia heshima viongozi wetu ili kuwapa uwezo wasaidie katika kuendelea kuiongoza nchi yetu katika kutoa michango ya kuongoza nchi yetu na kwa kushirikiana, kusaidiana katika uzoefu walioupata.

Mhe. Spika, sheria hii iliyokuja haina tofauti yoyote na sheria ambazo tumezipitisha huko nyuma kwa nia moja tu ya kuweka maslahi ya taifa letu mbele. Kwa hivyo, lengo la mabadiliko ya sheria hii kwanza ni kudhibiti matumizi na sio kuongeza matumizi kama ilivyosemwa na wengi wetu, kama msingi ni huo Mhe. Spika, hapana shaka yoyote serikali ilikuwa na nia nje ya kuileta sheria hii.

Sababu ya pili Mhe. Spika, ni kukidhi matakwa ya kikatiba, kwa kuwa wenzetu wawili hawa Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais katika sheria hii zile za mwanzo zilikuwa wao hawamo bali pale tulikuwa tunatambua Waziri Kiongozi. Ili wenzetu hawa kama miongoni mwa viongozi wakuu wa taifa letu nao tuweze kuwapa haki yao ambayo sote tunaipata.

Kwa msingi huo Mhe. Spika, sheria hii nia yake kubwa ni kurekebisha pale ambapo pana kasoro. Kwa hivyo, sioni sababu hata kidogo ya kusema sheria hii ni ya dhulma, sheria hii ya kibaguzi, sheria hii ni ya kutajirisha wenzetu.
Mhe. Spika, sheria hii nia yake ni kudhibiti matumizi, nia yake ni kukidhi matakwa ya katiba.

Mhe. Spika, viongozi wetu wanaotuongoza kuanzia Rais wetu, Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais mishahara yao ni midogo sana. Katika ukanda huu wa Afrika Mashariki viongozi wetu hawa ndio wana mishahara midogo kuliko nchi yoyote nyengine. Mhe. Spika, ni ujasiri tu wa rais wetu kwa kuwa yuko tayari kuwatumikia wananchi wenzake, lakini maslahi aliyokuwa akiyapata kama Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni makubwa zaidi kuliko maslahi anayoyapata akiwa Rais wa Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kuja hapa tukasema kwamba sheria hii nia yake ni kuwatajirisha wenzetu ukweli hatuwatendei haki viongozi wetu wakubwa hawa

ambao nia yao na moyo wao ni kutumikia. Jambo la msingi ni kuwapa moyo na kuwaunga mkono ili watumikie vizuri kwa maendeleo na umoja wa nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi naomba sana wajumbe wenzangu tuunge mkono sheria hii ili wananchi wetu waelewe *commitment* yetu juu ya uongozi wa nchi hii. Kufanya vyenginevyo Mhe. Spika, tutawavunja moyo sana wananchi wetu.

Mhe. Spika, viongozi wetu hawa wamejitolea kabisa kutusaidia kuongoza nchi yetu, viongozi walioko madarakani na viongozi wetu wastaafu. Ijapokuwa wamemaliza shughuli zao kikazi lakini kila saa tunakwenda kutafuta ushauri, tunakwenda kuchukua uzoefu wao, wanatusaidia katika mambo mbali mbali ya kuendesha vizuri nchi yetu ili iwe na manufaa makubwa zaidi, ili tuimarishe uchumi wetu vizuri zaidi tuondoe matatizo yaliyo mbele yetu.

Sasa Mhe. Spika, tunapowahudumia kwa mambo madogo madogo sioni kama kuna kosa lolote. Maana mambo haya hayafanyiki hapa Zanzibar tu Mhe. Spika, ni mambo yanayofanyika ulimwengu mzima. Nataka niseme kiwango chote hichi leo tunachoona kikubwa hakuna nchi yoyote inayowalipa viongozi wao wastaafu kiwango hichi, wote wanapata zaidi ya kiwango hichi. Kwa hivyo, kusema wao wanadhulumu, wao wanatajirika tunawadhalilisha Mhe. Spika na wananchi wetu wanatusikia.

Kwa hivyo, nawaombeni Waheshimiwa Wajumbe tumefikia hatua kubwa tumejenga umoja katika nchi yetu, njia ya pekee ya kunusuru hili ni kuendeleza umoja wetu kati ya serikali na *backbenchers*. Kufanya vyengine vyovyote wananchi wetu wa nchi hii hawatotuelewa.

Mhe. Spika, hili lililozungumzwa la matumizi makubwa wenzangu wengi wamelieleza na hii *formula x* dhamira yake ilikuwa njema sana. Dhamira ya serikali yetu ni kwamba sasa kila mwaka kadri ya uwezo wetu utakavyoruhusu ni kuongeza mishahara ya watumishi wa umma na viongozi wa kisiasa. Kama dhamira ni hiyo ndio maana tukaweka hii *formula x* kuondosha ile asilimia 100 kwa nia nzuri tu ili tuweze kumudu pale ambapo tutafikia wakati wa kustaafu.

Mhe. Spika, chochote tutakachokimudu haturudi nyuma ni ya kuongezeka kwenda mbele, sasa sioni sababu hata kidogo tuje tuvutane kwa mambo ambayo nia yetu ni njema. Ilikuwa sote tuungane mkono ili tufikie pahala pazuri na wananchi wetu waone ukomavu wetu na uadilifu wetu katika uongozi wa nchi hii.

Mhe. Spika, yamesemwa mambo kwamba serikali hii haikujali watumishi wengine na imetazama sana maslahi ya wakubwa. Mhe. Spika, wenzangu

walionitangulia walieleza kwamba serikali katika kipindi kisichokuwa kirefu imejaribu kuongeza mishahara kuanzia asilimia 25 mpaka asilimia 60 na hivi sasa watumishi wetu wengi wanashukuru na wanapongeza serikali yao. Pia imewawezesha wataalam wetu kuwa tayari kufanya kazi katika kada mbali mbali na kuwa tayari kutumikia nchi yao, wale wengi ambao walikuwa hawako tayari kukaa na kufanya kazi hapa Zanzibar sasa wameamua kurudi na kufanya kazi katika kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, hatua zimechukuliwa na Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban alieleza mambo mbali mbali hapa ambayo serikali inayafanya katika kuimarisha na kujenga maslahi ya watu wetu, kujenga uchumi wa watu wetu bila ya ubaguzi wa aina yoyote ili tuwe taifa moja, tuwe watu wamoja wenye mashirikiano na kuangalia maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu na kuwaomba sana wawakilishi wenzangu wauunge mkono mswada huu na vile vile turudishe nidhamu na heshima ya Baraza hili. Mhe. Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo): Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi, nataka niseme wenzangu wametoa ufafanuzi katika maeneo mengi sana na mimi nilikuwa na maeneo mengi lakini kila lililokuwa limeshazungumzwa nilikuwa natia *tick* kwamba hili limekwisha. Lakini ninayo kidogo kama matatu manne naomba na mimi niyatolee ufafanuzi kidogo.
Mhe. Spika, la kwanza nimesikia baadhi ya wajumbe hapa wakinukuu Katiba ya Zanzibar kifungu cha 35(1) naomba nikisome.

Kifungu cha 35(1):

> "Rais atapokea mshahara na posho na anapostaafu atapata malipo ya uzeeni, kiinua mgongo au posho kama itakavyoamuliwa na Baraza la Wawakilishi."

Mhe. Spika, nataka niwanasihi sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu tuwe tunasoma, bila ya kusoma hichi chombo kitapoteza heshima. Mwaka 1996 naomba waende wakatafute *hansard*, aliyekuwa Waziri wa Nchi (AR) Ikulu kwa utafiti wangu alikuwa Balozi Mohammed Ramia, alileta azimio humu ndani ya Baraza na kuomba Baraza lako tukufu suala hili likasimiwe Baraza la Mawaziri, Baraza la Mapinduzi yaani Serikali na azimio likapitishwa. Hatuielewi hiyo hansard, naomba sana wenzangu wakasome *hansard*. Unapoleta Azimio la Baraza sio wewe Juma, Kombo na azimio likapitishwa, likaungwa mkono na makofi likapigiwa kwamba Baraza la Mapinduzi sasa

limeachiwa litengeneze mishahara ya Rais na maposho yake. Leo tunakuja kuhoji mambo yetu wenyewe nasema tusome sana Mhe. Spika.

Lakini la pili Mhe. Spika, sheria hizi mbili zimepitishwa na Baraza lako tukufu na hicho kinachozungumzwa asilimia 80, asilimia 50 kipo kwenye sheria zile za mwanzo. Kinachofanyika hapa Mhe. Spika, ni kuziunga tu na kuangalia pale ambapo hapaendi sambamba na hali yetu ya kiuchumi ndipo ambapo tumekubali hapa kuleta ili yafanyiwe marekebisho.

Mhe. Spika, nataka ninukuu na nitatoa ulinganisho. Leo Rais Mstaafu ana walinzi, wasaidizi kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea sisi wenyewe, kumi na moja wapo hawa. Narudia ana walinzi, wasaidizi, hawa askari wote FFU kumi na moja anao Rais Mstaafu. Ukijumuisha yeye na *First Lady* Mstaafu chukua hao wawili tu kumi na tatu tunawapa milioni 4 kwa mwezi sio milioni 37 zilizozungumzwa. Hizi milioni 4 wanakula watu 13 kwa mwezi sio milioni 37, ndio nikasema tunapofanya ufafanuzi, tunapozungumza na wananchi tuwe tuna uhakika na tunachokizungumza.

Wananchi wameshangaa kama Rais Mstaafu kwa mwezi mnampa milioni 37 kumbe anapewa milioni 4 tu, milioni 4 ukigawa kwa siku kwa mtu ni shilingi elfu kumi milo tatu, chai ya asubuhi, chakula cha mchana, chakula cha usiku. Huwezi ukawaondosha wale walinzi na wahudumu pale. Mhe. Spika, mimi kazi yangu kuweka sawa tu.

Mhe. Spika, la pili tumeitoa hii *housing allowance* tunayompa Rais Mstaafu kwa mwezi ni shilingi 640,000/= ndio kwa maana nyumba zote za Marais Wastaafu zina ukungu, utafanya nini shilingi 640,000/=. Wawakilishi tunapewa shilingi 400,000/= huo ndio uwezo wetu. Mimi nimekaa pale miezi 13 sasa hivi Waziri wa Fedha hakuja Rais Mstaafu hata mmoja kulalamika. Hatupiti sisi majumba ya marais tukayaona hali yao, tumewapa hizi pesa ku-*maintain* zile nyumba zao angalau mgeni atakapokwenda aone hali ya Rais Mstaafu kwamba na sisi tunamsaidia. Mhe. Spika, mimi nina utamaduni wa kukarabati nyumba yangu hazinitoshi hizi. Hawa wote wanaopiga makofi hawana utamaduni huo.

Mhe. Spika, jengine Rais Mstaafu tunamlipa mafuta kiwango kimoja na Waziri shilingi 1,242,000/= hizi hesabu nilizonazo. Hatuwezi kusema tukiwasaidia hawa ndio uchumi wa nchi utaporomoka hapana hawa tunaowazungumza ni 9 tu lakini wawakilishi tupo 81 humu ndani. Ndio ile x inayopigiwa kelele watu hawataki ikae x. Hakuna cha kinachowasaidia humu ndani ni kidogo mno na hawa wameridhika kwa sababu ya hali yetu ya uchumi. Leo mnataka Rais Mstaafu wa Zanzibar aje awe anapiga virungu. Maana yake wapo Wabunge

Wastaafu, Wawakilishi Wastaafu, Mawaziri Wastaafu wanapiga virungu sasa hivi, mnataka na hawa jamani waje wapige virungu hiyo itakuwa si stahiki.

Mhe. Spika, nawaomba sana wenzangu wawakilishi huu mswada sio mbaya hata kidogo. Kama kuna kitu tunataka kukirekebisha kazi ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Spika, ni kurekebisha kupitia vifungu, tunakwenda kifungu unarekebisha.

Mhe. Spika, mimi nina *hansard* hapa ya Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, huyu ni sahibu yangu mkubwa sana. Anasema watu wake wa Kitope wamemwambia asiunge mkono mswada huu, hawa watu wa Kitope nawaambia mswada huu utamuingiza mtu wao mwengine wa Kitope. Usipopita mswada huu Mhe. Balozi Seif Ali Iddi hayumo. Sasa watwambie ukipita huu mswada Mhe. Makame Mshimba Mbarouk yumo, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi yumo, usipopita huu mswada Mhe. Balozi hayumo, Mhe. Mshimba yumo.

Mhe. Spika, mimi nataka nimalizie kwa kusema kwamba serikali hii imefanya mambo mengi sana na inawajali wananchi wake. Mimi nitakapoona hali yetu ya fedha hairuhusu ndio wa kwanza nitakayekwenda kumwambia Rais hairuhusu tubadilishe sheria hii. Lakini leo Mhe. Spika, kwa takwimu hizi nilipoziona mimi tunazolipwa sasa hivi nimekwenda kuzichukua kwa Mhasibu Mkuu leo asubuhi. Si mambo ya kupigishana kelele na tusomeni takwimu tatu nne hapo, hakuna kikubwa tunachowapa hawa wazee, tunawasaidia ili na wao waweze kuishi, tunawasaidia ili na wao wasije wakatupiga virungu.

Mhe. Spika, naomba sana tuiunge mkono na mimi naiunga mkono asilimia mia na ninasema nauunga mkono mswada huu na nawaomba sana wananchi wa Zanzibar wauunge mkono mswada huu wote tusipotoshwe. Nawaomba sana wananchi wa Kitope watafakari, kama mmoja apate, mmoja asipate huo si usawa, hiyo sio haki. Mhe. Spika, naunga mkono mswada.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote, nafikiri tumeuchangia mswada vya kutosha kabisa kwa wajumbe wote *backbenchers* pamoja na mawaziri. Muda umemalizika na shughuli nyengine ya majumuisho haiwezi ikafanyika leo. Kwa maana hiyo basi, niahirishe kikao hichi mpaka kesho tarehe 20/01/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 20/01/2012 saa 3:00 asubuhi)